


SALA YA JIONI



LONDON
SOCIETY OF SS. PETER AND PAUL
LIMITED
WESTMINSTER HOUSE
GREAT SMITH STREET



Kabla ya Sala.

Utujalie, tunakusihi, Mwenyiezi Mungu, tuku-abudu kwa mioyo safi. Kwa Kristo Bwana wetu. *Amin.*

Bwana Kristo, nataka kuitoa kwako sala hii. Uikubali, ukaipeleke mbele za Baba yetu wa mbinguni pamoja na sala zako ulizotoa duniani ; na sala za Watakatifu wako huko mbinguni. *Amin.*

Baada ya Sala.

Uikubali, Bwana, sala yetu ; utusamehe makosa yetu. Kwa Kristo Bwana wetu. *Amin.*

Neema ya Bwana Yesu Kristo, na pendo la Mungu, na ushirika wa Roho Mtakatifu, ukae nasi sote sasa na milele. *Amin.*

SALA YA JIONI

Kwa Jina la Baba na Mwana na Roho Mtakatifu. *Amin.* Baba yetu. Salamu, Mariamu.

✓. Ee Mungu, utuokoe kwa haraka.

R7. Ee Bwana, utusaidie hima.

✓. Utukufu una Baba, na Mwana : na Roho Mtakatifu.

R7. Ulivyokuwa mwanzo : ulivyo sasa, utakavyokuwa milele. *Amin.*

✓. Msifuni Bwana.

R7. Jina la Bwana lisifiwe.

ZABURI na *Antifona zake.*

SOMO LA KWANZA.

UIMBO WA KANUNI, *pamoja na ✓. na R7.*

MAGNIFICAT na *Antifona yake.*

Antifona iliyokhusika.

Magnificat.

1. Moyo wangu wamwadhimisha Bwana :
Roho yangu yamfurahia Mungu, Mwo-kozi wangu.
2. Kwa kuwa ameutazama :
Unyonge wa mjakazi wake.
3. Kwa maana hakika, tokea leo :
Vizazi vyote wataniita kheri.
4. Kwa kuwa aliye hodari amenitendea makuu :
Na Jina lake ni takatifu.

Sala ya Jioni

5. Na rehema zake vizazi hatta vizazi :
Kwao wanaomcha.
6. Ameterenda nguvu kwa mkono wake :
Amewatawanya walio na kiburi katika
mioyo yao.
7. Amewashusha wakuu katika viti :
Amewakweza wanyonge.
8. Wenye njaa amewashibisha mema :
Wenye mali amewaondoa mikono
mitupu.
9. Kwa kukumbuka rehema :
Amemsaidia Israeli mtumishi wake.
10. Kwa jinsi alivyowaambia baba zetu :
Ibrahimu na uzao wake, hatta milele.

Utukufu.

Antifona iliyokhusika.

SOMO LA PILI.

DEUS MISEREATUR *na Antifona yake.*

*Ant. Njia yako ijulike duniani : wokofu wako
kati ya mataifa yote. (Halleluya.)*

Deus misereatur.

1. Mungu atufadhili na kutubariki :
Na kutuangazia uso wake.
2. Njia yako ijulike duniani :
Wokofu wako kati ya mataifa yote.
3. Watu na wakushukuru, Ee Mungu :
Watu wote wakushukuru.
4. Mataifa na wafurahi :
Naam, waimbe kwa furaha.

Sala ya Jioni

5. Maana utawahukumu watu kwa haki :
Na kuwaongoza watu walioko duniani.
6. Watu na wakushukuru, Ee Mungu :
Watu wote wakushukuru.
7. Inchi imetoa mazao yake :
Mungu, Mungu wetu, atatubariki.
8. Mungu atatubariki :
Ncha zote za dunia zitamcha Yeye.

Utukufu.

*Ant. Njia yako ijulike duniani : wokofu wako
kati ya mataifa yote. (Halleluya.)*

SALA ZA KANUNI.

Ÿ. Bwana akae nanyi.

R7. Akae na roho yako.

Tuombe.

SALA YA SIKU.

SALA ZA UKUMBUSHO, *kama zipo, pamoja na*
Ant. Ÿ. na R7.

Ukumbusho wa Watakatifu wote.

*Ant. Bikira Mariamu, Mama mbarikiwa wa
Mungu : na Watakatifu wote, watuombe kwa
Mungu.*

Ÿ. Mungu amewatukuza Watakatifu wake.

R7. Walipomwita akawasikia.

Tuombe.

SALA.

Sala ya Jioni

Ÿ. Bwana akae nanyi.

R7. Akae na roho yako.

Ÿ. Tumhimidi Bwana.

R7. Tumshukuru Mungu.

Roho za waaminifu kwa rehema ya Mungu
wastarehe katika amani.

R7. *Amin.*

MAOMBEZI.

(*Ant. Utuokoe*, Ee Bwana, tulipo macho, tula-
lapo utulinde; tukeshe na Kristo, tukastarehe
kwa amani.

Ÿ. Utulinde, Ee Bwana, kama mboni wa
jicho.

R7. Utufiche chini ya uvuli wa mbawa zako.

Tuombe.

SALA.)

Baba yetu.

Msaada wa Mungu ukae nasi daima.

R7. *Amin.*



ANTIFONA ZILIZOBADILIKA ZA ZABURI.

(1) S. B. za Majilio.

Ant. Haya, killa aonae kiu, njoni majini :
mtafuteni Bwana maadam anapatikana. Halle-
luya.

(2) Kuzaliwa Bwana.

Ant. Mfalme wa amani ametukuzwa : kuliko
wafalme wote wa dunia. Halleluya.

(3) Ufunuo wa Bwana.

Ant. Nuru utokae Nuru, umeonekana, Ee
Kristo : kwako Mamajusi walileta tunu. Halle-
luya.

(4) S. B. za Kwaresima.

Ant. Ee Mungu, uniumbie moyo safi : uifanye
upya roho yangu ndani yangu.

(5) S. B. ya Mateso, na ya Mitende.

Ant. Uniponye na adui zangu, Ee Mungu
wangu : uniponye nao wafanyao maovu.

(6) Alkhamisi ya Amri, na Ijumaa Kuu.

Ant. Nitakipokea kikombe cha wokofu :
nitalitangaza Jina la Bwana.

(7) Mkesha wa Pasaka.

Ant. Halleluya, Halleluya : Halleluya.

Antifona za Zaburi

(8) Siku Kuu ya Pasaka.

Ant. Malaika akajibu, akawaambia wale wanawake : Msiogope ninyi ; kwa maana najua ya kuwa mnamtafuta Yesu. Halleluya.

(9) Wakati wa Pasaka.

Ant. Halleluya, Halleluya : Halleluya.

(10) Kupaa kwa Bwana.

Ant. Huyu Yesu aliyechukuliwa kutoka kwenu kwenda juu mbinguni : atakuja jinsi hiyo hiyo. Halleluya.

(11) Pentekote.

Ant. Nitamwomba Baba, nae atawapa Mfariji mwingine : Roho ya kweli. Halleluya.

(12) Utatu Mtukufu.

Ant. Utukufu una Wewe, Utatu ulio Uungu umoja : tangu milele, na sasa, na hatta milele.

(13) Mwili Mt. wa Kristo.

Ant. Kuhani wa milele kwa mfano wa daraja la Melkizedeki, Kristo aliye Bwana : alileta mkate na divai. Halleluya.

(14) Moyo Mt. wa Bwana.

Ant. Jifunzeni kwa mfano wangu : kwa kuwa Mimi ni mpole na moyo wangu umenyenyekea.

(15) Kutabaruku Kanisa.

Ant. Nyumba yangu itaitwa nyumba ya sala : kwa mataifa yote.

Antifona za Zaburi

(16) Siku Kuu ya Mariamu Mb.

Ant. Tazama, mimi mjakazi wa Bwana : na iwe kwangu kwa neno lako.

(17) Siku Kuu ya Mtume.

Ant. Amri yangu ndio hii, mpendane : kama nilivyowapenda ninyi.

(18) Siku Kuu ya Mtakatifu.

Antifona za kawaida.

(19) Siku Kuu ya Malaika.

Ant. Mhimidini Bwana : enyi Malaika zake.

(20) Yusuf, Mtunza Bwana wetu.

Ant. Malaika wa Bwana alimtokea Yusuf, akisema : Yusuf, mwana wa Daudi, usikhofu kumchukua Mariamu, mke wako.

(21) Marko, Mtunga Injili.

Ant. Ufalme wa mbinguni ndio makao ya Watakatifu, Halleluya : na raha yao ya milele. Halleluya.

(22) Kuzaliwa kwa Yohana Mbatizaji.

Ant. Atatangulia mbele ya uso wake, mwenye roho ya Eliya, na nguvu zake : illi kumfanyia tayari Bwana watu waliotengenezwa.

(23) Mitume wabarikiwa Petro na Paolo.

Ant. Wewe ndiwe Petro : na juu ya mwamba huu nitalijenga Kanisa langu.

Antifona za Zaburi

(24) Damu iliyo ya thamani ya Bwana.

Ant. Amevikwa vazi lililochovywa katika damu : na Jina lake aitwa Neno la Mungu.

(25) Mariamu (*wa Magdala*), mwenye toba.

Ant. Amesamehewa dhambi zake zilizo nyingi : kwa kuwa amependa sana.

(26) Kung'aa kwa Bwana wetu.

Ant. Yesu aliwachukua Petro na Yakobo na Yohana ndugu yake, akawaleta juu ya mlima mrefu peke yao : akageuka sura yake mbele yao.

(27) Jina Takatifu, Yesu.

Ant. Toka maawio ya jua hatta machweo yake : Jina la Bwana husifiwa.

(28) Kukatwa kichwa kwa Yohana Mbatizaji.

Ant. Herode alimkamata Yohana : akamfunga gerezani kwa ajili ya Herodias, mke wake.

(29) Msalaba Mtakatifu.

Ant. Imetupasa kujisifia : Msalaba wa Bwana wetu Yesu Kristo.

(30) Watakatifu wote.

Ant. *Msifuni Bwana*, enyi wateule wake : ziadhimisheni Siku Kuu zake zenye furaha.

ANTIFONA, V̄. NA R̄. ZA SALA ZA UKUMBUSHO.

(1) Siku ya Bwana.

Ant. *Twakushukuru*, Ee Mungu, twakushukuru : Utatu uliye Umoja khalisi, Uungu umoja usio mfano, Umoja uliye mmoja, Mtakatifu.

V̄. Sala yangu ipae, Ee Bwana.
R̄. Mbele zako kama uvumba.

(2) Mariamu Mb.

Ant. *Vizazi vyote* wataniita kheri : kwa kuwa Mungu ameutazama unyonge wa mjakazi wake. Halleluya.

V̄. Salamu, Mariamu, umejaa neema.
R̄. Bwana yu pamoja nawe.

(3) Mtakatifu. (*Sala ya Jioni ya 1.*)

Ant. *Wamevikwa* mavazi meupe, wakilia kwa sauti kuu, wakisema : Wokofu una Mungu wetu, aketiye katika kiti cha enzi, na Mwana Kondoo.

V̄. Shangilieni, enyi wenye haki.
R̄. Pigeni vigelegele vya furaha.

(4) Mtakatifu. (*Sala ya Jioni ya 2.*)

Ant. *Ee ajabu* ya utukufu wa ufalme ule! Ndipo wanapofurahi Watakatifu wote pamoja na Kristo : wamevikwa nguo nyeupe, wana-mfuata Mwana Kondoo killa aendako.

V̄. Watakatifu waushangilie utukufu.
R̄. Waimbe kwa sauti kuu vitandani mwao.

(5) Robo Mwaka.

Ant. Mfariji, Roho Mtakatifu, ambae Baba atampeleka kwa Jina langu : Yeye atawafundi-sha yote, na kuwakumbusha yote niliyowa-ambia.

Ƴ. Wote wakajazwa Roho Mtakatifu.

R7. Wakaanza kusema.

(6) Majilio.

Ant. Usiogope, Mariamu, kwa maana ume-pata neema kwa Mungu : tazama, utachukua mimba, utazaa mwana. Halleluya.

Ƴ. Uje, utufanye huru.

R7. Ee Bwana, Mungu wa majeshi.

(7) Kuzaliwa Bwana.

Ant. Utukufu una Mungu juu : katika inchi amani kwa watu aliowaridhia. Halleluya.

Ƴ. Bwana ameujulisha. Halleluya.

R7. Wokofu wake. Halleluya.

(8) Ufunuo wa Bwana.

Ant. Mamajusi walipoiona nyota waka-omezana, Hii ni ishara ya Mfalme mkuu : twende tukamtafute tukampe tunu, dhahabu na uvumba na manemane. Halleluya.

Ƴ. Wote kutoka Sheba watakuja. Halleluya.

R7. Wataleta dhahabu na uvumba. Halle-luya.

(9) Kwaresima.

Ant. Unirehemu, Ee Mungu, kwa kadiri ya fadhili zako : kwa kadiri ya wingi wa rehema zako, uyafute makosa yangu.

Ƴ. Uzifute khatiya zangu zote.

R7. Uifanye upya roho yangu ndani yangu.

(10) Wakati wa Pasaka.

Ant. Aliyesulibiwa amefufuka katika wafu : na kutukomboza sisi. Halleluya.

Ƴ. Semeni katika mataifa. Halleluya.

R7. Bwana ametamalaki. Halleluya.

(11) Kupaa kwa Bwana.

Ant. Ninapaa kwa Baba yangu na Baba yenu : kwa Mungu wangu na Mungu wenu. Halleluya.

Ƴ. Mungu amepaa kwa kelele za shangwe. Halleluya.

R7. Bwana kwa sauti ya baragumu. Halle-luya.

(12) Mwili Mt. wa Kristo.

Ant. Ee karamu takatifu! Twampokea Kristo, twafanya ukumbusho wa mateso yake : mioyo yetu hujazwa neema, twapewa arabuni ya utukufu ujao. Halleluya.

Ƴ. Uliwapa chakula cha mbinguni. Halle-luya.

R7. Ndicho kilicho kitamu. Halleluya.

Sala za Ukumbusho

(13) Moyo Mt. wa Bwana.

Ant. *Walipomjia* Yesu, wakiona ya kuwa amekwisha kufa, hawakumvunja miguu : lakini askari mmoja kwa mkuki alimchoma ubavu, ikatoka marra damu na maji.

✓. Kwa furaha mtateka.

R7. Visimani mwa wokofu.

(14) Kutabaruku Kanisa.

Ant. *Panatisha* namna gani mahali hapa : bila shaka hapa ni nyumba ya Mungu, na huu ni mlango wa mbinguni.

✓. Utakatifu ndio uifaa nyumba yako.

R7. Ee Bwana, milele na milele.

(15) Kuzaliwa kwa Yohana Mbatizaji.

Ant. *Mtoto aliyezaliwa* kwetu ni mkuu kuliko nabii ; kwa khabari zake Mwokozi alinena : Hajaondokea mtu katika wazao wa wanawake aliye mkuu kuliko Yohana Mbatizaji.

✓. Mtoto huyu atakuwa mkuu mbele za Mungu.

R7. Kwa maana mkono wa Bwana u pamoja nae.

(16) Mitume wabarikiwa Petro na Paolo.

Ant. *Wewe ndiwe mchungu kondoo*, mkuu wa Mitume : wewe ulipewa funguo za ufalme wa mbinguni.

✓. Wewe ndiwe Petro.

R7. Na juu ya mwamba huu nitalijenga Kanisa langu.

Maombezi

(17) Damu iliyo ya thamani ya Bwana.

Ant. *Tumeufikilia* mlima Sayuni, na Yesu mwenye kuleta agano jipya : na damu ya kunyunyizwa inenayo mema kuliko ile ya Habil.

✓. Umetukombo, Ee Bwana, kwa damu yako.

R7. Ukatufanya kuwa ufalme kwa Mungu wetu.

(18) Kung'aa kwa Bwana wetu.

Ant. *Wanafunzi* waliposikia, wakaanguka kifudifudi, wakaogopa sana : Yesu akaja, akawagusa, akasema, Ondokeni, msilogope. Halleluya.

✓. Ulionekana mtukufu machoni pa Bwana.

R7. Kwa sababu Bwana amekuvika uzuri.

ANTIFONA, ✓. NA R7. ZA SALA ZA MAOMBEZI

SIKU YA BWANA.

(1) Tumwombee Askofu wetu.

Ant. *Watoto wako* utawafanya kuwa wakuu katika inchi zote.

✓. Ee Mungu, Ngao yetu, uangalie.

R7. Umtazame uso Masihi wako.

(2) Tuwaombee Watu wa hali zote.

Ant. *Fadhili* na masamaha ni kwa Bwana, Mungu wetu, ingawa tumemwasi, wala hatu-kuitii sauti yake.

Ƴ. Utuonee huruma, Bwana.

R7. Kwa kuwa twakutumaini Wewe.

(3) Tumshukuru Mwenyiezi Mungu kwa rehemu zake.

Ant. *Twakushukuru*, Ee Bwana Mungu wetu, twalihimidi Jina lako milele na milele.

Ƴ. Kazi zako zote zitakushukuru, Ee Bwana.

R7. Na Watakatifu wako watakuhimidi.

JUMA A TATU.

(1) Tumwombee Mfalme wetu.

Ant. *Mpe mfalme* hukumu zako, atawaamua watu wako kwa haki.

Ƴ. Ee Bwana, umwokoe mfalme.

R7. Utuitike siku tuitayo.

(2) Tuwaombee Wenye mamlaka wote katika inchi hii.

Ant. *Mungu* ni mwamuzi mwenye haki, naam, Mungu hughadhabika killa siku.

Ƴ. Ubaya wao wasio haki na ukome,

R7. Umwimarisha mwenye haki,

(3) Tuwaombee Wasio dini waikubali.

Ant. *Nalisikia* sauti ya Bwana, ikisema, Nimtume nani? Ndipo nikasema, Mimi hapa, nitume mimi.

Ƴ. Mataifa wataliogopa Jina lako, Ee Bwana.

R7. Na wafalme wote wa dunia utukufu wako.

JUMA A NNE.

(1) Tuwaombee Wakhudumu wa Kanisa.

Ant. *Yapasa* midomo ya kuhani ihifadhi maarifa, tena yawapasa watu kuitafuta sharia kinywani mwake; kwa kuwa yeye ni mjumbe wa Bwana wa majeshi.

Ƴ. Makuhani wako na wavikwe haki.

R7. Watakatifu wako na washangilie.

(2) Tuwaombee Waalimu wote.

Ant. *Matendo yako* na yaonekane kwa watumishi wako, na adhama yako kwa watoto wao.

Ƴ. Neema ya Bwana Mungu wetu iwe juu yetu.

R7. Na kazi ya mikono yetu utufanyie thabiti.

(3) Tuliombee Kanisa la Mungu, lipate amani.

Ant. *Bwana* atawapa watu wake nguvu, Bwana atawabariki watu wake kwa amani.

Ƴ. Utupe amani, Ee Bwana, siku zetu.

R7. Kwa maana hakuna mwingine wa kutu-pigania, illa Wewe, Mungu wetu.

(1) Tuwaombee Watoto wa Shule.

Ant. Nitatia sharia yangu ndani yao, na katika mioyo yao nitaiandika ; nami nitakuwa Mungu wao, nao watakuwa watu wangu.

Ƴ. Kumcha Bwana ndio hekima.

R7. Na kujitenga na uovu ndio fahamu.

(2) Tuwaombee Wanafunzi wa Dini.

Ant. Mtu asipozaliwa kwa maji na Roho, hawezi kuingia ufalme wa Mungu.

Ƴ. Alituokoa kwa rehema yake.

R7. Kwa josho la kuzaliwa kwa pili, na kufanywa upya na Roho Mtakatifu.

(3) Tuwaombee Wagonjwa wetu.

Ant. Bwana ameumba madawa katika inchi, nae amewapa wanadamu maarifa, kusudi atukuzwe kwa ajili ya miujiza yake.

Ƴ. Mwenyewe alitwaa magonjwa yetu.

R7. Na kuchukua maradhi zetu.

ALKHAMISI.

(1) Tumshukuru Mungu kwa kutupa Sakramenti Mbarikiwa.

Ant. Ee karamu takatifu! Twampokea Kristo ; twafanya ukumbusho wa mateso yake ; mioyo yetu hujazwa neema ; twapewa arabuni ya utukufu ujao.

Ƴ. Uliwapa chakula cha mbinguni.

R7. Ndicho kilicho kitamu.

(2) Tuwaombee Walisikiaio neno la Mungu.

Ant. Ee Bwana, dunia imejaa fadhili zako, utufundishe amri zako.

Ƴ. Ee Bwana, utuonyeshe rehema zako.

R7. Utupe wokofu wako.

(3) Tuwaombee Waislamu, wamkubali Bwana Kristo.

Ant. Bwana Mungu wetu ni Bwana mmoja ; nawe mpende Bwana Mungu wako kwa moyo wako wote, na kwa roho yako yote, na kwa nguvu zako zote.

Ƴ. Bwana, Mungu wako, atakuondokeshea nabii.

R7. Msikilizeni Yeye.

IJUMAA.

(1) Tuwaombee Wenye kitubio cha Kanisa.

Ant. Kama ungehesabu maovu, Ee Bwana ; Ee Bwana, nani angesimama ?

Ƴ. Lakini kwako kuna samaha.

R7. Illi uogopwe.

(2) Tuwaombee Wajiwekao tayari kupokea Sakramenti za Kanisa.

Ant. Fumbua macho yetu tuyatazame maajabu yatokayo katika sharia yako.

Ƴ. Wewe ndiwe Mungu ufanyae maajabu.

R7. Uliudhihirisha uweza wako kati ya mataifa.

(3) Tuwaombee Waliobatizwa wadumu kuwa imara.

Ant. Urwe mwaminifu hatta kufa, nami nita-kupa taji ya uzima.

Ƴ. Ee Mungu, utuumbie mioyo safi.

R7. Wala Roho yako Mtakatifu usituondolee.

JUMA A MOSI.

(1) Tuwaombee Wakaao katika mitaa yetu.

Ant. Nitammimina Roho yangu juu ya wazao wako, na baraka yangu juu yao watokao kwako.

Ƴ. Ee Mungu wa majeshi, tunakusihi urudi.

R7. Utazame toka mbinguni, uone, uujilie mzabibu huu.

(2) Tuwaombee Wakaao mbali na kanisa.

Ant. Yu kheri mtu yule umchaguae, na kumkaribisha, akae nyuani mwako.

Ƴ. Wewe usikiae kuomba.

R7. Wote wenye mwili watakuja.

(3) Tuwaombee Wakristo wote.

Ant. Uturudishe, Ee Mungu wa wokofu wetu ; uukomeshe uchungu ulio nao juu yetu.

Ƴ. Uwaokoe watu wako, Bwana.

R7. Ubariki urithi wako.

KWA WAFU.

(4) Tuwaombee Waliofariki katika imani.

Ant. Wa kheri wafu wafao katika Bwana. Naam, asema Roho, wapate kupumzika baada ya taabu zao.

Ƴ. Raha ya milele uwajalie, Ee Bwana.

R7. Na nuru ya daima iwaangaze.

JUMA A TANO YA ROBO MWAKA.

(4) Tuwaombee Maaskofu.

Ant. Watoto wako utawafanya kuwa wakuu katika inchi zote.

Ƴ. Ee Mungu, Ngao yetu, uangalie.

R7. Umtazame uso Masihi wako.

IJUMAA YA ROBO MWAKA.

(4) Tuwaombee Makasisi.

Ant. Kwa Jina lako hufurahi mchana kutwa, na kwa haki yako hutukuzwa.

Ƴ. Makuhani wako na wavikwe haki.

R7. Watakatifu wako na washangilie.

JUMA A MOSI YA ROBO MWAKA.

(4) Tuwaombee Watakaoamriwa Khuduma ya Mungu.

Ant. Utufundishe njia yako, Ee Bwana, tutakwenda katika kweli yako ; utuunge mioyo yetu na kicho cha Jina lako.

Ƴ. Ee Bwana, uwaokoe watumishi wako.

R7. Wanaokutumaini Wewe.

Maombezi

MAOMBEZI MENGINE.

Kuomba chakula siku za kupanda.

Ant. Utupe leo riziki zetu.

☩. Ombeni.

R7. Na mtapewa.

Kushukuru baada ya mavuno.

Ant. Mshukuruni Bwana kwa kuwa yu mwema, kwa maana fadhili zake ni za milele.

☩. Na ahimidiwe Bwana, tangu milele hatta milele.

R7. Watu wote na waseme, Amin. Msifuni Bwana.

Kabla ya Safari.

Ant. Bwana ni mchungu wangu, sitapungukiwa na kitu.

☩. Wakamlilia Bwana katika dhiiki zao.

R7. Akawaponya na shidda zao.

Kushukuru baada ya Safari.

Ant. Na tumshukuru Bwana kwa fadhili zake, na maajabu yake kwa wanadamu.

☩. Akawaongoza kwa njia ya kunyoka.

R7. Wapate kwenda hatta mji wa kukaa.



MABADILIO MENGINE.

S. B. Septuajesima.

Mwisho wa Sala ya Jioni ya 1 ya Septuajesima ☩. na R7. ya mwisho huimbwa hivi.

☩. Tumhimidi Bwana. Halleluya, Halleluya.

R7. Tumshukuru Mungu. Halleluya, Halleluya.

Roho za waaminifu, etc.

Alkhamisi ya Amri na Ijumaa Kuu.

Sala ya Jioni imekatazwa isiimbwe.

Zikiisha sala za siri, inaanzia Zaburi.

UIMBO, ☩. na R7. hapana.

Ikiisha DEUS MISERATUR na Antifona yake, marra husemwa na wote, wakipiga magoti,

Kristo alikuwa mtii hatta mauti, nayo mauti ya msalaba.

Baba yetu (*kimoyomoyo*).

Zaburi 51

(Isemwe na wote pamoja kwa sauti ndogo).

1. Unirehemu, Ee Mungu :

Kwa kadiri ya fadhili zako.

2. Kwa kadiri ya wingi wa rehema zako :

Uyafute makosa yangu.

3. Unioshe kabisa na uovu wangu :

Unitakase dhambi zangu.

4. Maana nimejua mimi makosa yangu :

Na dhambi yangu i mbele yangu daima.

5. Nimekutenda dhambi Wewe peke yako :
Na maovu nimefanya mbele za macho yako.
6. Illi uhesabiwe kuwa una haki unenapo :
Na kuwa safi utoapo hukumu.
7. Mimi naliumbwa katika hali ya uovu :
Mama yangu alinichukua mimba khatiyani.
8. Bali wapendezwa na kweli iliyo moyoni :
Utanijulisha hekima kwa siri.
9. Unisafishe kwa husopo nami nitakuwa safi :
Unioshe nami nitakuwa mweupe kuliko thuluji.
10. Unisikize furaha na shangwe :
Mifupa uliyoiponda ifurahi.
11. Usetiri uso wako usitazame dhambi zangu :
Uzifute khatiya zangu zote.
12. Ee Mungu, uniumbie moyo safi :
Uifanye upya roho yangu ndani yangu.
13. Usinitenge na uso wako :
Wala Roho yako Mtakatifu usiniondolee.
14. Unirudishie furaha ya wokofu wako :
Unitegemeze kwa Roho yako bora.
15. Nitawafundisha wakosaji njia zako :
Na wenye dhambi watarejea kwako.
16. Uniponye na damu za watu, Ee Mungu,
Mungu wa wokofu wangu :
Na ulimi wangu utaiimba haki yako.
17. Ee Bwana, ufunue midomo yangu :
Na kinywa changu kitanena sifa zako.
18. Maana Wewe hupendezwi na dhabihu,
kama sivyo ningeitoa :
Walakini huridhii kafara.
19. Dhabihu za Mungu ni roho iliyovunjika :

- Moyo uliovunjika na kupondeka, Ee Mungu, hutaudharau.
20. Uitendee mema Sayuni kwa radhi yako :
Uzijenge kuta za Yerusalemi.
 21. Ndipo utakapopendezwa na dhabihu za haki :
Na sadaka za kuteketezwa na kafara.
 22. Ndipo watakapotoa ng'ombe :
Juu ya madhbahu yako.

(Isisemwe Utukufu.)

Ndipo hufuata SALA pasipo Bwana akae nanyi wala Tuombe.

Wala baadae wasiongeze neno.

Mkeshwa wa Pasaka.

UIMBO, *Ŷ. na R7. hapana.*

Ŷ. na R7. ya mwisho huimbwa hivi,

Ŷ. Tumhimidi Bwana. Halleluya, Halleluya.

R7. Tumshukuru Mungu. Halleluya, Halleluya.

Baba yetu isemwe na wote, kwa sauti ya kusikika, wangali wamesimama.

Wala baadae wasiongeze neno.

Siku Kuu ya Pasaka.

UIMBO, *Ŷ. na R7. hapana.*

Ŷ. na R7. ya mwisho huimbwa hivi,

Ŷ. Tumhimidi Bwana. Halleluya, Halleluya.

R7. Tumshukuru Mungu. Halleluya, Halleluya.

Roho za waaminifu, etc.

ZABURI SEHEMU A.

SIKU YA BWANA.

Ant. Uniendeshe, Ee Bwana : katika mapito ya maagizo yako.

Zab. II9.

33. Unifundishe, Ee Bwana, njia ya amri zako :
Nami nitaishika iwe thawabu.
34. Unifahamishe nami nitaishika sharia yako :
Nitaitii kwa moyo wangu wote.
35. Uniendeshe katika mapito ya maagizo yako :
Kwa maana nimependezwa nayo.
36. Unielekeze moyo wangu na shuhuda zako :
Wala usielekee tamaa.
37. Unigeuze macho yangu nisitazame visi-
vyofaa :
Unihuishe katika njia yako.
38. Umthubutishie mtumishi wako ahadi yako :
Inayokhusu kicho chako.
39. Uniondolee lawama niogopayo :
Maana hukumu zako ni njema.
40. Tazama, nimeyatamani mausia yako :
Unihuishe kwa haki yako.
41. Fadhili zako zinifikie na mimi, Ee Bwana :
Wokofu wako sawasawa na ahadi yako.
42. Nami nitamjibu neno anilaumuye :
Kwa maana nalitumainia neno lako.
43. Wala usiliondoe neno la kweli kinywani
mwangu kabisa :
Maana nimezingojea hukumu zako.
44. Nami nitaitii sharia yako daima :
Milele na milele.

Zaburi. S. B. A

45. Nami nitakwenda panapo nafasi :
Kwa kuwa nimejifunza mausia yako.
46. Nitazinena shuhuda zako mbele ya
wafalme :
Wala sitaona aibu.
47. Nami nitajifurahisha sana kwa maagizo
yako :
Niliyoyapenda.
48. Na mikono yangu nitayainulia maagizo
yako :
Nami nitazitafakari amri zako.
Utukufu.
Ant. Uniendeshe, Ee Bwana : katika mapito ya maagizo yako.
- Ant. Amri zako, Ee Bwana : zimekuwa nyimbo zangu.*
49. Likumbuke neno ulilomwambia mtumishi
wako :
Kwa sababu umenitumainisha.
50. Hii ndio faraja yangu katika taabu yangu :
Ya kwamba ahadi yako imenihuisha.
51. Wenye kiburi wamenidharau mno :
Sikuji pusha na sharia zako.
52. Nimezikumbuka hukumu zako za kale :
Ee Bwana, nikajifariji.
53. Ghadhabu imenishika kwa sababu ya
wasio haki :
Waiachao sharia yako.
54. Amri zako zimekuwa nyimbo zangu :
Katika nyumba ya ugeni wangu.
55. Wakati wa usiku nimelikumbuka Jina
lako :
Ee Bwana, nikaitii sharia yako.

56. Hayo ndiyo niliyokuwa nayo :
Kwa sababu nimeyashika mausia yako.
57. Bwana ndiye aliye fungu langu :
Nimesema kwamba nitayatii maneno yako.
58. Nimekuomba radhi yako kwa moyo wangu wote :
Unifadhili sawasawa na ahadi yako.
59. Nalizitafakari njia zangu :
Na miguu yangu nalizielekezea shuhuda zako.
60. Nalifanya haraka wala sikukawia :
Kuyatii maagizo yako.
61. Kamba za wasio haki zimenifunga :
Sikuisahau sharia yako.
62. Katikati ya usiku nitaamka nikushukuru :
Kwa sababu ya hukumu za haki yako.
63. Mimi ni mwenzi wa wote wakuchao :
Na wao wayatiio mausia yako.
64. Ee Bwana, dunia imejaa fadhili zako :
Unifundishe amri zako.

Utukufu.

Ant. Amri zako, Ee Bwana : zimekuwa nyimbo zangu.

Ant. Rehema zako, Ee Bwana : zinijie nipate kuishi.

65. Umentendea mema mtumishi wako :
Ee Bwana, sawasawa na neno lako.
66. Unifundishe akili na maarifa :
Maana nimeyaamini maagizo yako.
67. Kabla sijateswa mimi nalipotea :
Lakini sasa nimelitii neno lako,

68. Wewe U mwema na mtenda mema :
Unifundishe amri zako.
69. Wenye kiburi wamenizulia uwongo :
Mimi kwa moyo wangu wote nitayashika mausia yako.
70. Mioyo yao imenenepa kama shahamu :
Mimi nimefurahia sana sharia yako.
71. Ilikuwa vyema kwangu kuwa naliteswa :
Nipate kujifunza amri zako.
72. Sharia ya kinywa chako ni njema kwangu :
Kuliko maelfu ya dhahabu na fedha.
73. Mikono yako ilinifanya ikanitengeneza :
Unifahamishe nikajifunze maagizo yako.
74. Wakuchao na wanione na kufurahi :
Kwa sababu nimelingojea neno lako.
75. Najua ya kuwa hukumu zako zina haki :
Ee Bwana, na kwa uaminifu umenitesa.
76. Fadhili zako, nakuomba, na ziwe faraja kwangu :
Sawasawa na ahadi yako kwa mtumishi wako.
77. Rehema zako zinijie nipate kuishi :
Maana sharia yako ni furaha yangu.
78. Wenye kiburi waaibike, maana wamenidhulumu kwa uwongo :
Nitayatafakari mausia yako.
79. Wakuchao wanirudie :
Nao watajua shuhuda zako.
80. Moyo wangu uwe mkamilifu katika amri zako :
Nisije nikaaibika.

Utukufu.

Ant. Rehema zako, Ee Bwana : zinijie nipate kuishi.

JUMA A TATU.

Ant. Bwana akujibu : siku ya dhiiki.

Zab. 20.

1. Bwana akujibu siku ya dhiiki :
Jina la Mungu wa Yakobo likuinue.
2. Akupelekee msaada toka patakatifu pake :
Na kukutegemeza toka Sayuni.
3. Azikumbuke sadaka zako zote :
Na kuzitakabali dhabihu zako.
4. Akujalie kwa kadiri ya haja ya moyo wako :
Na kuyatimiza mashauri yako yote.
5. Na tuushangilie wokofu wako :
Na kwa Jina la Mungu wetu tuzipeze bendera zetu.
6. Bwana akutimizie matakwa yako yote :
Sasa najua ya kuwa Bwana amwokoa Masihi wake.
7. Atamjibu toka mbingu zake takatifu :
Kwa matendo makuu ya wokofu ya mkono wake wa kuume.
8. Hawa wanataja magari na hawa farasi :
Bali sisi tutalitaja Jina la Bwana Mungu wetu.
9. Wao wameinama na kuanguka :
Bali sisi tumeinuka na kusimama.
10. Ee Bwana, umwokoe mfalme :
Utuitike siku tuitayo.
Utukufu.

Ant. Bwana akujibu : siku ya dhiiki.

Ant. Mfalme atazifurahia : nguvu zako, Ee Bwana.

Zab. 21.

1. Mfalme atazifurahia nguvu zako, Ee Bwana :
Na wokofu wako ataufanyia shangwe nyingi sana.
2. Umempa haja ya moyo wake :
Wala hukumzuilia matakwa ya midomo yake.
3. Maana umemsogezea baraka za kheri :
Umemvika taji ya dhahabu safi kichwani pake.
4. Alikuomba uhayi ukampa :
Muda mrefu wa siku nyingi, milele na milele.
5. Utukufu wake ni mkuu kwa wokofu wako :
Heshima na adhama waweka juu yake.
6. Maana umemfanya kuwa baraka za milele :
Wamfurahisha kwa furaha ya uso wako.
7. Kwa kuwa mfalme humtumaini Bwana :
Na kwa fadhili zake Aliye juu hata-ondoshwa.
8. Mkono wako utawapata adui zako zote :
Mkono wako wa kuume utawapata wanaokuchukia.
9. Utawafanya kuwa kama tanuru ya moto :
Wakati wa ghadhabu yako.
10. Bwana atawameza kwa ghadhabu yake :
Na moto utawala.

11. Matunda yao utayaharibu na kuyaondoa katika inchi :
Na wazao wao katika wanadamu.
12. Kwa kuwa walinia kukutenda mabaya :
Waliwaza hila wasipate kuitimiza.
13. Kwa maana utawafanya kukupa kisogo :
Kwa uzi wa upinde wako ukiwaelekezea mishale.
14. Utukuzwe, Ee Bwana, kwa nguvu zako :
Nasi tutakuimba na kuuhimidi uweza wako.

Utukufu.

Ant. Mfalme atazifurahia : nguvu zako, Ee Bwana.

Ant. Ee Bwana, nitakutukuza : maana ume-niinua.

Zab. 30.

1. Ee Bwana, nitakutukuza, maana ume-niinua :
Wala hukuwafurahisha adui zangu.
2. Ee Bwana, Mungu wangu :
Nalikulilia ukaniponya.
3. Umeniinua roho yangu :
Ee Bwana, kutoka kuzimu.
4. Umenihuisha na kunitoa :
Miongoni mwao washukao shimoni.
5. Mwimbieni Bwana zaburi :
Enyi watakatifu wake.
6. Kashukuruni :
Kwa kumbukumbu la utakatifu wake.
7. Maana ghadhabu zake za kitambo :
Katika radhi yake mna uhayi.

8. Labda kilio huja kukaa usiku :
Lakini assubuhi huwa furaha.
9. Nami nilipofanikiwa nalisema :
Sitaondoshwa milele.
10. Wewe, Ee Bwana, kwa radhi yako :
Uliuweka imara mlima wangu.
11. Uliuficha uso wako :
Nami nikafadhaika.
12. Nalikulilia Wewe, Ee Bwana :
Naam, kwa Bwana naliomba dua.
13. Mna faida gani katika damu yangu :
Nishukapo shimoni ?
14. Mavumbi yatakusifu :
Yataitangaza haki yako ?
15. Usikie, Ee Bwana, unirehemu :
Ee Bwana, uwe msaidizi wangu.
16. Uligeuza matanga yangu kuwa machezo :
Ulinivua gunia, ukanivika furaha.
17. Illi utukufu wangu ukusifu :
Wala usinyamaze.
18. Ee Bwana, Mungu wangu :
Nitakushukuru milele.

Utukufu.

Ant. Ee Bwana, nitakutukuza : maana ume-niinua.



JUMA A NNE.

Ant. Mwimbieni Bwana : libarikini Jina lake.

Zab. 96.

1. Mwimbieni Bwana uimbo mpya :
Mwimbieni Bwana, inchi yote.
2. Mwimbieni Bwana, libarikini Jina lake :
Tangazeni khabari njema za wokofu wake killa siku.
3. Wakhubirini mataifa khabari za utukufu wake :
Na watu wote khabari za maajabu yake.
4. Bwana ni mkuu mwenye kusifiwa sana :
Na wa kuogopwa kuliko miungu yote.
5. Maana miungu yote ya watu si kitu :
Lakini Bwana ndiye aliyezifanya mbingu.
6. Heshima na adhama ziko mbele zake :
Nguvu na uzuri zimo katika patakatifu pake.
7. Mpeni Bwana, enyi jamaa za watu :
Mpeni Bwana utukufu na nguvu.
8. Mpeni Bwana utukufu wa Jina lake :
Leteni sadaka mkaziingie nyua zake.
9. Mwabuduni Bwana kwa uzuri wa utaka-tifu :
Tetemekeni mbele zake, inchi yote.
10. Semeni katika mataifa, Bwana ametamalakiki :
Naam, ulimwengu umethubutika usitikisike, atawahukumu watu kwa adili.
11. Mbingu na zifurahi, inchi na ishangilie :
Bahari na ivume na vyote viijazavyo.

12. Mashamba na yapige shangwe na vyote vilivyomo :
Ndipo miti yote ya mwituni itaimba kwa furaha.

13. Mbele za Bwana, kwa maana anakuja :
Kwa maana anakuja aihukumu inchi.

14. Atauhukumu ulimwengu kwa haki :
Na mataifa kwa uaminifu wake.

Utukufu.

Ant. Mwimbieni Bwana : libarikini Jina lake.

Ant. Msifuni Bwana, kwa kuwa yu mwema :
atawahurumia watumishi wake. Halleluya.

Zab. 135.

1. Lisifuni Jina la Bwana :
Sifuni, enyi watumishi wa Bwana.
2. Ninyi msimamao nyumbani mwa Bwana :
Nyuanani mwa nyumba ya Mungu wetu.
3. Msifuni Bwana kwa kuwa Bwana yu mwema :
Liimbeni Jina lake kwa maana lapendeza.
4. Kwa sababu Bwana amejichagulia Yakobo :
Na Israeli, wawe watu wake khassa.
5. Maana najua mimi ya kuwa Bwana ni mkuu :
Na Bwana wetu yu juu ya miungu yote.
6. Bwana amefanya killa lililompendeza :
Katika mbingu na katika inchi.
7. Katika bahari na vilindi vyote :
Ndiye apandishae mvuke toka miisho ya inchi.
8. Huifanyia mvua umeme :
Hutoa upepo katika hazina zake.

Zaburi. J. a 4. A

9. Aliwapiga wazaliwa wa kwanza wa Misri :
Wa wanadamu na wa nyama.
10. Alipeleka ishara na maajabu kati yako,
Misri :
Juu ya Farao na watumishi wake wote.
11. Aliwapiga mataifa mengi :
Akawaua wafalme wenye nguvu.
12. Sihon, mfalme wa Waamori, na Og,
mfalme wa Basani :
Na falme zote za Kanaani.
13. Akatoa inchi yao iwe urithi :
Urithi wa Israeli watu wake.
14. Jina lako, Ee Bwana, ni la milele :
Kumbukumbu lako, Ee Bwana, vizazi
hatta vizazi.
15. Kwa kuwa Bwana atawaamua watu wake :
Atawahurumia watumishi wake.
16. Sanamu za mataifa ni fedha na dhahabu :
Kazi ya mikono ya wanadamu.
17. Zina kinywa lakini hazisemi :
Zina macho lakini hazioni.
18. Zina masikio lakini hazisikii :
Wala hamna pumzi vinywani mwake.
19. Wazifanyao watafanana nazo :
Na killa mmoja anaezitumainia.
20. Nyumba ya Israeli, mhimidini Bwana :
Nyumba ya Haruni, mhimidini Bwana.
21. Nyumba ya Lawi, mhimidini Bwana :
Ninyi mnaomcha Bwana, mhimidini
Bwana.
22. Na ahimidiwe Bwana toka Sayuni :
Akaae Yerusalemi.

Utukufu.

Zaburi. J. a 4. A

Ant. Msifuni Bwana kwa kuwa yu mwema :
atawahurumia watumishi wake. Halleluya.

Ant. Wewe uketiye mbinguni : uturehemu sisi.

Zab. 123.

1. Nimekuinulia macho yangu :
Wewe uketiye mbinguni.
2. Kama vile macho ya watumishi :
Kwa mkono wa bwana zao.
3. Kama macho ya mjakazi :
Kwa mkono wa bibi yake.
4. Ndivyo macho yetu kwa Bwana Mungu
wetu :
Hatta atakapoturehemu.
5. Uturehemu, Bwana, uturehemu sisi :
Kwa maana tumeshiba dharau.
6. Roho zetu zimeshiba mzaha wa wenye
raha :
Na dharau ya wenye kiburi.

Utukufu.

Ant. Wewe uketiye mbinguni : uturehemu sisi.



JUMA A TANO.

Ant. Fadhili zako zipo mbele ya macho yangu :
nami nimekwenda katika kweli yako.

Zab. 26.

1. Unihukumu, Ee Bwana, maana nimekwen-
nda kwa ukamilifu wangu :
Nami nimemtumaini Bwana, sikusita.
2. Unijaribu, Ee Bwana, na kunipima :
Unisafishe mtima wangu na moyo
wangu.
3. Maana fadhili zako zipo mbele ya macho
yangu :
Nami nimekwenda katika kweli yako.
4. Sikuketi pamoja na watu wa ubatili :
Wala sitaingia mnamo wanafiki.
5. Nimelichukia kusanyiko la watenda ma-
baya :
Wala sitaketi pamoja na wasio haki.
6. Nitanawa mikono yangu kwa kutokuwa
na kosa :
Nitazunguka madhbahu yako, Ee Bwana.
7. Nipaaaze sauti ya kushukuru :
Niieneze miujiza yako yote.
8. Ee Bwana, nimependa makao ya nyumba
yako :
Na mahali pa masikani ya utukufu wako.
9. Usitie roho yangu pamoja na wenye
dhambi :
Wala maisha yangu pamoja na watu
wamwagao damu.
10. Mikononi mwao mna madhara :
Na mkono wao wa kuume umejaa
rushwa.

11. Lakini mimi kwa ukamilifu wangu nita-
kwenda :

Unikomboe, unirehemu.

12. Mguu wangu unasimama palipo sawa :
Katika makusanyiko nitamtukuza
Bwana.

Utukufu.

Ant. Fadhili zako zipo mbele ya macho yangu :
nami nimekwenda katika kweli yako.

Ant. Utapendezwa na dhabihu za haki : Ee
Bwana, juu ya madhbahu yako.

Zab. 51.

1. Unirehemu, Ee Mungu :
Kwa kadiri ya fadhili zako.
2. Kwa kadiri ya wingi wa rehema zako :
Uyafute makosa yangu.
3. Unioshe kabisa na uovu wangu :
Unitakase dhambi zangu.
4. Maana nimejua mimi makosa yangu :
Na dhambi yangu i mbele yangu daima.
5. Nimekutenda dhambi Wewe peke yako :
Na maovu nimefanya mbele za macho
yako.
6. Illi uhesabiwe kuwa una haki unenapo :
Na kuwa safi utoapo hukumu.
7. Mimi naliumbwa katika hali ya uovu :
Mama yangu alinichukua mimba khati-
yani.
8. Bali wapendezwa na kweli iliyo moyoni :
Utanjulisha hekima kwa siri.
9. Unisafishe kwa husopo nami nitakuwa safi :
Unioshe nami nitakuwa mweupe kuliko
thuluji.

10. Unisikize furaha na shangwe :
Mifupa uliyoiponda ifurahi.
11. Usetiri uso wako usitazame dhambi zangu :
Uzifute khatiya zangu zote.
12. Ee Mungu, uniumbie moyo safi :
Uifanye upya roho yangu ndani yangu.
13. Usinitenge na uso wako :
Wala Roho yako Mtakatifu usiniondolee.
14. Unirudishie furaha ya wokofu wako :
Unitegemeze kwa Roho yako bora.
15. Nitawafundisha wakosaji njia zako :
Na wenye dhambi watarejea kwako.
16. Uniponye na damu za watu, Ee Mungu,
Mungu wa wokofu wangu :
Na ulimi wangu utaiimba haki yako.
17. Ee Bwana, ufunue midomo yangu :
Na kinywa changu kitanena sifa zako.
18. Maana Wewe hupendezwi na dhabihu,
kama sivyo ningeitoa :
Walakini huridhii kafara.
19. Dhabihu za Mungu ni roho iliyovunjika :
Moyo uliovunjika na kupondeka, Ee
Mungu, hutaudharau.
20. Uitendee mema Sayuni kwa radhi yako :
Uzijenge kuta za Yerusalemi.
21. Ndipo utakapopendezwa na dhabihu za
haki :
Na sadaka za kuteketezwa na kafara.
22. Ndipo watakapotoa ng'ombe :
Juu ya madhbahu yako.

Utukufu.

Ant. Utapendezwa na dhabihu za haki ; Ee
Bwana, juu ya madhbahu yako.

Ant. Wema wa Mungu : upo siku zote.

Zab. 52.

1. Ya nini kujisifia uovu, Ee mdhalimu :
Wema wa Mungu upo siku zote.
2. Ulimi wako watunga madhara :
Kama wembe mkali, Ee mfanya hila.
3. Umependa mabaya kuliko mema :
Na uwongo kuliko kusema kweli.
4. Umependa maneno yote ya kupoteza
watu :
Ee ulimi wenye hila.
5. Lakini Mungu atakuharibu hatta milele :
Atakukamata.
6. Atakupokonya khemani mwake :
Atakung'oa katika inchi ya wahayi.
7. Nao wenye haki wataona :
Wataingiwa na khofu na kumcheka.
8. Kumbe ! huyu ndiye mtu yule :
Asiyemfanya Mungu kuwa nguvu zake.
9. Aliutumainia wingi wa mali zake :
Na kujifanya hodari kwa madhara yake.
10. Bali mimi ni kama mzeituni :
Umeao katika nyumba ya Mungu.
11. Nazitumainia fadhili za Mungu milele na
milele :
Nitakushukuru milele kwa maana ume-
tenda.
12. Nitalingojea Jina lako kwa kuwa li jema :
Mbele ya watakatifu wako.

Utukufu.

Ant. Wema wa Mungu : upo siku zote.

Ant. Toka mbinguni : Mungu aliwachungulia wanadamu.

Zab. 53.

1. Mpumbavu amesema moyoni, Hakuna Mungu :
Wametenda uovu wa ufisadi na kuchukiza, hakuna mtenda mema.
2. Toka mbinguni Mungu aliwachungulia wanadamu :
Aone kama yuko mtu mwenye akili amtafuta Mungu.
3. Killa mtu amepotoka, wameoza wote pamoja :
Hakuna mtenda mema hatta mmoja.
4. Je! wafanyao maovu hawajui :
Walao watu wangu kama walavyo mkate, hawakumwita Mungu.
5. Hapo waliingiwa na khofu pasipokuwa na khofu :
Maana Mungu ameitawanya mifupa yake aliyekuhusuru.
6. Umewatia aibu :
Kwa sababu Mungu amewadharau.
7. Wokofu wa Israeli na utoke katika Sayuni :
Mungu atakapowarudisha wafungwa wa watu wake.
8. Yakobo atashangilia :
Israeli atafurahi.
Utukufu.

Ant. Toka mbinguni : Mungu aliwachungulia wanadamu.

ALKHAMISI.

Ant. Ninyi mnaomtafuta Bwana : mioyo yenu ihuishwe.

Zab. 69.

1. Uniokoe, Ee Mungu :
Maana maji yamefika hatta rohoni mwangu.
2. Ninazama katika matope mengi :
Pasiposimamika.
3. Nimefika maji ya vilindi :
Mkondo wa maji unanigharikisha.
4. Nimechoka kwa kulia kwangu :
Koo yangu imekauka.
5. Macho yangu yamedhoofu :
Kwa kumngoja Mungu wangu.
6. Wanaonichukia burre ni wengi :
Kuliko nywele za kichwa changu.
7. Watakao kunikatilia mbali wamekuwa hodari :
Adui zangu kwa sababu ya uwongo.
8. Ndipo nalilipishwa vitu :
Nisivyovichukua kwa nguvu.
9. Ee Mungu, Wewe unajua upumbavu wangu :
Wala hukufichwa dhambi yangu.
10. Wanaokungoja Wewe wasiaibishwe :
Kwa ajili yangu, Ee Bwana MUNGU wa majeshi.
11. Wanaokutafuta Wewe wasifedheheshwe :
Kwa ajili yangu, Ee Mungu wa Israeli.
12. Maana kwa ajili yako nimestahimili lawama :
Fedheha imenifunika uso wangu.

Zaburi. Alkh. A

13. Nimekuwa mgeni kwa ndugu zangu :
Na mtu wa inchi nyingine kwa wana wa
mama yangu.
14. Maana wivu wa nyumba yako umenila :
Na lawama zao wanaokulaumu zime-
nipata.
15. Nilipolia na kuiadhibu roho yangu kwa
kufunga :
Ikawa lawama juu yangu.
16. Nilipofanya gunia kuwa nguo zangu :
Nikawa methali kwao.
17. Waketio langoni hunisema :
Na nyimbo za walevi hunidhihaki.
18. Nami maombi yangu nakuomba Wewe,
Bwana :
Wakati ukupendezao, Ee Mungu.
19. Kwa wingi wa fadhili zako unijibu :
Katika kweli ya wokofu wako.
20. Uniponye kwa kunitoa matopeni :
Wala usiniache nikazama.
21. Na niponywe nao wanaonichukia :
Na katika vilindi vya maji.
22. Mkondo wa maji usinigharikishe, wala
vilindi visinimeze :
Wala shimo lisifumbe kinywa chake
juu yangu.
23. Unijibu, Ee Bwana, maana fadhili zako ni
njema :
Kwa kadiri ya rehema zako unielekee.
24. Wala usinifiche uso wako mimi mtumishi
wako :
Maana mimi nimo taabuni, unijibu
upesi.

Zaburi. Alkh. A

25. Uikaribie roho yangu, uikomboe :
Kwa sababu ya adui zangu unifikie.
26. Wewe umejua kulaumiwa kwangu na
kuaibika kwangu na kufedheheka
kwangu :
Mbele zako Wewe wako watesi wangu
wote.
27. Lawama imenivunja moyo :
Nami ninaugua sana.
28. Nikangoja aje wa kunihurumia, wala
hakuna mtu :
Na wa kunifaraji, wala sikumwona mtu.
29. Wakanipa uchungu kuwa chakula changu :
Nami nilipokuwa na kiu wakaninyweshwa
siki.
30. Meza yao mbele yao na iwe mtego :
Naam, wakiwa salama na iwe kitu cha
kuwanasa.
31. Macho yao yatiwe giza wasione :
Na viuno vyao uvitetemeshe daima.
32. Umwage ghadhabu yako juu yao :
Na ukali wa hasira yako uwapate.
33. Matuo yao yawe ukiwa :
Pasiwe na mtu wa kukaa khemani mwao.
34. Maana wanamwudhi mtu uliyempiga
Wewe :
Wanasimulia maumivu yao uliowatia
jeraha.
35. Uwaongezee uovu juu ya uovu :
Wala wasiingie katika haki yako.
36. Na wafutwe katika chuo cha uhayi :
Wala pamoja na wenye haki wasiandi-
kwe.

37. Nami niliye maskini na mtu wa huzuni :
Wokofu wako, Ee Mungu, utaniinua.
38. Nitalisifu Jina la Mungu kwa uimbo :
Nami nitamtukuza kwa shukrani.
39. Nayo yatampendeza Bwana kuliko
ng'ombe :
Au ndama mwenye pembe na kwato.
40. Walioonewa watakapoona watafurahi :
Ninyi mnaomtafuta Mungu, mioyo yenu
ihuishwe.
41. Kwa kuwa Bwana huwasikia wahitaji :
Wala hawadharau wafungwa wake.
42. Mbingu na inchi zimsifu :
Bahari na vyote visogeavyo ndani yake.
43. Maana Mungu ataiokoa Sayuni, na kuijenga
miji ya Yuda :
Na watu watakaa ndani yake na kuimi-
liki.
44. Wazao wa watumishi wake watairithi :
Na walipendao Jina lake watakaa humo.
Utukufu.

Ant. Ninyi mnaomtafuta Bwana : mioyo yenu
ihuishwe.

Ant. *Fadhili zako*, Ee Bwana : zafika hatta
mbinguni.

Zab. 36.

1. Kuasi kwake mtu asiye haki hunena
moyoni mwake :
Hakuna khofu ya Mungu mbele ya
macho yake.
2. Kwa maana hujipendekeza machoni pake :
Ya kwamba upotofu wake hautatambu-
likana na kuchukiwa.

3. Maneno ya kinywa chake ni uovu na hila :
Ameacha kuwa na akili na kutenda mema.
4. Huwaza maovu kitandani pake :
Hujiweka katika njia isiyo njema, ubaya
hauchukii.
5. Fadhili zako, Ee Bwana, zafika hatta
mbinguni :
Uaminifu wako hatta mawinguni.
6. Haki yako ni kama milima ya Mungu,
hukumu zako ni vilindi vikuu :
Ee Bwana, unawaokoa wanadamu na
nyama.
7. Ee ajabu ya thamani ya fadhili zako,
Mungu :
Wanadamu huukimbilia uvuli wa mbawa
zako.
8. Watashibishwa kwa unono wa nyumba
yako :
Nawe utawanywesha mto wa furaha
zako.
9. Maana kwako Wewe iko chemchemi ya
uzima :
Katika nuru yako tutaona nuru.
10. Uwadumishie wakujua fadhili zako :
Na wanyofu wa moyo uaminifu wako.
11. Mguu wa kiburi usinikaribie :
Wala mkono wa wasio haki usinifukuze.
12. Huko ndiko walikoanguka wafanyao
maovu :
Wameangushwa chini wasiweze kusi-
mama.
Utukufu.

Ant. *Fadhili zako*, Ee Bwana : zafika hatta
mbinguni.

IJUMAA.

Ant. Usiwe mbali nami maana taabu i karibu :
kwa maana hakuna msaidizi.

Zab. 22.

1. Ee Mungu wangu, Ee Mungu wangu :
Mbona umeniacha ?
2. Mbona U mbali na wokofu wangu :
Na maneno ya kuugua kwangu ?
3. Ee Mungu wangu, nalia mchana lakini
hujibu :
Na wakati wa usiku lakini sipati raha.
4. Na Wewe U Mtakatifu :
Uketiye juu ya sifa za Israeli.
5. Baba zetu walikutumaini Wewe :
Walitumaini na Wewe ukawaokoa.
6. Walikulilia Wewe wakaokoka :
Walikutumaini wala hawakuaibika.
7. Lakini mimi ni mdudu wala si mtu :
Laumu ya wanadamu na mzaha wa
watu.
8. Wote wanionao hunicheka sana :
Hunifyonya wakitikisa vichwa vyao.
9. Umtegemee Bwana, na amponye :
Na amwokoe sasa, maana apendezwa nae.
10. Naam, Wewe ndiwe uliyenitoa tumboni :
Ulinitumainisha nilipokuwa maziwani
mwa mama yangu.
11. Kwako nalitupwa tokea tumboni :
Toka tumboni mwa mama yangu ndiwe
Mungu wangu.
12. Usiwe mbali nami maana taabu i karibu :
Kwa maana hakuna msaidizi.

13. Mafahali wengi wamenizunguka :
Walio hodari wa Bashani wamenisonga.
14. Wanarifumbulia vinywa vyao :
Kama simba apapurae na kunguruma.
15. Nimemwagika kama maji :
Mifupa yangu yote imeteguka.
16. Moyo wangu umekuwa kama nta :
Umeyeyuka ndani ya mtima wangu.
17. Nguvu zangu zimekauka kama gae :
Ulimi wangu waambatana na taya zangu.
18. Unaniweka katika mavumbi ya mauti :
Kwa maana mbwa wamenizunguka.
19. Kusanyiko la waovu wamenisonga :
Wamenizua mikono na miguu.
20. Naweza kuhesabu mifupa yangu yote :
Wao wananitazama na kunikodolea
macho.
21. Wanagawanya nguo zangu :
Na vazi langu wanalipigia kura.
22. Nawe, Bwana, usiwe mbali :
Ee nguvu zangu, fanya haraka kuni-
saidia.
23. Uniponye roho yangu na upanga :
Mpenzi wangu na nguvu za mbwa.
24. Kinywani mwa simba uniokoe :
Naam, toka pembe za nyati umenijibu.
25. Nitalikhubiri Jina lako kwa ndugu zangu :
Katikati ya kusanyiko nitakusifu.
26. Ninyi mnaomcha Bwana, msifuni :
Enyi nyote mlio wazao wa Yakobo,
mtukuzeni, mcheni, enyi nyote mlio
wazao wa Israeli.

27. Maana hakulidharau teso la mteswa :
Wala hakuchukizwa nalo.
 28. Wala hakumficha uso wake :
Bali alipomlilia akamsikia.
 29. Kwako zinatoka sifa zangu :
Katika kusanyiko kubwa.
 30. Nitaziondoa nadhiri zangu :
Mbele yao wamchao.
 31. Wapole watakula na kushiba :
Wamtafutao Bwana watamsifu.
 32. Mioyo yenu na iishi milele :
Miisho yote ya dunia itakumbuka.
 33. Watamrejea Bwana :
Jamaa zote za mataifa watasujudu mbele zake.
 34. Maana ufalme una Bwana :
Nae ndiye awatawalae mataifa.
 35. Wakwasi wote wa dunia watakula na kusujudu :
Mbele zake huinama wote washukao mavumbini.
 36. Naam, yeye asiyeweza hujihuisha roho yake :
Wazao wake watamtumikia.
 37. Zitasimuliwa khabari za Bwana :
Kwa kizazi kitakachokuja.
 38. Nao watawakhubiri watakaozaliwa haki yake :
Ya kwamba ndiye aliyeyafanya.
- Utukufu.


Ant. Usiwe mbali nami maana taabu i karibu : kwa maana hakuna msaidizi.

Ant. Kwa Bwana kuna fadhili : na kwake kuna ukombozi mwingi.

Zab. 130.

1. Toka vilindini nimekulilia, Ee Bwana :
Ee Bwana, uisikilize sauti yangu.
 2. Masikio yako na yaiangalie :
Sauti ya dua zangu.
 3. Kama ungehesabu maovu, Ee Bwana :
Ee Bwana, nani angesimama ?
 4. Lakini kwako kuna samaha :
Illi uogopwe.
 5. Nimemngoja Bwana, roho yangu imengoja :
Na neno lake nimelitumainia.
 6. Roho yangu inamngoja Bwana kuliko walinzi waingojavyo assubuhi :
Naam, kuliko walinzi assubuhi.
 7. Ee Israeli, umtarajie Bwana :
Maana kwa Bwana kuna fadhili.
 8. Na kwake kuna ukombozi mwingi :
Nae atamkomboa Israeli na maovu yake yote.
- Utukufu.

Ant. Kwa Bwana kuna fadhili : na kwake kuna ukombozi mwingi.



JUMA A MOSI.

*Ant. Wanyofu wa moyo wataona na kufurahi :
na wazitafakari fadhili za Bwana.*

Zab. 107.


1. Mshukuruni Bwana kwa kuwa yu mwema :
Kwa maana fadhili zake ni za milele.
2. Na waseme hivi waliokombolewa na
Bwana :
Aliowakomboa na mkono wa mtesi.
3. Akawakusanya kutoka inchi zote :
Toka mashariki na magharibi, toka
kaskazini na kusini.
4. Walitangatanga jangwani katika njia ya
nyika :
Hawakuona mji wa kukaa.
5. Waliona njaa, waliona na kiu :
Roho yao ilikuwa ikizimia ndani yao.
6. Wakamlilia Bwana katika dhiiki zao :
Akawaponya na shidda zao.
7. Akawaongoza kwa njia ya kunyoka :
Wapate kwenda hatta mji wa kukaa.
8. Na wamshukuru Bwana kwa fadhili zake :
Na maajabu yake kwa wanadamu.
9. Maana alishibisha roho yenye shauku :
Na roho yenye njaa alijaza mema.
10. Waliokaa katika giza na uvuli wa mauti :
Wamefungwa katika taabu na chuma.
11. Kwa sababu waliyaasi maneno ya Mungu :
Wakalidharau shauri lake Aliye juu.
12. Hatta akawadhili moyo kwa taabu :
Wakajikwaa wala hakuna msaidizi.

13. Wakamlilia Bwana katika dhiiki zao :
Akawaponya na shidda zao.
14. Aliwatoa katika giza na uvuli wa mauti :
Akayavunja mafungo yao.
15. Na wamshukuru Bwana kwa fadhili
zake :
Na maajabu yake kwa wanadamu.
16. Maana ameivunja milango ya shaba :
Ameyakata mapingo ya chuma.
17. Wapumbavu kwa sababu ya ukosaji wao :
Na kwa sababu ya maovu yao hujitesa.
18. Roho zao zachukia killa namna ya
chakula :
Wakaikaribia milango ya mauti.
19. Wakamlilia Bwana katika dhiiki zao :
Akawaponya na shidda zao.
20. Hulituma neno lake, huwaponya :
Huwatoa katika maangamizo yao.
21. Na wamshukuru Bwana kwa fadhili zake :
Na maajabu yake kwa wanadamu.
22. Na wamtolee dhabihu za kushukuru :
Na kuyasimulia matendo yake kwa
kuimba.
23. Washukao baharini katika merikebu :
Wafanyao kazi katika maji mengi.
24. Hawo wameiona kazi ya Bwana :
Na maajabu yake vilindini.
25. Maana alisema, akaondokesha upepo wa
dharuba :
Ukayainua juu mawimbi yake.
26. Wapanda mbinguni, watelemka vilindini :
Roho yao yayeyuka kwa hali mbaya.

27. Wayumbayumba, wapepesuka kama mlevi :
Akili zao zote zawapotea.
28. Wakamlilia Bwana katika dhiiki zao :
Akawatoa katika shidda zao.
29. Huituliza dharuba ikawa shwari :
Mawimbi yake yakanyamaza.
30. Ndipo wafurahi kwa kuwa yametulia :
Nae huwaleta hatta bandari waliyoi-
tamani.
31. Na wamshukuru Bwana kwa fadhili zake :
Na maajabu yake kwa wanadamu.
32. Na wamtukuze katika kusanyiko la watu :
Na wamhimidi katika baraza ya wazee.
33. Amegeuza mito ikawa jangwa :
Na chemchemi za maji zikawa inchi ya
kiu.
34. Inchi ya matunda mengi ikawa uwanda
wa chumvi :
Kwa sababu ya ubaya wao walioikaa.
35. Amegeuza jangwa ikawa ziwa la maji :
Na inchi kavu ikawa chemchemi za
maji.
36. Akawakalisha huko wenye njaa :
Nao wametengeneza mji wa kukaa.
37. Wakapanda mbegu mashambani, wakatia
mizabibu :
Iliyotoa matunda yake.
38. Nae huwabariki wakaongezeka sana :
Wala hayapunguzi makundi yao.
39. Na walipopungua na kudhilika :
Kwa kuonewa na mabaya na huzuni.
40. Awamwagia wakuu dharau :
Na kuwazungusha katika nyika isiyo
njia.

41. Alimweka mhitaji juu mbali ya mateso :
Akamfanyia jamaa kama kundi la
kondoo.
42. Wanyofu wa moyo wataona na kufurahi :
Na uovu wa killa namna unajifumba
kinywa.
43. Aliye na hekima na ayaangalie hayo :
Na wazitafakari fadhili za Bwana.
Utukufu.

Ant. Wanyofu wa moyo wataona na kufurahi :
na wazitafakari fadhili za Bwana.





ZABURI SEHEMU B.

SIKU YA BWANA.

Ant. Umwangazie, Ee Bwana : mtumishi wako uso wako.

Zab. 119.

129. Shuhuda zako ni maajabu :
Ndio maana roho yangu imezishika.
130. Kufafanusha maneno yako kwatia nuru :
Na kumfahamisha mjinga.
131. Nalifunua kinywa changu nikatweta :
Maana naliyatamani maagizo yako.
132. Unigeukie, unirehemu :
Kama ilivyo haki yao walipendao Jina lako.
133. Uzielekeze khatua zangu kwa neno lako :
Uovu usije ukanimiliki.
134. Unikomboe na dhuluma ya mwanadamu :
Nipate kuyashika mausia yako.
135. Umwangazie mtumishi wako uso wako :
Unifundishe amri zako.
136. Macho yangu yanachuruzika mito ya maji :
Kwa sababu hawaitii sharia yako.
137. Wewe U mwenye haki, Ee Bwana :
Na hukumu zako za adili.
138. Umeziagiza shuhuda zako kwa haki :
Na kwa uaminifu mwingi.
139. Juhudi yangu imeniangamiza :
Kwa sababu watesi wangu wameyasahau maneno yako.
140. Neno lako limesafika sana :
Mtumishi wako amelipenda.

Zaburi. S. B. B

141. Mimi mdogo, nadharauliwa :
Lakini siyasahau mausia yako.

142. Haki yako ni haki ya milele :
Na sharia yako ni kweli.

143. Taabu na dhiiki zimenipata :
Maagizo yako ni furaha yangu.

144. Haki ya shuhuda zako ni ya milele :
Unifahamishe nami nitaishi.

Utukufu.

Ant. Umwangazie, Ee Bwana : mtumishi wako uso wako.

Ant. Unihuishe, Ee Bwana : sawasawa na ahadi yako.

145. Nimeita kwa moyo wangu wote, unijibu :
Ee Bwana, nitazishika amri zako.

146. Nimekuita, uniokoe :
Nami nitazishika shuhuda zako.

147. Kutangulia mapambazuko naliomba msaada :
Naliyangojea maneno yako kwa tumaini.

148. Macho yangu yalitangulia makesha ya usiku :
Illi kuitafakari ahadi yako.

149. Uisikie sauti yangu sawasawa na fadhili zako :
Ee Bwana, unihuishe sawasawa na hukumu yako.

150. Wanakaribia wanaonifuatia kwa chuki :
Wamekwenda mbali ya sharia yako.

151. Wewe U karibu, Ee Bwana :
Na maagizo yako yote ni kweli.
152. Tokea zamani nimejua kwa shuhuda
zako :
Ya kuwa umeziweka zikae milele.
153. Uyaangalie mateso yangu, uniokoe :
Maana sikuisahau sharia yako.
154. Unitetee na kunikomboa :
Unihuishe sawasawa na ahadi yako.
155. Wokofu u mbali ya wasio haki :
Kwa maana hawazisomi amri zako.
156. Rehema zako zi nyingi, Ee Bwana :
Unihuishe sawasawa na hukumu zako.
157. Wanaonifuatia na watesi wangu ni wengi :
Lakini sikujiepusha na shuhuda zako.
158. Nimewaona watendao hila nikachukizwa :
Kwa sababu hawakulitii neno lako.
159. Uangalie niyapendavyo mausia yako :
Ee Bwana, unihuishe sawasawa na
fadhili zako.
160. Jumla ya neno lako ni kweli :
Na killa hukumu ya haki yako ni ya
milele.
Utukufu.
- Ant.* Unihuishe, Ee Bwana : sawasawa na
ahadi yako.
- Ant.* Unifahamishe, Ee Bwana : sawasawa na
neni lako.
161. Wakuu wameniudhi burre :
Lakini moyo wangu una khofu kwa
[sababu ya maneno yako.
162. Naifurahia ahadi yako :
Kama apatae mateka mengi.

163. Nimechukia uwongo, nitaukirihi :
Sharia yako nimeipenda.
164. Marra saba killa siku nakusifu :
Kwa sababu ya hukumu za haki yako.
165. Wana amani nyingi waipendao sharia
yako :
Wala hawana la kuwakwaza.
166. Nimeungojea wokofu wako, Ee Bwana :
Na maagizo yako nimeyatenda.
167. Roho yangu imezishika shuhuda zako :
Nami nazipenda mno.
168. Nimeyashika mausia yako na shuhuda
zako :
Maana njia zangu zote zi mbele zako.
169. Kilio changu na kikukaribie, Ee Bwana :
Unifahamishe sawasawa na neno lako.
170. Dua yangu na ifike mbele zako :
Uniponye sawasawa na neno lako.
171. Midomo yangu na itoe sifa :
Kwa kuwa unanifundisha mausia yako.
172. Ulimi wangu na uiimbe ahadi yako :
Maana maagizo yako yote ni haki.
173. Mkono wako na uwe tayari kunisaidia :
Maana nimeyachagua mausia yako.
174. Nimeutamani wokofu wako, Ee Bwana :
Na sharia yako ndiyo furaha yangu.
175. Roho yangu na iishi, ipate kukusifu :
Na hukumu zako zinisaidie.
176. Nikitangatanga umtafute mtumishi wako
kama kondoo aliyepotea :
Kwa maana sikuyasahau maagizo yako.
Utukufu.
- Ant.* Unifahamishe, Ee Bwana : sawasawa na
neni lako.

JUMA A TATU.

Ant. Mungu wa utukufu alipiga radi : mpeni utukufu wa Jina lake.

Zab. 29.

1. Mpeni Bwana, enyi wana wa Mungu :
Mpeni Bwana utukufu na nguvu.
 2. Mpeni Bwana utukufu wa Jina lake :
Mwabuduni Bwana kwa uzuri wa utakatifu.
 3. Sauti ya Bwana i juu ya maji :
Mungu wa utukufu alipiga radi.
 4. Bwana yu juu ya maji mengi :
Sauti ya Bwana ina nguvu.
 5. Sauti ya Bwana ina adhama :
Sauti ya Bwana yaivunja mierezi.
 6. Bwana aivunjavunja mierezi ya Lebanoni :
Airusharusha kama ndama ya ng'ombe.
 7. Lebanoni na Sirioni kama mwana nyati :
Sauti ya Bwana yaipasua miali ya moto.
 8. Sauti ya Bwana yalitetemesha jangwa :
Bwana alitetemesha jangwa la Kadeshi.
 9. Sauti ya Bwana yawazalisha ayala :
Na kuikashifu misitu.
 10. Na ndani ya hekalu lake :
Wanasema wote, Utukufu.
 11. Bwana aliketi juu ya Gharika :
Naam, Bwana ameketi mfano wa mfalme milele.
 12. Bwana atawapa watu wake nguvu :
Bwana atawabariki watu wake kwa amani.
- Utukufu,

Ant. Mungu wa utukufu alipiga radi : mpeni utukufu wa Jina lake.

Ant. Mpigieni kelele Mungu : kwa sauti ya shangwe.

Zab. 47.

1. Enyi watu wote, pigeni makofi :
Mpigieni kelele Mungu kwa sauti ya shangwe.
 2. Kwa kuwa Bwana Aliye juu, mwenye kuogofya :
Ndiye mfalme mkuu juu ya dunia yote.
 3. Atawatiisha watu wa inchi chini yetu :
Na mataifa chini ya miguu yetu.
 4. Atatuchagulia urithi wetu :
Fakhari ya Yakobo ambae alimpenda.
 5. Mungu amepaa kwa kelele za shangwe :
Bwana kwa sauti ya baragumu.
 6. Mwimbieni Mungu, naam, imbeni :
Mwimbieni mfalme wetu, naam, imbeni.
 7. Maana Mungu ndiye mfalme wa dunia yote :
Imbeni kwa akili.
 8. Mungu awamiliki mataifa :
Mungu ameketi katika kiti cha utakatifu wake.
 9. Wakuu wa watu wamekusanyika :
Wawe watu wa Mungu wa Ibrahimu.
 10. Maana ngao za dunia zina Mungu :
Ametukuka sana.
- Utukufu.

Ant. Mpigieni kelele Mungu : kwa sauti ya shangwe.

Zaburi. J. a 3. B

Ant. Mtu aliye na mikono safi na moyo mweupe : huyu atapanda katika mlima wa Bwana.

Zab. 24.

1. Inchi na vyote viijazavyo ni mali ya Bwana:
Dunia na wote wakaao ndani yake.
2. Maana Yeye ndiye aliyeiweka misingi yake
juu ya bahari :
Na juu ya mito ya maji alithubutisha.
3. Ni nani atakaepanda katika mlima wa
Bwana :
Ni nani atakaesimama katika patakatifu
pake ?
4. Mtu aliye na mikono safi na moyo mweupe,
asiyeiinua roho yake kwa ubatili :
Wala hakuapa kwa hila.
5. Atapokea baraka kwa Bwana :
Na haki kwa Mungu wa wokofu wake.
6. Hiki ndicho kizazi cha wamtafutao :
Wakutafutao uso wako, Ee Mungu wa
Yakobo.
7. Inueni vichwa vyenu, enyi malango, inu-
keni, enyi malango ya milele :
Mfalme wa utukufu apate kuingia.
8. Ni nani Mfalme wa utukufu :
Bwana mwenye nguvu na uhodari,
Bwana hodari wa vita.
9. Inueni vichwa vyenu, enyi malango, naam,
viinueni, enyi malango ya milele :
Mfalme wa utukufu apate kuingia.
10. Ni nani huyu Mfalme wa utukufu :
Bwana wa majeshi, ndiye Mfalme wa
utukufu.

Utukufu.

Zaburi. J. a 3. B

Ant. Mtu aliye na mikono safi na moyo mweupe : huyu atapanda katika mlima wa Bwana.

Ant. Unitakase, Ee Bwana : na mambo ya siri.

Zab. 19.

1. Mbingu zaukhubiri utukufu wa Mungu :
Na anga yaitangaza kazi ya mikono yake.
2. Mchana husemezana na mchana :
Usiku hutolea usiku maarifa.
3. Hakuna lugha wala maneno :
Sauti yao haisikilikani.
4. Sauti yao imeenea duniani mwote :
Na maneno yao hatta miisho ya uli-
mwengu.
5. Ameliwekea jua khema katika hizo :
Nalo kama bwana arusi atokae
chumbani mwake.
6. Lafurahi kama mtu aliye hodari :
Kwenda mbio katika njia yake.
7. Kutoka kwake lautoka mwisho wa mbingu :
Na kuzunguka kwake hatta miisho yake.
8. Wala kwa hari yake :
Hakuna kitu kilichosetirika.
9. Sharia ya Bwana ni kamilifu :
Huiburudisha roho.
10. Ushuhuda wa Bwana amini :
Humtia mjinga hekima.
11. Maagizo ya Bwana ya adili :
Huufurahisha moyo.
12. Amri ya Bwana ni safi :
Huyatia macho nuru.

13. Kumcha Bwana kutakatifu :
Kunadumu milele.
14. Hukumu za Bwana zi kweli :
Zina haki kabisa.
15. Ni za kutamanika kuliko dhahabu :
Kuliko wingi wa dhahabu safi.
16. Nazo ni tamu kuliko asali :
Kuliko sega la asali.
17. Tena mtumishi wako huonywa nazo :
Katika kuzishika kuna thawabu nyingi.
18. Ni nani awezae kuyatambua makosa
yake :
Unitakase na mambo ya siri.
19. Umzuie mtumishi wako asitende mambo
ya kiburi :
Yasinitawale mimi.
20. Ndipo nitakapokuwa kamili :
Nami nitakuwa safi, sina kosa lililo
kubwa.
21. Maneno ya kinywa changu :
Na mawazo ya moyo wangu.
22. Yapate kibali mbele zako, Ee Bwana :
Mwamba wangu na mwokozi wangu.
Utukufu.

Ant. Unitakase, Ee Bwana : na mambo ya siri.



JUMA A NNE.

Ant. Mungu wangu, nimekutumaini Wewe :
nisiaibike.

Zab. 25.

1. Ee Bwana, nakuinulia roho yangu :
Mungu wangu, nimekutumaini.
2. Nimekutumaini Wewe nisibiaike :
Adui zangu wasifurahi kwa kunishinda.
3. Naam, wakungojao hawataaibika hatta
mmoja :
Wataaibika watendao khiyana bila
sababu.
4. Unijulishe njia zako, Ee Bwana :
Unifundishe mapito yako.
5. Uniongoze katika kweli yako :
Na kunifundisha.
6. Maana Wewe ndiwe Mungu wangu :
Nakungoja Wewe mchana kutwa.
7. Kumbuka, Ee Bwana, rehema zako na
fadhili zako :
Maana zimekuwako tokea zamani.
8. Usizikumbuke dhambi za ujana wangu :
Wala maasi yangu.
9. Unikumbuke kwa kadiri ya fadhili zako :
Ee Bwana, kwa ajili ya wema wako.
10. Bwana yu mwema, mwenye adili :
Kwa hiyo atawafundisha wenye dhambi
njia.
11. Wenye upole atawaongoza katika huku-
mu :
Wenye upole atafundisha njia yake.

12. Njia zote za Bwana ni fadhili na kweli :
Kwao walishikao agano lake na shuhuda zake.
13. Kwa ajili ya Jina lako, Ee Bwana :
Unisamehe uovu wangu, maana ni mwingi.
14. Ni nani amchae Bwana :
Atamfundisha katika njia anayoichagua.
15. Roho yake itakaa hali ya kufanikiwa :
Wazao wake watairithi inchi.
16. Siri ya Bwana iko kwa wamchao :
Nae atawajulisha agano lake.
17. Macho yangu kwa Bwana daima :
Nae atanitoa miguu yangu katika wavu.
18. Uniangalie, unifadhili :
Maana mimi ni mkiwa na mteswa.
19. Katika shidda za moyo wangu unifanyie nafasi :
Ukanitoe katika dhiiki zangu.
20. Utazame teso langu na taabu yangu :
Unisamehe dhambi zangu zote.
21. Uwatazame adui zangu, maana ni wengi :
Wananichukia kwa machukio ya ukali.
22. Unilinde roho yangu, uniponye :
Nisiaibike maana nakukimbilia Wewe.
23. Ukamilifu na unyofu zinihifadhi :
Maana nakungoja Wewe.
24. Umkomboe Israeli, Ee Mungu :
Katika taabu zake zote.

Utukufu.

Ant. Mungu wangu, nimekutumaini Wewe :
nisiaibike.

Ant. Msaada wetu : u katika Jina la Bwana.

Zab. 124.

1. Kama isingalikuwa Bwana aliyekuwa pamoja nasi :
Israeli na aseme sasa.
2. Kama isingalikuwa Bwana aliyekuwa pamoja nasi :
Bin Adamu alipotushambulia.
3. Papo hapo wangelitumeza hayi :
Hasira yao ilipowaka juu yetu.
4. Papo hapo maji yangalitugharikisha :
Mto ungalipita juu ya roho zetu.
5. Papo hapo yangalipita juu ya roho zetu :
Maji yafurikayo.
6. Na ahimidiwe Bwana :
Asiyetutoa kuwa mawindo kwa meno yao.
7. Roho yetu imeokoka kama ndege katika mtego wa wawindaji :
Mtego umevunjika nasi tumeokoka.
8. Msaada wetu u katika Jina la Bwana :
Aliyezifanya mbingu na inchi.

Utukufu.

Ant. Msaada wetu : u katika Jina la Bwana.

Ant. Ee Bwana, uwatendee mema walio wema : Amani ikae na Israeli.

Zab. 125.

1. Wamtumainio Bwana ni kama mlima Sayuni :
Ambao hautatikisika, wakaa milele.

2. Kama milima inavyozunguka Yerusalemi :

Ndivyo Bwana anavyowazunguka watu wake, tangu sasa na hatta milele.

3. Kwa maana fimbo ya udhalimu :
Haitakaa juu ya fungu la wenye haki.

4. Wenye haki wasije wakainyosha :
Mikono yao kwa upotofu.

5. Ee Bwana, uwatendee mema walio wema :
Nao walio wanyofu wa moyo.

6. Bali wao wanaozigeukia njia zao zilizopotoka :
Bwana atawaondoa pamoja na watenda maovu.

Utukufu.

Ant. Ee Bwana, uwatendee mema walio wema : Amani ikae na Israeli.

Ant. Bwana alitutendea mambo makuu : tulikuwa tukifurahi.

Zab. 126.

1. Bwana alipowarejeza waliorejea Sayuni :
Tulikuwa kama waotao ndoto.

2. Ndipo kinywa chetu kikajaa kicheko :
Na ulimi wetu kelele za furaha.

3. Ndipo waliposema katika mataifa :
Bwana amewatendea mambo makuu.

4. Bwana alitutendea mambo makuu :
Tulikuwa tukifurahi.

5. Ee Bwana, uwarejeze watu wetu waliofungwa :
Kama vijito vya Kusini.

6. Wapandao kwa machozi :
Watavuna kwa kelele za furaha.

7. Ingawa anakwenda zake akilia :
Achukuapo mbegu za kupanda.

8. Hakika atarudi kwa kelele za furaha :
Achukuapo miganda yake.

Utukufu.

Ant. Bwana alitutendea mambo makuu :
tulikuwa tukifurahi.

Ant. Bwana atujengee nyumba : na kuulinda mji wetu.

Zab. 127.

1. Bwana asipojenga nyumba :
Waijengao wafanya kazi burre.

2. Bwana asipoulinda mji :
Yeye aulindae akesha burre.

3. Kazi yenu ni burre, ninyi mnaoamka mapema :
Na kukawia kwenda kulala.

4. Mnapokula chakula cha taabu :
Humpa mpenzi wake usingizi.

5. Wana ndio walio urithi wa Bwana :
Uzao wa tumbo ni thawabu.

6. Kama mishale mkononi mwa shujaa :
Ndivyo walivyo wana wa ujanani.

7. Yu kheri mtu yule :
Aliyelijaza podo lake hivyo.

8. Naam, hawataona aibu :
Wanapokisema na adui langoni.

Utukufu.

Ant. Bwana atujengee nyumba : na kuulinda mji wetu.

JUMA A TANO.

Ant. Utayafunika, Ee Mungu : maasi yetu.

Zab. 65.

1. Sifa zakulaiki Wewe, Ee Mungu, katika Sayuni :
Na kwako Wewe itaondolewa nadhiri.
2. Wewe usikiae kuomba :
Wote wenye mwili watakuja.
3. Ingawa maovu mengi yanatushinda :
Wewe utayafunika maasi yetu.
4. Yu kheri mtu yule umchaguae :
Na kumkaribisha akae nyuani mwako.
5. Na tushibe wema wa nyumba yako :
Patakatifu pa hekalu lako.
6. Kwa mambo ya kutisha utatujibu :
Katika haki, Ee Mungu wa wokofu wetu.
7. Wewe uliye tumaini la miisho yote ya inchi :
Na la bahari iliyo mbali sana.
8. Milima aiweka imara kwa nguvu zake :
Amejifunga uweza kama mshipi.
9. Autuliza uvumi wa bahari, uvumi wa mawimbi yake :
Na ghasia ya mataifa.
10. Kwa hiyo wakaao mbali kabisa huogopa ishara zako :
Milango ya assubuhi na jioni waifurahisha.
11. Umejilia inchi na kuisitawisha :
Umeitajirisha sana.
12. Mto wa Mungu umejaa maji :
Wawaruzuku watu nafaka.

13. Maana ndiwe uitengenezae inchi :
Matuta yake wayajaza maji.
14. Wapasawazisha palipoinuka :
Wailainisha inchi kwa manyunyu.
15. Waibariki mimea yake :
Umeuvika mwaka taji ya wema wako.
16. Mapito yako yadondoza unono :
Huyadondokea malisho ya nyikani.
17. Na vilima vyajifunga furaha :
Na malisho yamevikwa kondoo.
18. Na mabonde yamepambwa nafaka :
Yanashangilia, naam, yanaimba.
Utukufu.

Ant. Utayafunika, Ee Mungu : maasi yetu.

Ant. Mcha Mungu ndiye aliye kheri : Amani ikae na Israeli.

Zab. 128.

1. Yu kheri killa mtu amchae Bwana :
Aendae katika njia yake.
2. Taabu ya mikono yako hakika utaila :
Utakuwa kheri na kwako kwema.
3. Mke wako atakuwa kama mzabibu uzaao :
Vyumbani mwa nyumba yako.
4. Wanawo kama miche ya mizeituni :
Wakiizunguka meza yako.
5. Hivyo ndivyo atakavyobarikiwa :
Mtu yule amchae Bwana.
6. Bwana akubariki toka Sayuni :
Upate kuuona ukheri wa Yerusalemi.
7. Siku zote za maisha yako :
Naam, ukawaone wana wa wanawo.
Utukufu.

Zaburi. J. a 5. B

Ant. Mcha Mungu ndiye aliye kheri : Amani ikae na Israeli.

Ant. Na waaibishwe wote : wanaoichukia Sayuni.

Zab. 129.

1. Marra nyingi wamenitesa tangu ujana wangu :
Israeli na aseme sasa.
2. Marra nyingi wamenitesa tangu ujana wangu :
Lakini hawakuniweza.
3. Wakulima wamelima mgongoni mwangu :
Wamefanya mirefu mifuo yao.
4. Bwana ndiye mwenye haki :
Amezikata kamba zao wasio haki.
5. Na waaibishwe, warudishwe nyuma :
Wote wanaoichukia Sayuni.
6. Na wawe kama majani ya darini :
Yanyaukayo kabla hayajamea.
7. Ambayo mvunaji haujazi mkono wake :
Wala mfunga miganda kifua chake.
8. Wala hawasemi wapitao, Amani ya Bwana ikae nanyi :
Twakubarikini kwa Jina la Bwana.
Utukufu.

Ant. Na waaibishwe wote : wanaoichukia Sayuni

Ant. Ee Israeli : umtumaini Bwana.

Zab. 131.

1. Ee Bwana, moyo wangu hauna kiburi :
Wala macho yangu hayainuki.

Zaburi. J. a 5. B

2. Wala sijishughulishi na mambo makuu :
Wala na mambo yashindayo nguvu zangu.
3. Hakika nimeituliza roho yangu :
Na kuinyamazisha.
4. Kama mtoto aliyeachishwa :
Kifuani mwa mama yake.
5. Kama mtoto aliyeachishwa :
Ndivyo roho yangu ilivyo kwangu.
6. Ee Israeli, umtumaini Bwana :
Tangu leo na hatta milele.
Utukufu.

Ant. Ee Israeli : umtumaini Bwana.

Ant. Bwana ameichagua Sayuni : akae ndani yake.

Zab. 132.

1. Ee Bwana, umkumbukie Daudi :
Taabu zake zote alizotaabika.
2. Ndiye aliyemwapia Bwana :
Akaweka nadhiri kwa Shujaa wa Yakobo.
3. Sitaingia khemani mwa nyumba yangu :
Wala sitapanda matandiko ya kitanda changu.
4. Sitaacha macho yangu kuwa na usingizi :
Wala kope zangu kusinzia.
5. Hatta nitakapompata Bwana mahali :
Na Shujaa wa Yakobo masikani.
6. Tazama, tulisikia khabari zake katika Efrata :
Katika konde la Yearim tuliiona.
7. Na tuiingie masikani yake :
Na tusujudu penye kiti cha kuwekea miguu yake.

8. Uondoke, Ee Bwana, uende kwenye raha yako :
Wewe na sanduku la nguvu zako.
9. Makuhani wako na wavikwe haki :
Watakatifu wako na washangilie.
10. Kwa ajili ya Daudi mtumishi wako :
Usiurudishe nyuma uso wa Masihi wako.
11. Bwana amemwapa Daudi neno la kweli :
Hatarudi nyuma akaikhalifu.
12. Baadhi ya wazao wa mwili wako :
Nitawaweka katika kiti chako cha enzi.
13. Wana wako wakiyashika maagano yangu :
Na shuhuda nitakazowafundisha.
14. Wana wao nao wataketi :
Katika kiti chako cha enzi milele.
15. Maana Bwana ameichagua Sayuni :
Ameitamani akae ndani yake.
16. Hapa ndipo mahali pangu pa raha milele :
Hapa nitakaa kwa maana nimepatamani.
17. Hakika nitavibariki vyakula vyake :
Wahitaji wake nitawashibisha kwa mkate.
18. Na makuhani wake nitawavika wokofu :
Na watakatifu wake watashangilia.
19. Hapa nitamchipushia Daudi pembe :
Na taa nime mtengenezea Masihi wangu.
20. Adui zake nitawavika aibu :
Bali juu yake taji yake itasitawi.

Utukufu.

Ant. Bwana ameichagua Sayuni : akae ndani yake.

ALKHAMISI.

Zab. 133.

Ant. Vyapendeza namna gani : ndugu wakae pamoja, pia kwa umoja.

1. Ni vyema namna gani, vyapendeza namna gani :
Ndugu wakae pamoja, pia kwa umoja.
2. Ni kama mafuta mazuri kichwani :
Yashukayo ndevuni, ndevu za Haruni.
3. Yashukayo mpaka upindo wa mavazi yake :
Kama umande wa Hermoni ushukao milimani pa Sayuni.
4. Maana ndiko Bwana alikoamuru baraka :
Naam, uzima hatta milele.
Utukufu.

Ant. Vyapendeza namna gani : ndugu wakae pamoja, pia kwa umoja.

Ant. Fadhili za Bwana : ni za milele.

Zab. 136.

1. Mshukuruni Bwana kwa kuwa yu mwema :
Kwa maana fadhili zake ni za milele.
2. Mshukuruni Mungu wa miungu :
Kwa maana fadhili zake ni za milele.
3. Mshukuruni Bwana wa mabwana :
Kwa maana fadhili zake ni za milele.
4. Yeye peke yake afanya maajabu makuu :
Kwa maana fadhili zake ni za milele.

5. Yeye alifanya mbingu kwa fahamu zake :
Kwa maana fadhili zake ni za milele.
6. Yeye aliitandaza inchi juu ya maji :
Kwa maana fadhili zake ni za milele.
7. Yeye alifanya mianga mikubwa :
Kwa maana fadhili zake ni za milele.
8. Jua litawale mchana :
Kwa maana fadhili zake ni za milele.
9. Mwezi na nyota zitawale usiku :
Kwa maana fadhili zake ni za milele.
10. Yeye aliwapiga Wamisri kwa kuwaua
wazaliwa wa kwanza wao :
Kwa maana fadhili zake ni za milele.
11. Akawatoa Waisraeli katika katikati yao :
Kwa maana fadhili zake ni za milele.
12. Kwa mkono hodari na mkono ulionyosh-
wa :
Kwa maana fadhili zake ni za milele.
13. Yeye aliigawa Bahari ya Sham :
Kwa maana fadhili zake ni za milele.
14. Akawavusha Israeli katikati yake :
Kwa maana fadhili zake ni za milele.
15. Akamwangusha Farao na jeshi lake katika
Bahari ya Sham :
Kwa maana fadhili zake ni za milele.
16. Yeye aliwaongoza watu wake jangwani :
Kwa maana fadhili zake ni za milele.
17. Yeye aliwapiga wafalme wakuu :
Kwa maana fadhili zake ni za milele.
18. Akawaua wafalme mashuhuri :
Kwa maana fadhili zake ni za milele.
19. Sihon, mfalme wa Waamori :
Kwa maana fadhili zake ni za milele.

20. Na Og, mfalme wa Basani :
Kwa maana fadhili zake ni za milele.
21. Akaitoa inchi yao iwe urithi :
Kwa maana fadhili zake ni za milele.
22. Urithi wa Israeli watumishi wake :
Kwa maana fadhili zake ni za milele.
23. Alitukumbuka katika unyonge wetu :
Kwa maana fadhili zake ni za milele.
24. Akatuokoa na adui zetu :
Kwa maana fadhili zake ni za milele.
25. Killa chenye mwili akipa chakula chake :
Kwa maana fadhili zake ni za milele.
26. Mshukuruni Mungu wa mbingu :
Kwa maana fadhili zake ni za milele.

Utukufu.

Ant. Fadhili za Bwana : ni za milele.

Ant. Ulimi wangu na ugandamane na kaakaa
la kinywa changu : nisipokukumbuka, Ee Yeru-
salemi.

Zab. 137.

1. Kando ya mito ya Babeli ndiko tuliketi :
Tukalia tulipoikumbuka Sayuni.
2. Katika miti iliyo katikati yake :
Tulivitundika vinubi vyetu.
3. Maana huko waliotuchukua mateka :
Walitaka tuwaimbie.
4. Na waliotuonea walitaka furaha :
Tuimbieni baadhi ya nyimbo za Sayuni.
5. Tuimbeje uimbo wa Bwana :
Katika inchi ya ugeni ?
6. Kama nikikusahau, Ee Yerusalemi :
Mkono wangu wa kuume na usahau.

Zaburi. Alkh. B

7. Ulimi wangu na ugandamane :
Na kaakaa la kinywa changu nisipoku-
kumbuka.
8. Nisipoikuza Yerusalemi :
Zaidi ya furaha yangu iliyo kuu.
9. Uwakumbuke, Ee Bwana, wana wa
Edomi :
Siku ya Yerusalemi.
10. Waliosema, Bomoeni :
Bomoeni hatta misingini !
11. Ee binti Babeli uliye tayari kuangamia :
Yu kheri atakaekupatiliza ulivyotupa-
tiliza sisi.
12. Yu kheri atakaewakamata watoto wako
walio wachanga :
Na kuwaseta juu ya mwamba.

Utukufu.

Ant. Ulimi wangu na ugandamane na kaakaa
la kinywa changu : nisipokukumbuka, Ee Yeru-
salemi.

Ant. Nitalishukuru Jina lako, Ee Bwana : kwa
ajili ya fadhili zako na uaminifu wako.

Zab. 138.

1. Nitakushukuru kwa moyo wangu wote :
Mbele za miungu nitakuimbia zaburi.
2. Nitasujudu nikikabili hekalu lako taka-
tifu :
Nitalishukuru Jina lako.
3. Kwa ajili ya fadhili zako na uaminifu
wako :
Kwa maana umelikuza Jina lako juu
ya yote.

Zaburi. Alkh. B

4. Siku ile niliyokuita ulinjibu :
Ukanifariji roho kwa kunitia nguvu.
5. Wafalme wote wa dunia watakushukuru,
Ee Bwana :
Watakaposikia maneno ya kinywa chako.
6. Naam, wataziimba njia za Bwana :
Kwa maana utukufu wa Bwana ni mkuu.
7. Maana ingawa Bwana yuko juu amwona
mnyenyekevu :
Nae amjua mwenye kujivuna tokea
mbali.
8. Nijapokwenda kati ya shidda utanihuisha :
Utaunyosha mkono wako juu ya gha-
dhabu ya adui zangu.
9. Na mkono wa kuume utaniokoa :
Bwana atanitimizia mambo yangu.
10. Fadhili zako, Ee Bwana, ni za milele :
Usiziache kazi za mikono yako.

Utukufu.

Ant. Nitalishukuru Jina lako, Ee Bwana : kwa
ajili ya fadhili zako na uaminifu wako.



IJUMAA.

Ant. Matendo yako ya ajabu, Ee Bwana : na roho yangu yajua sana.

Zab. 139.

1. Ee Bwana, umenichunguza na kunijua :
Wewe wajua kuketi kwangu.
2. Wajua na kuondoka kwangu :
Umefahamu wazo langu tokea zamani.
3. Umepepeta mwenendo wangu na kulala kwangu :
Umeelewa na njia zangu zote.
4. Maana hamna neno ulimini mwangu :
Usilolijua kabisa, Ee Bwana.
5. Umenihusuru nyuma na mbele :
Ukanishika kwa mkono wako.
6. Maarifa haya ni ya ajabu, yanishinda mimi :
Hayadirikiki siwezi kuyafikia.
7. Niende wapi nijiepushe na roho yako :
Niende wapi niukimbie uso wako ?
8. Kama ningepanda mbinguni, Wewe uko :
Ningefanya kuzimu kitanda changu,
Wewe uko.
9. Ningezitwaa mbawa za assubuhi :
Na kukaa pande za mwisho za bahari.
10. Huko nako mkono wako utaniongoza :
Na mkono wako wa kuume utanishika.
11. Kama nikisema, Hakika giza litanifunika :
Na nuru inizungukayo ikawa usiku.

12. Giza nalo halikufichi kitu, bali usiku huangaza kama mchana :
Giza na mwanga kwako ni sawasawa.
13. Maana Wewe ndiwe uliyeniumba mtima wangu :
Uliniunga tumboni mwa mama yangu.
14. Nitakushukuru kwa kuwa nimeumbwa :
Kwa jinsi ya ajabu ya kutisha.
15. Matendo yako ya ajabu :
Na roho yangu yajua sana.
16. Mifupa yangu haikusetirika kwako :
Nilipoumbwa kwa siri.
17. Nilipoungwa kwa ustadi pande za chini za inchi :
Macho yako yaliniona kabla sijakamilika.
18. Chuoni mwako ziliandikwa zote pia :
Siku zilizoamriwa kabla hazijawa bado.
19. Kwangu mimi fikara zako zina thamani nyingi, Ee Mungu :
Ee ajabu ya wingi wa jumla yake !
20. Kama ningezihesabu zi nyingi kuliko mchanga :
Niamkapo nikali pamoja nawe.
21. Ningependa kama ungewaua waovu, Ee Mungu :
Ondokeni kwangu, enyi watu wa damu.
22. Kwa maana wakuasi kwa ubaya :
Adui zako wakutaja Jina lako burre.
23. Nisiwachukie, Ee Bwana, wanaokuchukia :
Nisikirihike nao wakuasio ?
24. Nawachukia kwa ukomo wa chuki :
Wamekuwa adui kwangu.

Zaburi. Ij. B

25. Unichunguze, Ee Mungu, ujue moyo wangu :

Unijaribu, ujue mawazo yangu.

26. Ukaone kama iko njia iletayo majuto ndani yangu :

Ukaniongoze katika njia ya milele.

Utukufu.

Ant. Matendo yako ya ajabu, Ee Bwana : na roho yangu yajua sana.

Ant. Kunatupendeza : kumsifu Mungu wetu. Halleluya.

Zab. 147.

1. Ni vyema kumwambia Mungu wetu :
Maana kwapendeza, kusifu ni kuzuri.
2. Bwana ndiye aijengae Yerusalemi :
Huwakusanya waliotawanyika wa Israeli.
3. Huwaponya waliopondeka moyo :
Na kuzifunga jeraha zao.
4. Huihesabu idadi ya nyota :
Huzipa zote majina.
5. Bwana wetu mkuu na mwingi wa nguvu :
Akili zake hazina idadi.
6. Bwana huwategemeza wenye upole :
Huwaangusha chini wasio haki.
7. Mwimbieni Bwana kwa kushukuru :
Mwimbieni Mungu wetu kwa kinubi.
8. Huzifunika mbingu kwa mawingu, huite-
ngenezea inchi mvua :
Huyameesha majani milimani.
9. Humpa nyama chakula chake :
Wana kunguru wamliliao.

Zaburi. Ij. B

10. Hapendezwi na nguvu za farasi :
Wala hairidhii miguu ya mtu.

11. Bwana huwaridhia wamchao :
Wazingojao fadhili zake.

12. Msifuni Bwana, Ee Yerusalemi :
Msifuni Mungu wako, Ee Sayuni.

13. Maana ameyakaza mapingo ya malango yako :

Amewabariki wanawo ndani yako.

14. Ndiye afanyae amani mipakani mwako :
Akushibishae kwa unono wa nganu.

15. Huipeleka amri yake juu ya inchi :
Neno lake lapiga mbio sana.

16. Ndiye atoe thuluji kama sufu :
Huimwaga jalidi yake kama majivu.

17. Hutupa mvua ya mawe kama makombo :
Mbele ya baridi yake ni nani awezae kusimama ?

18. Hulituma neno lake akaviyeyusha :
Huuvumisha upepo wake, maji yakati-
ririka.

19. Humkhubiri Yakobo neno lake :
Israeli amri zake na hukumu zake.

20. Hakulitendea taifa lo lote mambo kama hayo :

Na hukumu zake hawakuzijua.

Utukufu.

Ant. Kunatupendeza : kumsifu Mungu wetu. Halleluya.



JUMA A MOSI.

*Ant. Uniponye, Ee Bwana, na adui zangu :
nimekukimbilia Wewe, unifiche.*

Zab. 143.

1. Ee Bwana, usikie sala yangu, usikilize dua zangu :
Kwa uaminifu wako unijibu kwa haki yako.
2. Wala usimhukumu mtumishi wako :
Maana mbele zako hakuna aliye hayi atakaekuwa mwenye haki.
3. Maana adui ameifuatia roho yangu :
Ameutupa chini uzima wangu.
4. Amenikalisha mahali penye giza :
Kama watu waliokufa zamani.
5. Na roho yangu imezimia ndani yangu :
Moyo wangu ndani yangu umeshituka.
6. Nimezikumbuka siku za kale :
Nimeyatafakari matendo yako yote.
7. Naziwaza kazi za mikono yako :
Nakunyoshea mikono yangu.
8. Roho yangu yakutamani kama inchi kame :
Unijibu hima, Ee Bwana, roho yangu imelekea.
9. Usinifiche uso wako :
Nisifanane nao washukao shimoni.
10. Unisikize fadhili zako assubuhi :
Kwa maana nimekutumaini Wewe.

11. Unijulisha njia nitakayoidea :
Kwa maana nakuinulia roho yangu.
12. Uniponye, Ee Bwana, na adui zangu :
Nimekukimbilia Wewe, unifiche.
13. Unifundisha kuyatenda mapenzi yako :
Kwa maana ndiwe Mungu wangu.
14. Roho yako mwema aniongoze kwenye inchi sawa :
Kwa ajili ya Jina lako, Ee Bwana, unihuishe.
15. Kwa haki yako unitoe roho yangu taabuni :
Kwa fadhili zako utawakatilia mbali adui zangu.
16. Na kuwaangamiza wote wanitesao :
Kwa maana mimi ni mtumishi wako.
Utukufu.

*Ant. Uniponye, Ee Bwana, na adui zangu :
nimekukimbilia Wewe, unifiche.*

Ant. Wa kheri watu : wenye Bwana kuwa Mungu wao.

Zab. 144.

1. Na ahimidiwe Bwana, mwamba wangu :
Anifundishae mikono yangu vita, vidole vyangu kupigana.
2. Fadhili zangu na boma langu :
Ngome yangu na mwokozi wangu.
3. Ngao yangu niliyemkimbilia :
Huwatiisha watu wangu chini yangu.
4. Ee Bwana, mtu ni nini hatta umjue :
Na bin Adamu hatta umwangalie ?

5. Bin Adamu amefanana na ubatili :
Siku zake kama kivuli kipitacho.
6. Ee Bwana, uziinamishe mbingu zako,
ushuke :
Uiguse milima nayo itatoka moshi.
7. Utupe umeme, uwatawanye :
Uipige mishale yako, uwafadhaishe.
8. Unyoshe mikono yako toka juu, uniponye :
Unitoe katika maji mengi, katika mkono
wa wageni.
9. Vinywa vyao vyasema visivyofaa :
Na mkono wao wa kuume mkono wa
uwongo.
10. Nitakuimbia uimbo mpya, Ee Mungu :
Kwa kinanda chenye nyuzi kumi nita-
kuimba.
11. Awapae wafalme wokofu :
Amwokoia Daudi mtumishi wake na
upanga wa uovu.
12. Uniponye, unitoe :
Katika mkono wa wageni.
13. Vinywa vyao vyasema visivyofaa :
Na mkono wao wa kuume mkono wa
uwongo.
14. Wana wetu na wawe kama miche :
Waliokua ujanani.
15. Binti zetu kama nguzo za pembeni :
Zilizonakishwa kwa kupamba hekalu.
16. Ghala zetu zijae :
Zenye akiba za jinsi zote.
17. Kondoo zetu zizae :
Elfu na makumi elfu mashambani
mwetu.

18. Ng'ombe zetu zichukue mizigo :
Kusiwe na kushambuliwa.
19. Wala kusiwe na kuhamishwa :
Wala malalamiko katika njia zetu.
20. Wa kheri watu wenye hali hiyo :
Wa kheri watu wenye Bwana kuwa
Mungu wao.
Utukufu.
Ant. Wa kheri watu : wenye Bwana kuwa
Mungu wao.
Ant. Nitamwimbia Mungu wangu : muda wa
uhayi wangu. Halleluya.

Zab. 146.

1. Msifuni Bwana :
Ee roho yangu, umsifu Bwana.
2. Nitamsifu Bwana maadam ninaishi :
Nitamwimbia Mungu wangu muda wa
uhayi wangu.
3. Msiwatumainie wakuu :
Wala bin Adamu ambae hakuna wokofu
kwake.
4. Pumzi yake hutoka, hukurudia udongo
wake :
Siku hiyo mawazo yake yapotea.
5. Yu kheri mwenye Mungu wa Yakobo
kuwa msaada wake :
Na tumaini lake kwa Bwana Mungu
wake.
6. Aliyezifanya mbingu na inchi :
Bahari na vitu vyote vilivyomo.

Zaburi. J. a 1. B

7. Huishika kweli milele :
Huwafanyia hukumu walioonewa.
8. Huwapa wenye njaa chakula :
Bwana hufungua waliofungwa.
9. Bwana huwafumbua macho waliopofuka :
Bwana huwainua walioinama.
10. Bwana huwapenda wenye haki :
Bwana huwahifadhi wageni.
11. Huwategemeza yatima na mjane :
Bali njia ya wasio haki huipotosha.
12. Bwana atamiliki milele :
Mungu wako, Ee Sayuni, kizazi hatta
kizazi.

Utukufu.

Ant. Nitamwimbia Mungu wangu : muda wa
uhayi wangu. Halleluya.



ZABURI SEHEMU C.

Ant. Bwana alijenga patakatifu pake : kama
dunia aliyoiweka imara milele.

Zab. 78.

41. Wakakumbuka kuwa Mungu yu mwamba
wao :
Na Mungu Aliye juu mkombozi wao.
42. Lakini walindanganya kwa vinywa vyao :
Wakamwambia uwongo kwa ndimi zao.
43. Kwa maana mioyo yao haikuwa thabiti
kwake :
Wala hawakuwa waaminifu katika
agano lake.
44. Lakini Yeye kwa kuwa ana rehema :
Husamehe uovu wala haangamizi.
45. Marra nyingi huipishia mbali ghadhabu
yake :
Wala haiwashi hasira yake yote.
46. Akakumbuka ya kuwa wao ni kiwiliwili :
Upepo upitao wala haurudi.
47. Walimwasi jangwani marra ngapi :
Na kumhuzunisha nyikani !
48. Wakarudi nyuma wakamjaribu Mungu :
Wakampa mpaka Mtakatifu wa Israeli.
49. Hawakukumbuka mkono wake :
Wala siku ile alipowakomboa na adui.
50. Alivyoweka ishara zake katika Misri :
Na miujiza yake katika konde la Zoani.
51. Aligeuza damu mito yao :
Na vijito vyao wasipate kunywa.
52. Aliwapelekea mainzi yakawala :
Na vyura vikawaharibu.

Zaburi. C

53. Akawapa panzi mazao yao :
Na nziye kazi yao.
54. Aliharibu mizabibu yao kwa mvua ya mawe :
Na mikuyu yao kwa mawe ya barafu.
55. Akaacha ng'ombe zao wapigwe kwa mvua ya mawe :
Na makundi yao kwa umeme.
56. Akawapelekea ukali wa hasira yake :
Ghadhabu na uchungu na taabu.
57. Kundi la malaika waletao mabaya :
Akaifanyizia hasira yake njia.
58. Wala hakuziepusha roho zao na mauti :
Bali aliiachia tauni uhayi wao.
59. Akampiga killa mzaliwa wa kwanza wa Misri :
Malimbuko ya nguvu katika khema za Ham.
60. Bali aliwaongoza watu wake kama kondoo :
Akawachunga kama kundi jangwani.
61. Akawachukua salama wala hawakuogopa :
Bali bahari iliwafunikiza adui zao.
62. Akawapeleka hatta mpaka wake mta-
katifu :
Mlima huu alioununua kwa mkono wake wa kuume.
63. Akawafukuza mataifa mbele yao, aka-
wapimia urithi kwa kamba :
Akawakalisha kabila za Israeli katika khema zao.
64. Illakini walimjaribu Mungu Aliye juu wakamwasi :
Wala hawakuzishika shuhuda zake.

Zaburi. C

65. Bali walirudi nyuma wakatenda khiyana kama baba zao :
Wakaepea kama upinde usiofaa.
66. Wakamkasirisha kwa mahali pao pa juu :
Wakamtia wivu kwa sanamu zao.
67. Mungu akasikia akaghadhabika :
Akamkataa Israeli kabisa.
68. Akaiacha masikani ya Shilo :
Khema aliyoiweka kati ya wanadamu.
69. Akazitia nguvu zake kifungoni :
Na fakhari yake mkononi mwa adui.
70. Akawatoa watu wake wapigwe kwa upanga :
Akaughadhabikia urithi wake.
71. Moto ukawala vijana wao :
Wanawali wao hawakuimbiwa nyimbo za arusi.
72. Makuhani wao walianguka kwa upanga :
Wala wajane wao hawakuomboleza.
73. Ndipo Bwana akaamka kama aliyelala usingizi :
Kama shujaa apigae kelele baada ya kunywa mvinyo.
74. Akawapiga adui zake akawarudisha nyuma :
Akawatia aibu ya milele.
75. Akaikataa khema ya Yusufu :
Wala hakuichagua kabila ya Efraimi.
76. Bali aliichagua kabila ya Yuda :
Mlima Sayuni alioupenda.
77. Akajenga patakatifu pake kama vilele :
Kama dunia aliyoiweka imara milele.
78. Akamchagua Daudi mtumishi wake :
Akamwondoa katika mazizi ya kondoo.

Zaburi. C

79. Nyuma ya kondoo wanyonyeshao alimwondoa :

Awachunge Yakobo watu wake, na Israeli urithi wake.

80. Akawalisha kwa ukamilifu wa moyo wake :
Akawaongoza kwa busara ya mikono yake.

Utukufu.

Ant. Bwana alijenga patakatifu pake : kama dunia aliyoiweka imara milele.



ZABURI SEHEMU D.

Ant. Bwana ametuokoa : kwa ajili ya Jina lake. Halleluya.

Zab. 106.

1. Mshukuruni Bwana kwa kuwa yu mwema :
Kwa maana fadhili zake ni za milele.
2. Ni nani awezae kuyanena matendo makuu ya Bwana :
Kuzikhubiri sifa zake zote ?
3. Wa kheri washikao hukumu :
Na kutenda haki siku zote.
4. Unikumbuke, Ee Bwana, kwa kibali :
Uliyo nayo kwa watu wako.
5. Unijilie kwa wokofu wako :
Nipate kuuona ukheri wa wateule wako.
6. Nipate kuifurahia furaha ya taifa lako :
Na kujisifu pamoja na watu wako.
7. Tumetenda dhambi pamoja na baba zetu :
Tumetenda maovu, tumefanya yasiyo haki.
8. Baba zetu katika Misri :
Hawakufikiri matendo yako ya ajabu.
9. Hawakukumbuka wingi wa fadhili zako :
Wakaasi penye bahari, bahari ya Sham.
10. Lakini akawaokoa kwa ajili ya Jina lake :
Ayadhihirishe matendo yake makuu.
11. Akaikemea bahari ya Sham ikakauka
Akawaongoza vilindini kana kwamba ni uwanda.
12. Akawaokoa na mkono wa mtu aliye-wachukia :
Na kuwakomboa na mkono wa adui zao.

13. Maji yakawafunika watesi wao :
Hakusalia hatta mmoja wao.
14. Ndipo walipoyaamini maneno yake :
Waliziimba sifa zake.
15. Wakayasahau matendo yake kwa haraka :
Hawakulingojea shauri lake.
16. Bali walitamani sana jangwani :
Wakamjaribu Mungu nyikani.
17. Akawapa walichomtaka :
Akawakondesha roho zao.
18. Wakamhusudu Musa matuoni :
Na Haruni, mtakatifu wa Bwana.
19. Inchi ikapasuka ikammeza Dathani :
Ikaufunika mkutano wa Abirami.
20. Moto ukawaka katika mkutano wao :
Miali yake ikawateketeza wabaya.
21. Walifanya ndama huko Horeb :
Wakaisujudia sanamu iyeyukayo.
22. Wakaubadili utukufu wao :
Kuwa mfano wa ng'ombe mla majani.
23. Wakamsahau Mungu mwokozi wao :
Aliyetenda makuu katika Misri.
24. Matendo ya ajabu katika inchi ya Ham :
Mambo ya kutisha penye bahari ya Sham.
25. Akasema ya kuwa atawaangamiza :
Lakini Musa mteule wake alisimama.
26. Mbele zake kama palipobomolewa :
Illi aigeuze hasira yake asiye akawaharibu.
27. Wakaidharau inchi ile ya kupendeza :
Wala hawakuliamini neno lake.
28. Bali wakanung'unika khemani mwao :
Wala hawakuisikiliza sauti ya Bwana.

29. Ndipo akawainulia mkono wake :
Ya kuwa atawaangamiza jangwani.
30. Ya kuwa atawatawanya wazao wao kati
ya mataifa :
Na kuwatapanya katika inchi mbali
mbali.
31. Wakajiambatiza na Baal Peor :
Wakala dhabihu za wafu.
32. Wakamkasirisha kwa matendo yao :
Tauni ikawashambulia.
33. Ndipo Finehas akasimama akafanya hu-
kumu :
Tauni ikazuiwa.
34. Akahesabiwa kuwa ana haki :
Kizazi baada ya kizazi hatta milele.
35. Wakamghadhabisha penye maji ya Meriba :
Khasara ikampata Musa kwa ajili yao.
36. Kwa sababu waliiasi roho yake :
Akasema yasiyofaa kwa midomo yake.
37. Hawakuwaharibu watu wa inchi :
Kama Bwana alivyowaambia.
38. Bali walijichanganya na mataifa :
Wakajifunza matendo yao.
39. Wakazitumikia sanamu zao :
Nazo zikawa mtego kwao.
40. Naam, walitoa wana wao na binti zao :
Kuwa dhabihu kwa mashetani.
41. Wakamwaga damu isiyo khatiya :
Damu ya wana wao na binti zao.
42. Waliowatoa kuwa dhabihu kwa sanamu
za Kanaani :
Inchi ikatiwa najisi kwa damu.
43. Ndivyo walivyotiwa uchafu kwa kazi zao :
Wakafanya uasherati kwa matendo yao.

Zaburi. E

44. Hasira ya Bwana ikawaka juu ya watu wake :

Akauchukia urithi wake.

45. Akawatia mikononi mwa mataifa :

Na waliowachukia wakawatawala.

46. Adui zao wakawaonea :

Wakatiishwa chini ya mkono wao.

47. Marra nyingi aliwaponya :

Lakini wao walikuwa wakimwasi kwa mashauri yao, wakadhilika katika uovu wao.

48. Illakini aliyaangalia mateso yao :

Aliposikia kilio chao.

49. Akawakumbukia agano lake :

Akawahurumia kwa wingi wa fadhili zake.

50. Akawajalia kuhurumiwa :

Na watu wote waliowateka.

51. Utuokoe, Ee Bwana Mungu wetu :

Utukusanye kwa kututoa katika mataifa.

52. Tulishukuru Jina lako takatifu :

Tuzifanyie shangwe sifa zako.

53. Na ahimidiwe Bwana, Mungu wa Israeli :

Tangu milele hatta milele.

54. Watu wote na waseme, Amin :

Msifuni Bwana.

Utukufu.

Ant. Bwana ametuokoa : kwa ajili ya Jina lake. Halleluya.

ZABURI SEHEMU E.

Ndio Zaburi 106, juu. uk. 93.



ZABURI SEHEMU F.

Siku Kuu za Bwana wetu, Pentekote, na Utatu Mt.

Sala ya Jioni ya 1.

Antifona iliyokhusika.

Zab. 145.

1. Nitakutukuza, Ee Mungu wangu, mfalme :
Nitalihimidi Jina lako milele na milele.
2. Killa siku nitakuhimidi :
Nitalisifu Jina lako milele na milele.
3. Bwana ndiye mkuu mwenye kusifiwa sana :
Na ukuu wake hautambulikani.
4. Kizazi kwa kizazi kitayasifu matendo yako :
Kitayatangaza matendo ya uweza wako.
5. Nitafikiri fakhari ya utukufu wa adhama yako :
Na matendo yako yote ya ajabu.
6. Watu watayataja matendo yako ya kutisha :
Nami nitausimulia ukuu wako.
7. Watahubiri kumbukumbu la wema wako :
Wataimba haki yako.
8. Bwana ana fadhili, yu mwingi wa huruma :
Si mwepesi wa hasira, yu mwingi wa fadhili.
9. Bwana yu mwema kwa watu wote :
Na rehema zake zi juu ya kazi zake zote.
10. Kazi zako zote zitakushukuru, Ee Bwana :
Na watakatifu wako watakuhimidi.
11. Wataunena utukufu wa ufalme wako :
Na kuuhadithia uweza wako.

Zaburi. F

12. Illi kuwajulisha wanadamu matendo ya uweza wako :
Na utukufu wa fakhari ya ufalme wako.
13. Ufalme wako ufalme wa zamani zote :
Na mamlaka yako ya vizazi vyote.
14. Bwana yu amini katika maneno yake yote :
Na mwenye fadhili katika kazi zake zote.
15. Bwana huwategemeza wote waangukao :
Huwainua wote walioinama chini.
16. Macho ya watu wote yakuelekea Wewe :
Nawe huwapa chakula chao wakati wake.
17. Waufumbua mkono wako :
Washibisha killa kilicho hayi matakwa yake.
18. Bwana yu mwenye haki katika njia zake zote :
Na mwenye fadhili katika kazi zake zote.
19. Bwana yu karibu na wote wamwitao :
Wote wamwitao kwa uaminifu.
20. Atawafanyia wamchao matakwa yao :
Nae atasikia kilio chao na kuwaokoa.
21. Bwana huwahifadhi wote wampendao :
Na wote wasio haki atawaangamiza.
22. Kinywa changu kitazinena sifa za Bwana :
Wote wenye mwili na walihimidi Jina lake takatifu milele na milele.

Utukufu.

Zab. 149.

1. Mwimbieni Bwana uimbo mpya :
Sifa zake katika kusanyiko la watakatifu.
2. Israeli na amfurahie Yeye aliyemfanya :
Wana wa Sayuni wamshangilie mfalme wao.

Zaburi. F

3. Na walisifu Jina lake kwa kucheza :
Kwa ngoma na kinubi wamwimbie.
4. Kwa kuwa Bwana awaridhia watu wake :
Huwapamba wenye upole kwa wokofu.
5. Watakatifu waushangilie utukufu :
Waimbe kwa sauti kuu vitandani mwao.
6. Sifa kuu za Mungu ziwe vinywani mwao :
Na upanga mkali kuwili mikononi mwao.
7. Illi kufanya kisasi juu ya mataifa :
Na adhabu juu ya kabila za watu.
8. Wawafunge wafalme wao kwa minyororo :
Na wakuu wao kwa pingu za chuma.
9. Kuwafanyia hukumu iliyoandikwa :
Hii ndiyo heshima ya watakatifu wake wote.

Utukufu.

Zab. 150.

1. Msifuni Mungu katika patakatifu pake :
Msifuni katika nafasi ya uweza wake.
2. Msifuni kwa matendo yake makuu :
Msifuni kwa kadiri ya wingi wa ukuu wake.
3. Msifuni kwa mvumo wa baragumu :
Msifuni kwa kinanda na kinubi.
4. Msifuni kwa ngoma na kucheza :
Msifuni kwa zeze na filimbi.
5. Msifuni kwa matoazi yaliayo :
Msifuni kwa matoazi yavumayo sana.
6. Killa mwenye pumzi na amsifu Bwana :
Msifuni Bwana.

Utukufu.

Antifona iliyokhusika.

Sala ya Jioni ya 2.

*Antifona iliyokhusika.**Zab. IIO.*

1. Neno la Bwana kwa bwana wangu :
Uketi mkono wangu wa kuume.
2. Hatta niwafanyapo adui zako :
Kuwa chini ya miguu yako.
3. Fimbo ya nguvu zako :
Bwana atainyosha toka Sayuni.
4. Uwe na enzi kati ya adui zako :
Watu wako wanajitoa kwa khiari.
5. Siku ya uwezo wako :
Kwa uzuri wa utakatifu.
6. Tokea tumbo la assubuhi :
Unao umande wa ujana wako.
7. Bwana ameapa wala hataghairi :
Ndiwe kuhani milele kwa mfano wa
daraja la Mekizedeki.
8. Bwana mkono wako wa kuume :
Atawaseta wafalme siku ya ghadhabu
yake.
9. Atahukumu kati ya mataifa, ataijaza inchi
mizoga :
Ataseta kichwa katika inchi nyingi.
10. Atakunywa maji ya mto njiani :
Kwa hiyo atainua kichwa chake.

Utukufu.

Zab. III.

1. Nitamshukuru Bwana kwa moyo wangu
wote :
Katika baraza la wanyofu wa moyo na
katika mkutano.
2. Matendo ya Bwana ni makuu :
Yafikiriwa sana na wapendezwao nayo.
3. Kazi yake ni heshima na adhama :
Na haki yake yakaa milele.
4. Amefanya ukumbusho wa matendo yake
ya ajabu :
Bwana yu mwenye fadhili na rehema.
5. Amewapa wamchao chakula :
Atalikumbuka agano lake milele.
6. Amewajulisha watu wake uwezo wa ma-
tendo yake :
Kwa kuwapa urithi wa mataifa.
7. Matendo ya mikono yake ni kweli na
hukumu :
Maagizo yake yote ni amini.
8. Yamethubutika milele na milele :
Yamefanywa katika kweli na adili.
9. Amewapelekea watu wake ukombozi,
ameamuru agano lake liwe la milele :
Jina lake li takatifu la kuogopwa.
10. Kumcha Bwana ndio mwanzo wa hekima,
wote wafanyao haya wana akili njema :
Sifa zake zakaa milele.

Utukufu.

Zab. 112.

1. Yu kheri mtu yule amchae Bwana :
Apendezwae sana na maagizo yake.
2. Wazao wake watakuwa hodari duniani :
Kizazi cha wenye adili kitabarikiwa.
3. Nyumbani mwake mna utajiri na mali :
Na haki yake yakaa milele.
4. Nuru huwazukia wenye adili gizani :
Ana fadhili na huruma na haki.
5. Yu kheri atendae fadhili na kukopesha :
Atengenezae mambo yake kwa haki.
6. Kwa maana hataondoshwa kamwe :
Mwenye haki atakumbukwa milele.
7. Hataogopa khabari mbaya :
Moyo wake u imara ukimtumaini Bwana.
8. Moyo wake umethubutika hataogopa :
Hatta atakapowaona adui zake.
9. Amekirimu, amewapa maskini, haki yake
yakaa milele :
Pembe yake itatukuzwa kwa utukufu.
10. Asiyeye haki ataona na kusikitika, atasaga
meno yake na kuyeyuka :
Tamaa ya wasio haki itapotea.

Utukufu.

Zab. 113.

1. Sifuni, enyi watumishi wa Bwana :
Lisifuni Jina la Bwana.
2. Jina la Bwana lihimidiwe :
Tangu leo na hatta milele.
3. Toka maawio ya jua hatta machweo yake :
Jina la Bwana husifiwa.
4. Bwana ni mkuu juu ya mataifa yote :
Na utukufu wake juu ya mbingu.
5. Ni nani aliye mfano wa Bwana :
Mungu wetu ajikuzae aketi ?
6. Ajinyenyekeae atazame :
Mbinguni na duniani ?
7. Humwinua mnyonge kutoka mavumbini :
Humpandisha maskini kutoka jaani.
8. Amketishe pamoja na wakuu :
Pamoja na wakuu wa watu wake.
9. Huweka nyumbani mwanamke aliye tassa :
Yu mama ya watoto mwenye furaha.
Utukufu.

Zab. 117.

1. Msifuni Bwana, enyi mataifa yote :
Mhimidini, enyi watu wote.
2. Maana fadhili zake kwetu sisi ni kuu :
Na uaminifu wa Bwana ni wa milele.
Utukufu.

Antifona iliyokhusika.



ZABURI SEHEMU G.

Siku Kuu za Mariamu Mb.

Sala ya Jioni (ya 1 na ya 2).

Ant. Tazama, mimi mjakazi wa Bwana : na iwe kwangu kwa neno lako.

Zab. 110.

1. Neno la Bwana kwa bwana wangu :
Uketi mkono wangu wa kuume.
2. Hatta niwafanyapo adui zako :
Kuwa chini ya miguu yako.
3. Fimbo ya nguvu zako :
Bwana atainyosha toka Sayuni.
4. Uwe na enzi kati ya adui zako :
Watu wako wanajitoa kwa khiari.
5. Siku ya uwezo wako :
Kwa uzuri wa utakatifu.
6. Tokea tumbo la assubuhi :
Unao umande wa ujana wako.
7. Bwana ameapa wala hataghairi :
Ndiwe kuhani milele kwa mfano wa daraja la Melkizedeki.
8. Bwana mkono wako wa kuume :
Atawaseta wafalme siku ya ghadhabu yake.
9. Atahukumu kati ya mataifa, ataijaza inchi mizoga :
Ataseta kichwa katika inchi nyingi.
10. Atakunywa maji ya mto njiani :
Kwa hiyo atainua kichwa chake.
Utukufu.

Zab. 122.

1. Nalifurahi waliponiambia :
Tutakwenda nyumbani kwa Bwana.
2. Miguu yetu ilikuwa ikisimama :
Ndani ya malango yako, Ee Yerusalemi.
3. Yerusalemi uliojengwa :
Kama mji ulioshikamana.
4. Huko ndiko walikopanda kabila :
Kabila za Bwana.
5. Ushuhuda kwa Israeli :
Walishukuru Jina la Bwana.
6. Maana huko viliwekwa viti vya hukumu :
Viti vya enzi vya nyumba ya Daudi.
7. Utakieni Yerusalemi amani :
Na wafanikiwe wakupendao.
8. Amani na ikae ndani ya kuta zako :
Na kufanikiwa ndani ya majumba yako.
9. Kwa ajili ya ndugu zangu na rafiki zangu :
Niseme sasa, Amani ikae nawe.
10. Kwa ajili ya nyumba ya Bwana Mungu wetu :
Nikutafutie mema.
Utukufu.

Zab. 127.

1. Bwana asipoijenga nyumba :
Waijengao wafanya kazi burre.
2. Bwana asipoulinda mji :
Yeye aulindae akesha burre.
3. Kazi yenu ni burre, ninyi mnaoamka mapema :
Na kukawia kwenda kulala.
4. Mnapokula chakula cha taabu :
Humpa mpenzi wake usingizi.

Zaburi. G

5. Wana ndio walio urithi wa Bwana :
Uzao wa tumbo ni thawabu.
6. Kama mishale mkononi mwa shujaa :
Ndivyo walivyo wana wa ujanani.
7. Yu kheri mtu yule :
Aliyelijaza podo lake hivyo.
8. Naam, hawataona aibu :
Wanapokisema na adui langoni.
Utukufu.

Zab. 149.

1. Mwimbieni Bwana uimbo mpya :
Sifa zake katika kusanyiko la watakatifu.
2. Israeli na amfurahie Yeye aliyemfanya :
Wana wa Sayuni wamshangilie mfalme wao.
3. Na walisifu Jina lake kwa kucheza :
Kwa ngoma na kinubi wamwimbie.
4. Kwa kuwa Bwana awaridhia watu wake :
Huwapamba wenye upole kwa wokofu.
5. Watakatifu waushangilie utukufu :
Waimbe kwa sauti kuu vitandani mwao.
6. Sifa kuu za Mungu ziwe vinywani mwao :
Na upanga mkali kuwili mikononi mwao.
7. Illi kufanya kisasi juu ya mataifa :
Na adhabu juu ya kabila za watu.
8. Wawafunge wafalme wao kwa minyororo :
Na wakuu wao kwa pingu za chuma.
9. Kuwafanyia hukumu iliyoandikwa :
Hii ndiyo heshima ya watakatifu wake wote.
Utukufu.

Ant. Tazama, mimi mjakazi wa Bwana : na
iwe kwangu kwa neno lako.



ZABURI SEHEMU H.

Siku Kuu za Mitume na Watunga Injili,
Yusuf Mt., Yohana Mbatizaji, Mikael Mt. na
Malaika zote, Watakatifu wote, Kutabaruku
Kanisa, na Mtakatifu wa Mtaani.

Sala ya Jioni ya 1.

Antifona iliyokhusika.

Zab. 139.

1. Ee Bwana, umenichunguza na kunijua
Wewe wajua kuketi kwangu.
2. Wajua na kuondoka kwangu :
Umefhamu wazo langu tokea zamani.
3. Umeupepeta mwenendo wangu na kulala
kwangu :
Umeelewa na njia zangu zote.
4. Maana hamna neno ulimini mwangu :
Usilolijua kabisa, Ee Bwana.
5. Umenihusuru nyuma na mbele :
Ukanishika kwa mkono wako.
6. Maarifa haya ni ya ajabu, yanishinda
mimi :
Hayadirikiki siwezi kuyafikia.
7. Niende wapi nijiepushe na roho yako :
Niende wapi niukimbie uso wako ?
8. Kama ningepanda mbinguni, Wewe uko :
Ningefanya kuzimu kitanda changu,
Wewe uko.

Zaburi. H

9. Ningezitwaa mbawa za assubuhi :
Na kukaa pande za mwisho za bahari.
10. Huko nako mkono wako utaniongoza :
Na mkono wako wa kuume utanishika.
11. Kama nikisema, Hakika giza litanifunika :
Na nuru inizungukayo ikawa usiku.
12. Giza nalo halikufichi kitu, bali usiku huan-
gaza kama mchana :
Giza na mwanga kwako ni sawasawa.
13. Maana Wewe ndiwe uliyeniumba mtima
wangu :
Uliniunga tumboni mwa mama yangu.
14. Nitakushukuru kwa kuwa nimeumbwa :
Kwa jinsi ya ajabu ya kutisha.
15. Matendo yako ya ajabu :
Na roho yangu yajua sana.
16. Mifupa yangu haikusetirika kwako :
Nilipoumbwa kwa siri.
17. Nilipoungwa kwa ustadi pande za chini
za inchi :
Macho yako yaliniona kabla sijakamilika.
18. Chuoni mwako ziliandikwa zote pia :
Siku zilizoamriwa kabla hazijawa bado.
19. Kwangu mimi fikara zako zina thamani
nyingi, Ee Mungu :
Ee ajabu ya wingi wa jumla yake !
20. Kama ningezihesabu zi nyingi kuliko
mchanga :
Niamkapo nikali pamoja nawe.
21. Ningependa kama ungewaua waovu, Ee
Mungu :
Ondokeni kwangu, enyi watu wa damu.
22. Kwa maana wakuasi kwa ubaya :
Adui zako wakutaja Jina lako burre.

Zaburi. H

23. Nisiwachukie, Ee Bwana, wanaokuchukia :
Nisikirihike nao wakuasio ?
24. Nawachukia kwa ukomo wa chuki :
Wamekuwa adui kwangu.
25. Unichunguze, Ee Mungu, ujue moyo
wangu :
Unijaribu, ujue mawazo yangu.
26. Ukaone kama iko njia iletayo majuto ndani
yangu :
Ukaniongoze katika njia ya milele.
Utukufu.

Zab. 145.

1. Nitakutukuza, Ee Mungu wangu, mfalme :
Nitalihimidi Jina lako milele na milele.
2. Killa siku nitakuhimidi :
Nitalisifu Jina lako milele na milele.
3. Bwana ndiye mkuu mwenye kusifiwa
sana :
Na ukuu wake hautambulikani.
4. Kizazi kwa kizazi kitayasifu matendo yako :
Kitayatangaza matendo ya uweza wako.
5. Nitaifikiri fakhari ya utukufu wa adhama
yako :
Na matendo yako yote ya ajabu.
6. Watu watayataja matendo yako ya
kutisha :
Nami nitausimulia ukuu wako.
7. Watahubiri kumbukumbu la wema wako :
Wataimba haki yako.
8. Bwana ana fadhili, yu mwingi wa huruma :
Si mwepesi wa hasira, yu mwingi wa
fadhili.

9. Bwana yu mwema kwa watu wote :
Na rehema zake zi juu ya kazi zake zote.
10. Kazi zako zote zitakushukuru, Ee Bwana :
Na watakatifu wako watakuhimidi.
11. Wataunena utukufu wa ufalme wako :
Na kuuhadithia uweza wako.
12. Ili kuwajulisha wanadamu matendo ya
uweza wako :
Na utukufu wa fakhari ya ufalme wako.
13. Ufalme wako ufalme wa zamani zote :
Na mamlaka yako ya vizazi vyote.
14. Bwana yu amini katika maneno yake yote :
Na mwenye fadhili katika kazi zake zote.
15. Bwana huwategemeza wote waangukao :
Huwainua wote walioinama chini.
16. Macho ya watu wote yakuelekea Wewe :
Nawe huwapa chakula wakati wake.
17. Waufumbua mkono wako :
Washibisha killa kilicho hayi matakwa
yake.
18. Bwana yu mwenye haki katika njia zake
zote :
Na mwenye fadhili katika kazi zake zote.
19. Bwana yu karibu na wote wamwitao :
Wote wamwitao kwa uaminifu.
20. Atawafanyia wamchao matakwa yao :
Nae atasikia kilio chao na kuwaokoa.
21. Bwana huwahifadhi wote wampendao :
Na wote wasio haki atawaangamiza.
22. Kinywa changu kitazinena sifa za Bwana :
Wote wenye mwili na walihimidi Jina
lake takatifu milele na milele.

Utukufu.

Zab. 150.

1. Msifuni Mungu katika patakatifu pake :
Msifuni katika nafasi ya uweza wake.
2. Msifuni kwa matendo yake makuu :
Msifuni kwa kadiri ya wingi wa ukuu
wake.
3. Msifuni kwa mvumo wa baragumu :
Msifuni kwa kinanda na kinubi.
4. Msifuni kwa ngoma na kucheza :
Msifuni kwa zeze na filimbi.
5. Msifuni kwa matoazi yaliayo :
Msifuni kwa matoazi yavumayo sana.
6. Killa mwenye pumzi na amsifu Bwana :
Msifuni Bwana.

Utukufu.

Antifona iliyokhusika.

Sala ya Jioni ya 2.

Zaburi 110. 111. 112. 113. 117.

Tazama ukarasa wa 100.





ZABURI SEHEMU I.

S. B. ya Mateso, na S. B. ya Mitende.

Ant. Uniponye.*Zab. 22.*

1. Ee Mungu wangu, Ee Mungu wangu :
Mbona umeniacha ?
2. Mbona U mbali na wokofu wangu :
Na maneno ya kuugua kwangu ?
3. Ee Mungu wangu, nalia mchana lakini
hujibu :
Na wakati wa usiku lakini sipati raha.
4. Na Wewe U Mtakatifu :
Uketiye juu ya sifa za Israeli.
5. Baba zetu walikutumaini Wewe :
Walitumaini na Wewe ukawaokoa.
6. Walikulilia Wewe wakaokoka :
Walikutumaini wala hawakuaibika.
7. Lakini mimi ni mdudu wala si mtu :
Laumu ya wanadamu na mzaha wa
watu.
8. Wote wanionao hunicheka sana :
Hunifyonya wakitikisa vichwa vyao.
9. Umtegemee Bwana, na amponye :
Na amwokoe sasa, maana apendezwa
nae.
10. Naam, Wewe ndiwe uliyenitoa tumboni :
Ulinitumainisha nilipokuwa maziwani
mwa mama yangu.
11. Kwako nalitupwa tokea tumboni :
Toka tumboni mwa mama yangu ndiwe
Mungu wangu.

12. Usiwe mbali nami maana taabu i karibu :
Kwa maana hakuna msaidizi.
13. Mafahali wengi wamenizunguka :
Walio hodari wa Bashani wamenisonga.
14. Wananifumbulia vinywa vyao :
Kama simba apapurae na kunguruma.
15. Nimemwagika kama maji :
Mifupa yangu yote imeteguka.
16. Moyo wangu umekuwa kama nta :
Umeyeyuka ndani ya mtima wangu.
17. Nguvu zangu zimekauka kama gae :
Ulimi wangu waambatana na taya zangu.
18. Unaniweka katika mavumbi ya mauti :
Kwa maana mbwa wamenizunguka.
19. Kusanyiko la waovu wamenisonga :
Wamenizua mikono na miguu.
20. Naweza kuhesabu mifupa yangu yote :
Wao wananitazama na kunikodolea
macho.
21. Wanagawanya nguo zangu :
Na vazi langu wanalipigia kura.
22. Nawe, Bwana, usiwe mbali :
Ee nguvu zangu, fanya haraka kuni-
saidia.
23. Uniponye roho yangu na upanga :
Mpenzi wangu na nguvu za mbwa.
24. Kinywani mwa simba uniokoe :
Naam, toka pembe za nyati umenijibu.
25. Nitalikhubiri Jina lako kwa ndugu zangu :
Katikati ya kusanyiko nitakusifu.
26. Ninyi mnaomcha Bwana, msifuni :
Enyi nyote mlio wazao wa Yakobo,
mtukuzeni, mcheni, enyi nyote mlio
wazao wa Israeli.

Zaburi. I

27. Maana hakulidharau teso la mteswa :
Wala hakuchukizwa nalo.
28. Wala hakumficha uso wake :
Bali alipomlilia akamsikia.
29. Kwako zinatoka sifa zangu :
Katika kusanyiko kubwa.
30. Nitaziondoa nadhiri zangu :
Mbele yao wamchao.
31. Wapole watakuja na kushiba :
Wamtafutao Bwana watamsifu.
32. Mioyo yenu na iishi milele :
Miisho yote ya dunia itakumbuka.
33. Watamrejea Bwana :
Jamaa zote za mataifa watasujudu mbele zake.
34. Maana ufalme una Bwana :
Nae ndiye awatawalae mataifa.
35. Wakwasi wote wa dunia watakula na kusujudu :
Mbele zake huinama wote washukao mavumbini.
36. Naam, yeye asiyeweza kujihuisha roho yake :
Wazao wake watamtumikia.
37. Zitasimuliwa khabari za Bwana :
Kwa kizazi kitakachokuja.
38. Nao watawakhubiri watakaozaliwa haki yake :
Ya kwamba ndiye aliyeyafanya.
Utukufu.

Zaburi. I

Zab. 88.

1. Ee Bwana, Mungu wa wokofu wangu :
Mchana na usiku nimelia mbele zako.
2. Maombi yangu yafike mbele zako.
Utegee ukelele wangu sikio lako.
3. Maana roho yangu imeshiba taabu :
Na uhayi wangu umekaribia kuzimu.
4. Nimehesabiwa pamoja nao washukao shimoni :
Nimekuwa kama mtu asiye msaada.
5. Miongoni mwao waliokufa nimetupwa :
Kama waliouawa walalao makaburini.
6. Ambao huwakumbuki tena :
Nao wametengwa mbali ya mkono wako.
7. Umenilaza katika chini ya shimo :
Katika mahali penye giza vilindini.
8. Ghadhabu yako imenilemea :
Umenitesa kwa mawimbi yako yote.
9. Wanijuao umewatenga nami :
Umenifanya kuwa chukizo kwao.
10. Nimefungwa wala siwezi kutoka :
Jicho langu limefifia kwa ajili ya mateso.
11. Nimekuita, Ee Bwana, killa siku :
Nimekunyoshea Wewe mikono yangu.
12. Wafu je ! utawafanyia miujiza :
Au waliofariki watasimama na kukuhimidi ?
13. Fadhili zako zitasimuliwa kaburini :
Au uaminifu wako katika uharibifu ?
14. Miujiza yako itajulika gizani :
Na haki yako katika inchi ya usahaulifu ?

Zaburi. I

15. Lakini mimi nimekulilia Wewe, Ee Bwana :
Na assubuhi maombi yangu yatakuwasilia.
16. Ee Bwana, ya nini kuitupa roho yangu :
Na kunificha uso wako ?
17. Nateswa mimi katika hali ya kufa tangu
ujana :
Nimevumilia vitisho vyako na kufadhika.
18. Hasira zako kali zimepita juu yangu :
Maogofyo yako yameniangamiza.
19. Yamenizunguka kama maji mchana kuta :
Yamenisonga yote pamoja.
20. Mpenzi na rafiki umewatenga nami :
Nao wanijuao giza.

Utukufu.

Ant. Uniponye na adui zangu, Ee Mungu wangu : uniponye nao wafayao maovu.



ZABURI SEHEMU J.

Alkhamisi ya Amri na Ijumaa Kuu.

Ant. Nitakipokea kikombe cha wokofu :
nitalitangaza Jina la Bwana.

Zab. 116.

1. Nampenda kwa kuwa Bwana anasikiliza :
Sauti yangu na dua zangu.
2. Kwa maana amenitegea sikio lake :
Kwa hiyo nitamwita siku zangu zote.
3. Kamba za mauti zilinizunguka :
Shidda za kuzimu zilinipata.
4. Naliona taabu na huzuni :
Nikaliita Jina la Bwana.
5. Ee Bwana, nakuomba sana :
Uniokoe roho yangu.
6. Bwana yu mwenye neema na haki :
Naam, Mungu wetu yu mwenye rehema.
7. Bwana huwalinda wasio hila :
Nalidhilika akaniokoa.
8. Urudi, Ee roho yangu, rahani mwako :
Kwa kuwa Bwana amekutendea kwa ukarimu.
9. Maana umeniponya roho yangu na mauti,
macho yangu na machozi :
Na miguu yangu na kuanguka.
10. Nitaenenda mbele za Bwana :
Katika inchi za wahayi.

Zaburi. J

11. Naliamini, maana nitasema :
Mimi naliteswa sana.
12. Mimi nalisema katika khofu yangu :
Wanadamu wote ni wawongo.
13. Nimrudishie Bwana nini :
Kwa ukarimu wake wote alionitendea ?
14. Nitakipokea kikombe cha wokofu :
Nitalitangaza Jina la Bwana.
15. Nitaziondoa nadhiri zangu kwa Bwana :
Naam, mbele ya watu wake wote.
16. Ina thamani machoni pa Bwana :
Mauti ya watakatifu wake.
17. Nakusihi, Bwana, maana ni mtumishi wako :
Mtumishi wako, mwana wa mjakazi wako, umefungua vifungo vyangu.
18. Nitakutolea dhabihu ya kushukuru :
Nitalitangaza Jina la Bwana.
19. Nitaziondoa nadhiri zangu kwa Bwana :
Naam, mbele ya watu wake wote.
20. Katika nyua za nyumba ya Bwana :
Ndani yako, Ee Yerusalemi.

(Isisemwe Utukufu.)

Zab. 120.

1. Katika shidda yangu nalimlilia Bwana :
Nae akaniitikia.
2. Ee Bwana, uiponye roho yangu :
Na midomo ya uwongo na ulimi wa hila.
3. Akupe nini, akuzidishie nini :
Ee ulimi wa hila ?
4. Mishale ya mtu hodari iliyotiwa ncha :
Pamoja na makaa ya mretemi.

Zaburi. J

5. Ole wangu mimi :
Kwa kuwa nimekaa katika Meshek.
6. Na kufanya masikani yangu :
Kati ya khema za Kedari.
7. Roho yangu imekaa siku nyingi :
Pamoja nae aichukiae amani.
8. Mimi wa amani :
Bali ninenapo wao huelekea vita.
(Isisemwe Utukufu.)
Zab. 140.
1. Uniokoe, Ee Bwana, na mtu mbaya :
Unihifadhi na mtu wa jeuri.
2. Waliowaza mabaya mioyoni mwao :
Killa siku huondokesha vita.
3. Wamenoa ndimi zao kama nyoka :
Sumu ya pili i chini ya midomo yao.
4. Unilinde, Ee Bwana, na mikono ya mtu asiye haki :
Unihifadhi na mtu wa jeuri.
5. Waliowaza kupotosha khatua zangu :
Wenye kiburi wameficha mitego na kamba waninase.
6. Wametandika wavu kando ya njia :
Wameniwekea matanzi.
7. Nimemnena Bwana, Ndiwe Mungu wangu :
Ee Bwana, usikie sauti ya dua zangu.
8. Ee MUNGU Bwana, nguvu za wokofu wangu :
Umefunika kichwa changu siku ya vita.
9. Ee Bwana, usimpe asiye haki tamaa zake :
Usiifanikishe hila yake.
10. Watu wanaonizunguka wainuapo vichwa vyao :
Madhara ya midomo yao yawafunike.

Zaburi. J

11. Makaa ya moto yawaangukie, watupwe motoni :
Na katika mashimo wasipate kusimama tena.
12. Msingiziaji hatawekwa imara katika inchi :
Mtu wa jeuri mabaya yatamwinda hatta kumwangamiza.
13. Najua ya kuwa Bwana atamfanyia mnyonge hukumu :
Na wahitaji haki yao.
14. Hakika wenye haki watalishukuru Jina lako :
Wenye adili watakaa mahali ulipo Wewe.
(*Isisemwe Utukufu.*)
Ant. Nitakipokea kikombe cha wokofu : nitangaza Jina la Bwana.

MKESHA WA PASAKA

Ant. Halleluya, Halleluya : Halleluya.

Zab. 117. peke yake.

1. Msifuni Bwana, enyi mataifa yote :
Mhimidini, enyi watu wote.
2. Maana fadhili zake kwetu sisi ni kuu :
Na uaminifu wa Bwana ni wa milele.

Utukufu.

Ant. Halleluya, Halleluya : Halleluya.



SALA ZA KUOMBEA WAFU

¶ *Siku ya Ukumbusho wa Roho zote kila Antifona isemwe yote mbele ya Zaburi na baada yake.*

¶ *Siku yo yote ikisemwa sala hii peke yake, wala si marra baada ya Sala ya Jioni ya siku ile, zisemwe kwanza sala za siri ilivyo kawaida.*

¶ *Siku yo yote ikisemwa sala hii marra baada ya Sala ya Jioni ya siku ile, mwisho wa Sala ya Jioni ya siku isisemwe, Roho za waaminifu, etc. bali marra hufuata Sala ya Jioni ya Wafu.*

Sala ya Jioni.

¶ *Inaanzia ZABURI.*

Ant. Nitaenenda mbele za Bwana : katika inchi za wahayi.

Zab. 116.

1. Nampenda kwa kuwa Bwana anasikiliza :
Sauti yangu na dua zangu.
2. Kwa maana amenitegea sikio lake :
Kwa hiyo nitamwita siku zangu zote.
3. Kamba za mauti zilizunguka :
Shida za kuzimu zilinipata.
4. Naliona taabu na huzuni :
Nikaliita Jina la Bwana.
5. Ee Bwana, nakuomba sana :
Unikoe roho yangu.
6. Bwana yu mwenye neema na haki :
Naam, Mungu wetu yu mwenye rehema.

Sala za Wafu

7. Bwana huwalinda wasio hila :
Nalidhilika akaniokoa.
8. Urudi, Ee roho yangu, rahani mwako :
Kwa kuwa Bwana amekutendea kwa ukarimu.
9. Maana umeniponya roho yangu na mauti,
macho yangu na machozi :
Na miguu yangu na kuanguka.
10. Nitaenenda mbele za Bwana :
Katika inchi za wahayi.
Raha ya milele :
Uwajalie, Ee Bwana.
Na nuru ya daima :
Iwaangaze.

Ant. Nitaenenda mbele za Bwana : katika inchi za wahayi.

Ant. Ole wangu mimi, Ee Bwana : kwa kuwa kukaa kwangu kumezidishwa.

Zab. 120.

1. Katika shidda yangu nalimlilia Bwana :
Nae akaniitikia.
2. Ee Bwana, uiponye roho yangu :
Na midomo ya uwongo na ulimi wa hila.
3. Akupe nini, akuzidishie nini :
Ee ulimi wa hila ?
4. Mishale ya mtu hodari iliyotiwa ncha :
Pamoja na makaa ya mretemi.
5. Ole wangu mimi :
Kwa kuwa nimekaa katika Meshek.
6. Na kufanya masikani yangu :
Kati ya khema za Kedari.

Sala za Wafu

7. Roho yangu imekaa siku nyingi :
Pamoja nae aichukiae amani.
8. Mimi wa amani :
Bali ninenapo wao huelekea vita.
Raha ya milele.

Ant. Ole wangu mimi, Ee Bwana : kwa kuwa kukaa kwangu kumezidishwa.

Ant. Bwana atakulinda na mabaya yote :
Bwana atakulinda roho yako.

Zab. 121.

1. Nitainua macho yangu niitazame milima :
Msaada wangu utatoka wapi ?
2. Msaada wangu u kwa Bwana :
Aliyezifanya mbingu na inchi.
3. Asiache mguu wako usogezwe :
Asisinzie akulindae.
4. Hatasinzia wala hatalala usingizi :
Yeye aliye mlinzi wa Israeli.
5. Bwana ndiye mlinzi wako :
Bwana ni uvuli mkono wako wa kuume.
6. Jua halitakupiga mchana :
Wala mwezi wakati wa usiku.
7. Bwana atakulinda na mabaya yote :
Atakulinda roho yako.
8. Bwana atakulinda utokapo na uingiapo :
Tangu sasa na hatta milele.
Raha ya milele.

Ant. Bwana atakulinda na mabaya yote :
Bwana atakulinda roho yako.

Sala za Wafu

*Ant. Kama ungehesabu maovu, Ee Bwana :
Ee Bwana, nani angesimama ?*

Zab. 130.

1. Toka vilindini nimekulilia, Ee Bwana :
Ee Bwana, uisikilize sauti yangu.
2. Masikio yako na yaiangalie :
Sauti ya dua zangu.
3. Kama ungehesabu maovu, Ee Bwana :
Ee Bwana, nani angesimama ?
4. Lakini kwako kuna samaha :
Illi uogopwe.
5. Nimemngoja Bwana, roho yangu imengoja :
Na neno lake nimelitumainia.
6. Roho yangu inamngoja Bwana kuliko
walinzi waingojavyo assubuhi :
Naam, kuliko walinzi assubuhi.
7. Ee Israeli, umtarajie Bwana :
Maana kwa Bwana kuna fadhili.
8. Na kwake kuna ukombozi mwingi :
Nae atamkomboa Israeli na maovu yake
yote.

Raha ya milele.

*Ant. Kama ungehesabu maovu, Ee Bwana :
Ee Bwana, nani angesimama ?*

*Ant. Fadhili zako, Ee Bwana, ni za milele :
usiziache kazi za mikono yako.*

Zab. 138.

1. Nitakushukuru kwa moyo wangu wote :
Mbele za miungu nitakuimbia zaburi.
2. Nitasujudu nikikabili hekalu lako takatifu :
Nitalishukuru Jina lako,

Sala za Wafu

3. Kwa ajili ya fadhili zako na uaminifu
wako :

Kwa maana umelikuza Jina lako juu ya
yote.

4. Siku ile niliyokuita ulinjibu :
Ukanifariji roho kwa kunitia nguvu.
5. Wafalme wote wa dunia watakushukuru,
Ee Bwana :
Watakaposikia maneno ya kinywa chako.
6. Naam, wataziimba njia za Bwana :
Kwa maana utukufu wa Bwana ni
mkuu.
7. Maana ingawa Bwana yuko juu amwona
mnyenyekevu :
Nae amjua mwenye kujivuna tokea
mbali.
8. Nijapokwenda kati ya shidda utanihuisha :
Utaunyosha mkono wako juu ya gha-
dhabu ya adui zangu.
9. Na mkono wako wa kuume utaniokoa :
Bwana atanitimizia mambo yangu.
10. Fadhili zako, Ee Bwana, ni za milele :
Usiziache kazi za mikono yako.

Raha ya milele.

*Ant. Fadhili zako, Ee Bwana, ni za milele :
usiziache kazi za mikono yako.*

SOMO na UIMBO hapana.

¶. Nalisikia sauti kutoka mbinguni ikisema.
R7. Wa kheri wafu wafao katika Bwana.

*Ant. Mag. Yote anipayo Baba itakuja kwangu :
nae ajae kwangu sitamtupa nje kamwe.*

MAGNIFICAT, na *mwishoni*, Raha ya milele.

Sala za Wafu

¶ *Ikiisha* MAGNIFICAT na Antifona yake, marra husemwa na wote, wakipiga magoti,

Baba yetu. (*kimoyomoyo*).

∇. Usitutie majaribuni.

R7. Lakini utuokoe na maovu.

*∇. Ee Bwana, uziokoe roho zao.

R7. Na milango ya Jehanum.

∇. Wastarehe katika amani.

R7. *Amin.*

∇. Ee Bwana, usikie kuomba kwangu.

R7. Kilio changu kikufikie.

∇. Bwana akae nanyi.

R7. Akae na roho yako.

Tuombe.

Ee Mungu, umewaumba waaminifu wote na kuwaokoa : Uzijalie roho za watumishi na wajakazi wako ondoleo la dhambi zao zote ; wapewe, kwa sala za pendo, masamaha waliyoyataka siku zote. Uishiye.

∇. Bwana akae nanyi.

R7. Akae na roho yako.

∇. Raha ya milele uwajalie, Ee Bwana.

R7. Na nuru ya daima iwaangaze.

Wastarehe katika amani.

R7. *Amin.*

**Ikisemwa sala hii kwa ajili ya mtu mmoja,*

∇. Ee Bwana, uikoe roho yake.

R7. Na milango ya Jehanum.

∇. Astorehe katika amani.

R7. *Amin.*

Walakini isitumike jumla ya umoja mahali pengine.

Sala za Wafu

¶ *Ni halali kusema sala hii marra moja kwa mwezi kutangulia Missa ya Wafu ya kwanza ya mwezi; yaani isemwe jioni panapo Missa ya Wafu assubuhi ifuatayo.*

¶ *Na vile vile marra moja kwa juma Wakati wa Majilio na Kwaresima.*

¶ *Walakini Antifona zisisemwe yote mbele ya Zaburi wala mbele ya Magnificat, illa hatta mwisho wa italics tu.*

¶ *Aidha, yafaa kusema sala hii kwa ajili ya mtu fulani siku ya kufa kwake, au kuzikwa kwake, au siku ya ukumbusho wake; au kwa ajili ya watu fulani vile vile.*

¶ *Tena, ikiwa hivyo, Antifona na zisemwe yote mbele ya Zaburi na Magnificat na baadae, walakini Sala na ibadilirwe hivi :*

(1) *Askofu au Kasisi.*

Ee Mungu ulimkubali mtumishi wako N. katika cheo cha Uaskofu (au Ukasisi) wa Mwana wako : Usikie kuomba kwetu ; umjalie furaha ya milele pamoja na Maaskofu (au Makasisi) wako waaminifu. Kwa Yeye. Aishiye.


(2) *Siku ya kufa au ya kuzikwa.*

Tunakuomba, Ee Bwana, uighofiri roho ya mwanawo N. aliyefariki katika dunia illi akuishie Wewe : Umsamehe yote aliyokukosa kwa udhaifu wake wa ubinadamu ; ukamsafishe kwa huruma zako nyingi.

Sala za Wafu

(3) *Siku ya ukumbusho.*

Ee Mungu, Bwana wa rehema : Tunawa-
ombea kwako wanawo N., N., na N. ambao
tunawakumbuka mbele zako leo ; uwajalie
mahali pa kuburudika, furaha ya amani, na
mwanga wa nuru yako.



NYIMBO ZA KANUNI



NYIMBO ZA JUMA

SIKU YA BWANA.

Sala ya Assubuhi.

1. Giza lapita na kivuli chake,
Nuru na jua tumeona tena,
Sasa tumwombe kwa sauti moja
Mungu Mwenyiezi.

Utujalie kwa fadhili zako
Tusisumbuke leo kwa shughuli,
Tupe wokofu, na karama kubwa,
Ndio amani.

Mungu Mwenyiezi utoae neema,
Baba na Mwana nawe Mfariji,
Uhimidiwe hivi killa siku,
Killa mahali. Amin.

V. Bwana ametamalaki, amejivika adhama.

R7. Bwana amejivika, amejifunga nguvu kama
mshipi.

*Ant. Ben. Ahimidiwe Utatu Mtakatifu aliye
Umoja, Muumba, Mtawala vyote : sasa, na
siku zote, na hatta milele na milele.*

Nyimbo za Juma

Sala ya Jioni.

2. Muumba nuru na mchana,
Unaotuangaza hapa,
Ulipoumba ulimwengu,
Uliumba nuru kwanza.

Usiku na mchana nao
Ulizifanya siku moja ;
Linapotukaribu giza,
Usikilize sala zetu.

Zisitunyime dhambi zetu
Karama yako ya uzima ;
Dunia kwa tamaa zake
Isitufunge kwa ubaya.

Utujalie neema yako
Tusiikose taji yetu,
Tushinde hila za Shetani,
Tukasafishwe roho zetu.

Ee Baba, hayo tuombayo
Kwa Mwana wako tujalie,
Amilikiye siku zote
Pamoja nawe, nae Roho. Amin.

∇. Sala yangu ipae, Ee Bwana.
R7. Mbele zako kama uvumba.

*Ant. Mag. Twakushukuru, Ee Mungu, twaku-
shukuru : Utatu uliye Umoja khalisi, Uungu
umoja usio mfano, Umoja uliye mmoja, Mta-
katifu.*

Nyimbo za Juma

SIKU ZA KAZI.

Sala ya Assubuhi.

3. Ee Roho Mtakatifu, uje,
Wa Baba Roho, na wa Mwana,
Utuletee neema yako,
Ikae nasi siku zote.

Kwa vinywa vyetu na mioyo
Tukuhimidi vema leo :
Upendo wako ututie,
Wengine wakawashwe nao.

Ee Baba, hayo tuombayo
Kwa Mwana wako tujalie ;
Amilikiye siku zote
Pamoja nawe, nae Roho. Amin.

∇. Utushibishe assubuhi kwa fadhili zako.
R7. Nasi tutashangilia na kufurahi.

Juma a tatu.

*Ant. Ben. Atukuzwe Bwana, Mungu wa
Israeli : kwa kuwa ametujia na kutukomboa.*

Juma a nne.

*Ant. Ben. Bwana ametuondokeshea wokofu wa
nguvu : katika nyumba ya Daudi mtumishi
wake.*

Juma a tano.

*Ant. Ben. Katika mikono yao wote wanaotu-
chukia : Bwana ametuokoa.*

Nyimbo za Juma

Alkhamisi.

*Ant. Ben. Katika utakatifu tumwabudu
Bwana : nae atatuokoa na adui zetu.*

Ijumaa.

*Ant. Ben. Kwa rehema zake Mungu wetu :
mwangaza wa juu umetujia.*

Juma a mosi.

*Ant. Ben. Ee Bwana, uwaangaze wakaao
katika giza na uvuli wa mauti : uelekeze miguu
yetu mnamo njia ya amani.*



Nyimbo za Juma

JUMA A TATU.

Sala ya Jioni.

4. Muumba anga na dunia,
Uliamuru yatengane
Maji ya anga na dunia,
Nafasi iwe kati kati.

Kwa amri yako uliumba
Maji ya inchi, yapunguze
Joto la jua, lisichome
Dunia, ikaharibika.

Kwa pendo lako tunyeshee
Umande, ndio neema yako ;
Uburudishe roho zetu,
Zisituchome dhambi zetu.

Tuone nuru ya milele
Kwa nguvu za imani yetu ;
Tushike njia ya uzima
Linapotuzunguka giza.

Ee Baba, hayo tuombayo
Kwa Mwana wako tujalie ;
Amilikiye siku zote
Pamoja nawe, nae Roho. Amin.

¶. Sala yangu ipae, Ee Bwana.
R7. Mbele zako kama uvumba.

*Ant. Mag. Moyo wangu wamwadhimisha
Bwana : kwa kuwa Mungu ameutazama unyonge
wangu.*

Nyimbo za Juma

JUMA A NNE.

Sala ya Jioni.

5. Muumba vyote, inchi kavu
Uliitenga na bahari,
Misingi ukaimarisha
Pasiwe khofu ya mawimbi.

Kwa amri yako inchi yetu
Hutoa mbegu na mazao,
Matunda yatokea mengi,
Chakula, na furaha kwetu.

Kovu za roho uzipake
Mafuta, ndio neema yako ;
Zifutwe dhambi na machozi,
Tamaa za mwili zizuiwe.

Sauti yako tuitii,
Madhara yasitupatie ;
Tujae mema na furaha,
Mauti tusiiogope.

Ee Baba, hayo tuombayo
Kwa Mwana wako tujalie ;
Amilikiye siku zote
Pamoja nawe, nae Roho. Amin.

Ÿ. Sala yangu ipae, Ee Bwana.
R7. Mbele zako kama uvumba.

*Ant. Mag. Roho yangu yamfurahia Mungu :
Mwokozi wangu.*

Nyimbo za Juma

JUMA A TANO.

Sala ya Jioni.

6. Ee Mungu, ndiwe Mtakatifu,
Mtanda mbingu kwa fakhari,
Yalipoonekana kwanza
Mapambazuko assubuhi.

Latoka jua kwa furaha
Kushangilia nguvu zake ;
Na mwezi nao waongoza,
Na nyota zisikose njia.

Mipaka inajulikana
Ya giza na ya nuru hivi ;
Twajua mwaka uanzapo,
Na mwanzo wa miezi pia.

Akili zisitiwe giza,
Takasa taka za moyoni,
Tunalemewa na makosa,
Tufunguliwe mzigo wetu.

Ee Baba, hayo tuombayo
Kwa Mwana wako tujalie ;
Amilikiye siku zote
Pamoja nawe, nae Roho. Amin.

Ÿ. Sala yangu ipae, Ee Bwana.
R7. Mbele zako kama uvumba.

*Ant. Mag. Bwana ameutazama unyonge
wangu : nae aliye hodari amenitendea makuu.*

Nyimbo za Juma

ALKHAMISI.

Sala ya Jioni.

7. Ee Mungu, mwenye nguvu zote,
Muumba anga na bahari,
Uliwaumba siku moja
Wahayi wenye namna mbili.

Samaki, ndege, wamepewa
Mahali pao, mbali mbali,
Samaki ziwe baharini,
Na ndege ziwe juu angani.

Kwa maji na kwa Roho yako
Tumebatizwa, utulinde,
Tusikuache na kupata
Adhabu, kufa kwa milele.

Tusijivune kwa kiburi,
Dhambini tusitumbukizwe ;
Tutubu sana tusikose
Taraja la wokofu wetu.

Ee Baba, hayo tuombayo
Kwa Mwana wako tujalie ;
Amilikiye siku zote
Pamoja nawe, nae Roho. Amin.

Ÿ. Sala yangu ipae, Ee Bwana.
R7. Mbele zako kama uvumba.

Ant. Mag. Mungu ametenda nguvu kwa
mkono wake : amewatawanya walio na kiburi
katika mioyo yao.

Nyimbo za Juma

IJUMAA.

Sala ya Jioni.

8. Ee Mungu, Mtawala vyote,
Uliwaumba nyama leo,
Vitambaavyo vingi sana,
Na mwanadamu, bora yeye.

Viumbe vyako ukampa
Wakili wako duniani,
Ukamtawaza mfalme wao,
Ukaamuru vimitii.

Tufukuzie mbali, Bwana,
Mawazo yote ya ubaya
Yaliyotukosesha leo
Na kuchafua nia zetu.

Utupe neema yako hapa
Tupate raha ya mbinguni ;
Kifungo cha fitina vunja,
Amani ikatutawale.

Ee Baba, hayo tuombayo
Kwa Mwana wako tujalie ;
Amilikiye siku zote
Pamoja nawe, nae Roho. Amin.

Ÿ. Sala yangu ipae, Ee Bwana.
R7. Mbele zako kama uvumba.

Ant. Mag. Bwana amewashusha wakuu katika
viti : amewakweza wanyonge.

Nyimbo za Juma

JUMA A MOSI.

Sala ya Jioni.

9. Ee Mungu, uliumba vyote,
Dunia, anga, na bahari ;
Mchana umevikwa nuru,
Usiku una usingizi.

Kwa raha unatufaraji,
Tuanze kazi zetu tena ;
Kwa raha moyo hutulia
Na kusahau hamu zake.

Na sasa kunakuchwa, Bwana,
Twakuhimidi Jina lako ;
Usiku huu utuhifadhi
Na killa namna ya ubaya.

Utuepushe na tamaa,
Tukukumbuke tulalapo,
Asikaribu yule mwovu
Na kuharibu raha yetu.

Ee Baba, hayo tuombayo
Kwa Mwana wako tujalie ;
Amilikiye siku zote
Pamoja nawe, nae Roho. Amin.

V. Sala yetu ya jioni ipae mbele zako, Ee
Bwana.

R7. Na fadhili zako zitushukie.

Ant. Mag. Twakushukuru, Ee Mungu, twaku-
shukuru : Utatu uliye Umoja khalisi, Uungu
umoja usio mfano, Umoja uliye mmoja, Mta-
katifu.



NYIMBO ZA WAKATI

MAJILIO.

Sala ya Assubuhi.

10. Sauti yasikiwa leo
Ya mjumbe, anatuambia,
Usingizini na tuamke
Kwa maana Yesu anakuja.

Mioyo yetu iwe safi,
Tuache mambo ya dunia ;
Na Kristo akituangaza
Tuondolewe killa dhara.

Aliyetazamiwa sana,
Makosa atuondolee,
Tumwombe sasa kwa machozi
Atujalie masamaha.

Yuaja tena kwa fakhari,
Na wote watatetemeka,
Asitutie khatiyani
Wokofu tuushike leo.

Majilio

Heshima, sifa, utukufu,
Kwa Mungu Baba, Mungu Mwana,
Na Mungu Roho Mtakatifu,
Zamani, leo, na milele. Amin.

Ÿ. Itengenezeni njia ya Bwana.
R7. Nyosheni mapito yake.

Ant. Ben. Tazama, Mimi namtuma mjumbe wangu : atakaeitengeneza njia yangu mbele ya uso wako. (Ant. hii itumike killa siku illa S. B.)

Sala ya Jioni.

11. Muumba nyota za mbinguni,
Uwatiae watu nuru,
Mwokozi wetu wanadamu,
Utusikie tuombapo.

Kwa pendo lako ulikuja
Kusudi uwe dawa yetu ;
Milele tusingamizwe
Kwa hila nyingi za Shetani.

Ee Mwana wa Bikira safi,
Umekubali msalabani
Kutuokoa sisi sote,
Ziondolewe dhambi zetu.

Viumbe vyako vya mbinguni
Na duniani, vyote pia,
Wasikiapo Jina lako
Kwa khofu wakusujudia.

Majilio

Mwamuzi mkuu wa siku ile,
Tunakuomba, utuvike
Silaha zako za rohoni,
Adui asitupoteze.

Heshima, sifa, utukufu,
Kwa Mungu Baba, Mungu Mwana,
Na Mungu Roho Mtakatifu,
Zamani, leo, na milele. Amin.

Ÿ. Uje, utufanye huru.
R7. Ee Bwana, Mungu wa majeshi.

Ant. Mag. Tazama, mimi mjakazi wa Bwana : na iwe kwangu kwa neno lako.

(Ant. hii itumike killa siku illa S. B. na siku zilizoamriwa Ant. kuu.)

S. B. ya I Majilio.

Sala ya Jioni ya 1.

Ant. Mag. Tazama, Jina la Bwana latoka mbali : dunia nayo imejaa utukufu wake.

Sala ya Assubuhi.

Ant. Ben. Roho Mtakatifu atakujia, Mariamu : usiogope, mimba utakayochukua ndiyo Mwana wa Mungu. Halleluya.

Sala ya Jioni ya 2.

Ant. Mag. Usiogope, Mariamu, kwa maana umepata neema kwa Mungu : tazama, utachukua mimba, utazaa mwana. Halleluya.

S. B. ya II Majilio.

Sala ya Jioni ya 1.

Ant. Mag. Njoo, Ee Bwana, utujie kwa amani : illi tufurahi mbele zako kwa moyo mkamilifu.

Sala ya Assubuhi.

Ant. Ben. Yohana aliposikia huko gerezani matendo yake Kristo, alituma wawili katika wanafunzi wake, kumwambia : Wewe ndiwe yule ajae, au tumtazamie mwingine ? Halleluya.

Sala ya Jioni ya 2.

Ant. Mag. Wewe ndiwe yule ajae, au tumtazamie mwingine ? Mwelezeni Yohana mnayo-yaona : vipofu wanapata kuona, wafu wanafufuliwa, na maskini wanakhubiriwa khabari njema. Halleluya.

S. B. ya III Majilio.

Sala ya Jioni ya 1.

Ant. Mag. Kabla yangu hakuna Mungu, wala baada yangu hakutakuwa : kwa maana killa goti litanikunjia, na killa ulimi utanikiri. (au Ant. kuu.)

Sala ya Assubuhi.

Ant. Ben. Ataketi katika kiti cha Daudi : na juu ya ufalme wake atamiliki milele. Halleluya.

Sala ya Jioni ya 2.

Ant. Mag. U kheri, Mariamu, uliyesadiki : kwa maana yatatimizwa uliyoambiwa na Bwana, Halleluya. (au Ant. kuu.)

S. B. ya IV Majilio.

Sala ya Jioni ya 1.

Ant. Mag. (Antifona kuu.)

Sala ya Assubuhi.

Ant. Ben. Salamu, Mariamu, umejaa neema, Bwana yu pamoja nawe : umebarikiwa kuliko wanawake wote. Halleluya.

Sala ya Jioni ya 2.

Ant. Mag. (Antifona kuu.)

Antifona kuu za Magnificat.

Killa moja isemwe yote mbele yake na baada yake.

Des. 16. Ee Hekima, uliyetoka kinywani mwake Aliye juu, umeenea tangu mwanzo hatta mwisho, unatengeneza yote vizuri : uje, utufundishe njia ya busara.

Des. 17. Ee Bwana, Mtawala nyumba ya Israeli, uliyemtokea Musa katika moto uliowaka kijitini, ukampa torati katika Sinai : uje, utuokoe kwa mkono ulionyoshwa.

Des. 18. Ee Shina la Yese, usimamae Ishara ya mataifa, ambae wafalme watakufumbia vinywa vyao, na mataifa watakuomba : uje utuokoe wala usikawie.

Des. 19. Ee Ufunguo wa Daudi, na Fimbo ya enzi ya nyumba ya Israeli, ufunguae wala mtu hafungi, ufunguae wala mtu hafungui : uje, utoe kifungoni waliofungwa.

Kuzaliwa

Des. 20. Ee Mapambazuko, Mwanga wa nuru ya milele, Jua la haki : uje, uwaangaze wakaa katika giza na uvuli wa mauti.

Des. 21. Ee Mfalme wa mataifa, utamaniwae nao, Jiwe la pembeni, ufanyae yote mawili moja : uje, uwaokoe wanadamu uliowaumba katika mavumbi.

Des. 22. Ee Immanueli, Mfalme wetu, Mtoa sharia, ambae mataifa wanakungoja, Mwokozi wao : uje, utuokoe, Ee Bwana Mungu wetu.

Des. 23. Ee Bikira wa mabikira, haya yatakuwaje ? Maana kabla yako hakuna mfano wako, wala baada yako hakutakuwa : Binti za Yerusalemi, kwa nini mnanistaajabia ? Mlionalo ni fumbo la Mungu.

KUZALIWA BWANA

Sala ya Jioni ya 1.

12. Mwokozi wetu wanadamu,
Isijaumbwa nuru bado,
U Mungu, Mwana wa azali,
Katika Mungu unatoka.

Wa Mungu Mwanga wa milele,
Na Tumaini letu hapa,
Usikilize sala leo
Watumwa wako waombazo.

Kuzaliwa

Muumba vyote, ukumbuke
Ulivyojitwalia utu
Tumboni mwa Bikira safi,
Ukazaliwa Mwanadamu.

Yashuhudia siku hii
Irejeapo killa mwaka,
Ya kuwa Wewe peke yako
Ulitujia utuponye.

Bahari, inchi, mbingu, nyota,
Viumbe vyote vya dunia,
Vyakuimbia uimbo mpya,
Awali ya wokofu wetu.

Na sisi, wenye kusafishwa
Kwa Damu yako ya thamani,
Siku ya Kuzaliwa kwako
Twakuimbia nyimbo zetu.

Ee Yesu, Mwana wa Bikira,
Twakutolea sifa zetu,
Pamoja nae Mungu Baba,
Na Mungu Roho Mtakatifu. Amin.

Y. Kesho uovu wa ulimwengu utaondolewa.
R7. Na Mwokozi wa ulimwengu atatutawala.

Ant. Mag. Jua litakapopanda mbinguni
mtamwona Mfalme wa wafalme, akitoka kwa
Baba : kama Bwana arusi akitoka chumbani
mwake.

Kuzaliwa

Sala ya Assubuhi.

13. Enyi miisho ya dunia,
Sikilizeni nyimbo zetu!
Twamsifu Mfalme wa wafalme,
Mwokozi, Mwana wa Bikira.

Muumba ana utu wetu,
Mtoa amri anatii;
Katika mwili akombo
Miili ya viumbe vyake.

Ee fumbo la ajabu kuu,
Tusiloweza kufahamu!
Pasipo mume Mariamu
Bikira achukua mimba.

Na mwili wa Bikira safi
Ni kao lake Mungu kweli;
Kwa muda ule alimzaa
Aliotaja Gabrieli.

Muumba vyote azaliwa,
Horini amelazwa Mungu;
Wahayi wote huwalisha,
Mamae amnyonyesha Yeye.

Mbinguni Malaika wengi
Waimba sana, jeshi kuu;
Na makondeni wachungaji
Wafunuliwa Mchungu wao.

Ee Yesu, Mwana wa Bikira,
Twakutolea sifa zetu,
Pamoja nae Mungu Baba,
Na Mungu Roho Mtakatifu. Amin.

Stefano

☩. Bwana ameujulisha. Halleluya.
R7. Wokofu wake. Halleluya.

Ant. Ben. Utukufu una Mungu juu : katika inchi amani kwa watu aliowaridhia. Halleluya.

Sala ya Jioni ya 2.

UIMBO 12.

☩. Bwana ameujulisha. Halleluya.
R7. Wokofu wake. Halleluya.

Ant. Mag. Leo Kristo amezaliwa, leo Mwokozi ameonekana, leo Malaika waimba duniani na Malaika wakuu wafurahi : leo wenye haki washangilia wakisema, Utukufu una Mungu juu. Halleluya.

Stefano, Shahidi wa kwanza.

14. Wa Mashahidi Bwana mkuu,
U taji na thawabu juu,
Shahidi wako tukimsifu,
Tupewe na utakatifu.

Matata kwake si kikwazo,
Anasa hakunaswa nazo,
Alizona kuwa taka,
Kashiba sasa mibaraka.

Mateso huyu yalimfaa,
Kazi si kazi kwa shujaa,
Alikufia kwa furaha,
Ee Yesu, ukampa raha.

Tukimtukuza asikari
Wa vita zako, Jemadari,
Fadhili zako tupokee,
Makosa utuondolee.

Ee Yesu, Mwana wa Bikira,
Twakutolea sifa zetu,
Pamoja nae Mungu Baba,
Na Mungu Roho Mtakatifu. Amin.

✓. Stefano alizona mbingu zimefunuka.

R7. Aliona akaingia ; yu kheri aliyefunuliwa
mbingu.

Ant. Watu watawa wakamzika Stefano :
wakamfanyia maombolezo mengi.

Yohana, Mtume, Mtunga Injili.

15. Dunia ifurahi sana,
Waitikie Malaika,
Pamoja nao wanadamu,
Waimbe sifa za Mitume.

Wa ulimwengu waamuzi,
Na nuru kweli ya dunia,
Saidieni tukiomba
Aturehemu Bwana Kristo.

Funguo mmepewa ninyi
Za mbingu, mtufungulie ;
Twamwomba Mungu neema yake,
Tufunguliwe dhambi zetu.

Maneno yenu yaliponya
Wagonjwa wengi wa zamani ;
Wagonjwa sisi wa mioyo,
Turudishiwe afya zetu.

Na Kristo atakaporudi
Kuuhukumu ulimwengu,
Tushirikishwe sisi nanyi
Furaha zenu za milele.

Ee Yesu, Mwana wa Bikira,
Twakutolea sifa zetu,
Pamoja nae Mungu Baba,
Na Mungu Roho Mtakatifu. Amin.

✓. Yohana mbarikiwa aliheshimiwa sana.

R7. Aliyeegamia kifuani pa Bwana wakati wa
chakula.


Ant. Neno hili lilienea katika ndugu kwamba
mwanafunzi yule hafi : walakini Yesu, haku-
mwambia, Hafi ; bali, Nikitaka akae hatta
nijapo, imekukhusu nini ?

Wasio Khatiya.

16. Wa Mungu mawaridi ninyi
Mliochumwa na Herode,
Alipotaka kumharibu
Mwokozi wetu, Bin Mariamu.

Twawasalimu, Mashahidi !
Karibu na madhbahu juu
Mnachezea taji zenu,
Awatazama kwa upendo.

Kuzaliwa

Ee Yesu, Mwana wa Bikira,
Twakutolea sifa zetu. 
Pamoja nae Mungu Baba,
Na Mungu Roho Mtakatifu. Amin.

℣. Herode akaghadhabika, akaua watoto wengi.

℞. Katika Bethlehemu ya Yahudi, mji wa Daudi.

Ant. Watoto wachanga wasio khatiya waliuawa kwa ajili ya Kristo, hatta wanyonyao waliuawa na mfalme mkali : wasio khatiya wamfuata Mwana Kondoo mwenyewe, wakisema daima, Atukuzwe Bwana.

Siku za Oktavo.

(zisizo Antifona zake)

NYIMBO za *Siku Kuu*. ℣. na ℞. Bwana. etc.

Ant. Ben. Utukufu. . . . *Ant.* Mag. Leo Kristo. . . .

S. B. baada ya Kuzaliwa.

NYIMBO za *Siku Kuu*.

℣. Neno alifanyika mwili. Halleluya.
℞. Akakaa kwetu. Halleluya.

Ant. Mtoto Yesu akazidi kuendelea katika hekima na kimo : na neema kwa Mungu na kwa watu. Halleluya.

(*Siku ya Bwana ikija Des. 30 au 31, ℣. na ℞. na Ant. hizi zitumike Sala ya Jioni ya I pia.*)

Ufunuo

Kutahiriwa kwa Bwana.

NYIMBO za *Siku Kuu ya Kuzaliwa*.

℣. Neno alifanyika mwili. Halleluya.
℞. Akakaa kwetu. Halleluya.

Ant. Mungu kwa wingi wa upendo wake aliotupenda : alimtuma Mwana wake mwenyewe katika mfano wa mwili ulio wa dhambi. Halleluya.

(*Ikiwa Jan. 2, 3, au 4 ni Siku ya Bwana, sala yake ndio ya Jina Takatifu, Yesu. UIMBO 61.*)

Mkeshwa wa Ufunuo.

Sala ya Jioni ya 1.

Kama S. B. baada ya Kuzaliwa.

Sala ya Assubuhi.

Kama Kutahiriwa kwa Bwana.

UFUNUO WA BWANA

Sala ya Jioni ya 1.

17. Mfalme mkali, Ee Herode,
Ya nini kumwogopa Yesu ?
Ufalme wako hautaki,
Aliye Mfalme wa mbinguni.

Waona nyota Mamajusi,
Ingozako wafuata,
Kwa nuru wamtafuta Nuru,
Wamkiri Mungu kwa sadaka.

Na Mungu Mwana abatizwa
Katika maji ya Yordani,
Asiyetenda dhambi kamwe
Aziondoa dhambi zetu.

Muumba vyote kwa ajabu
Aweza kubadili maji ;
Tekeni maji, aamuru,
Na kumbe ! maji ni divai.

Kwa Ufunuo wako, Bwana,
Twakuhimidi sana leo,
Pamoja nae Mungu Baba,
Na Mungu Roho Mtakatifu. Amin.

Ψ. Wafalme wa Tarashishi na visiwa na
walete kodi.

R7. Wafalme wa Sheba na Seba na watoe
vipawa.

Ant. Mag. Mamajusi walipoiona nyota waka-
semezana, Hii ni ishara ya Mfalme mkuu :
twende tukamtafute tukampe tunu, dhahabu na
uvumba na manemane. Halleluya.

Sala ya Assubuhi.

18. Katika miji yenye sifa
Hakuna mkuu kuliko wewe ;
Hu mdogo kamwe, Bethlehemu,
Alimotoka Bwana Yesu.

Na nyota yenye utukufu,
Iliyong'aa kuliko jua,
Ilitangaza kuwa Mungu
Amejichukulia utu.

Walipoona Mamajusi
Wamsujudie walikuja ;
Dhahabu bora na uvumba
Na manemane wakaleta.

Dhahabu yaonyesha Mfalme,
Uvumba wamtolea Mungu,
Na manemane yatabiri
Mateso yake na kaburi.

Kwa Ufunuo wako, Bwana,
Twakuhimidi sana leo,
Pamoja nae Mungu Baba,
Na Mungu Roho Mtakatifu. Amin.

Ψ. na R7. na *Ant.* kama Sala ya Jioni ya 1.

Sala ya Jioni ya 2.

UIMBO 17. Ψ. na R7. Wafalme, etc.

Ant. Mag. Twafanya Siku Kuu yenye kupa-
mbwa miujiza mitatu : leo nyota iliwaongoza
Mamajusi zizini, leo maji yaligeuka kuwa
divai arusini, leo Kristo alikubali kubatizwa na
Yohana Yordani, illi atuokoe. Halleluya.

Siku za Oktavo.

NYIMBO za Siku Kuu. Ψ. na R7. Wafalme, etc.

Sala ya Assubuhi.

Ant. Ben. Tuliona nyota yake mashariki :
nasi tumekuja na tunu kumsujudu Bwana.
Halleluya.

Ufunuo

Sala ya Jioni.

Ant. Mag. Wote kutoka Sheba watakuja : wataleta dhahabu na uvumba. Halleluya.

S. B. ya I Ufunuo.

NYIMBO za Siku Kuu. *Ŷ. na R7. Wafalme. etc.*

Sala ya Jioni ya 1.

Ant. Mag. Mtoto Yesu akabaki nyuma Yeruselemi, wala wazee wake hawakujua, wakadhani yumo katika msafara wao : wakamtafuta katika jamaa zao na wenzao.

Sala ya Assubuhi.

Ant. Ben. kama Ant. Mag. juu.

Sala ya Jioni ya 2.

Ant. Mag. Mwanangu, kwani ukatutenda hivi? Tazama, baba yako na mimi tulikuwa tukikutafuta kwa huzuni : Kwani kunitafuta? Hamkujua ya kuwa imenipasa kuwa katika nyumba ya Baba yangu?

S. 8. Ufunuo.

Yote kama Siku Kuu yenyewe.

¶ *Baada ya S. 8. Ufunuo hatta Kwaresima NYIMBO ZA JUMA zitumike, isipokuwa ni Siku Kuu.*



KWARESIMA

Sala ya Assubuhi.

19. Ee Yesu, Jua la wokofu,
Mioyo yetu uangaze ;
Mchana tunaona tena,
Tuondolewe giza letu.

Wakati wa kukubalika
Umetujia kwa rehema :
Utupe mito ya machozi,
Mioyo utujaze pendo.

Tuzililie dhambi zetu,
Tuoshwe, tusafishwe pia ;
Utupe toba, ulegeze
Ugumu wa mioyo yetu.

Kwa maana siku inakuja
Na vyote utatengeneza ;
Hatta njiani tufurahi
Kwa kuwa unatuongoza.

Ee Mungu, Baba, Mwana, Roho,
Usiyegawanyika kamwe,
Utupe kwa mfungo huu
Faida ya kutubu kwetu. Amin.

Ŷ. Mungu atakuagizia Malaika zake.
R7. Wakulinde katika njia zako zote.

Ant. Ben. Mfungapo, msiwe kama wanafiki : wenyewe uso wa kukunjamana.

(Ant. hii itumike killa siku illa S. B.)

Kwaresima

Sala ya Jioni.

20. Muumba mwema, sikiliza,
Tukuombapo kwa machozi ;
Twalia sana siku nyingi
Za Kwaresima, juma sita.

Mioyo yetu waijua,
Hatuna nguvu, tu dhaifu ;
Kwa toba tunakurudia,
Tuondolewe dhambi zetu.

Makosa mengi twaungama,
Rehema nyingi tuonyeshe ;
Wagonjwa, tulettee dawa,
Lihimidiwe Jina lako.

Na kwa kufunga kwetu, Bwana,
Utupe moyo wa kiasi ;
Tujikataze killa dhambi
Kwa nguvu mpya za rohoni.

Ee Mungu, Baba, Mwana, Roho,
Usiyegawanyika kamwe,
Utupe kwa mfunjo huu
Faida ya kutubu kwetu. Amin.

✓. Mungu atakuagizia Malaika zake.
R/. Wakulinde katika njia zako zote.

Ant. Mag. Jiwekeeni hazina mbinguni :
zisikoharibu nondo wala kutu.

(Ant. hii itumike killa siku illa S. B.)

Kwaresima

S. B. ya I Kwaresima.

Sala ya Jioni ya 1.

Ant. Mag. Ndipo utaita nae Bwana ataitika :
utalia nae atasema, Mimi hapa.

Sala ya Assubuhi.

Ant. Ben. Ndipo Yesu alipopandishwa na
Roho hatta jangwani, illi ajaribiwe na Shetani :
Akafunga siku arubaini mchana na usiku,
baadae akaona njaa.

Sala ya Jioni ya 2.

Ant. Mag. Tazama, sasa ndio wakati ulio-
kubalika sana ; tazama, sasa ndio siku ya
wokofu : bassi, siku hizi tujipatie sifa njema,
kama wakhudumu wa Mungu, katika saburi
nyingi, katika kufunga, katika kukesha, na
katika upendo usio unafiki.

S. B. ya II Kwaresima.

Sala ya Jioni ya 1.

Ant. Mag. Msimwambie mtu khabari ya
mambo hayo : hatta Mwana wa Adamu ataka-
pofufuka katika wafu.

Sala ya Assubuhi.

Ant. Ben. Yesu aliwachukua wanafunzi wake,
akapanda juu ya mlima : akageuka sura yake
mbele yao.

Sala ya Jioni ya 2.

Ant. Mag. kama Sala ya Jioni ya 1. juu.

S. B. ya III Kwaresima.

Sala ya Jioni ya 1.

Ant. Mag. Baba yake aliwaambia watu-mishi wake, Ileteni joho iliyo bora, mkamvike : mpeni pete kwa kidole chake na viatu kwa miguu yake.

Sala ya Assubuhi.

Ant. Ben. Aliye na nguvu, mwenye silaha zake, alindapo ua wake : mali zake zimo katika amani.

Sala ya Jioni ya 2.

Ant. Mag. Mwanamke mmoja katika makutano akapaaza sauti yake akamwambia, Li kheri tumbo lililokuchukua, na maziwa uliyonyonya : Lakini Yesu akasema, Bali afadhali wa kheri wenye kulisikia neno la Mungu na kulishika.

S. B. ya IV Kwaresima.

Sala ya Jioni ya 1.

Ant. Mag. Mwanamke, hapana aliyekuhukumu? Hapana, Bwana : Nami sikuhukumu ; enenda, wala usitende dhambi tena.

Sala ya Assubuhi.

Ant. Ben. Yesu alipoinua macho yake akaona makutano mengi yanakuja kwake, akamwambia Filipo, Tununue wapi mikate, hawa wapate kula : Alinena haya illi amjaribu ; kwa maana alijua mwenyewe atakalotenda.

Sala ya Jioni ya 2.

Ant. Mag. Yesu alipanda mlimani : akaketi huko pamoja na wanafunzi wake.

WAKATI WA MATESO

Sala ya Assubuhi.

21. Na miaka thelathini
Huku kwetu alikaa,
Na wakati ukitimu,
Yu tayari kujitoa,
Auawe msalabani,
Madhabuha kamilifu.

Alistahimili siki,
Misumari na miiba,
Na mkuki ukampenya,
Damu, maji, yakimtoka ;
Mbingu, inchi, visafishwe,
Nao ulimwengu wote.

Msalaba wa wokofu !
Ndiwe mti wa pekee,
Hamna jani wala ua
Wala tunda kama lako ;
Mti mzuri ! Misumari !
Mzigo mzuri mwachukua !

Mti mrefu uiname,
Na ugumu wako acha,
Uchukue kwa upole
Mwili wa Mfalme wako ;
Wamchukua Mkombozi
Wetu na wa ulimwengu.

Umepewa peke yako
Mkombozi kumchukua,
Illi wenye kupotea
Warudishwe bandarini,
Wakinyunyiziwa damu
Ya dhabihu ya milele.

Utukufu na fakhari
Ina Mungu juu ya yote,
Baba, Mwana, nae Roho,
Nafsi tatu, Mungu mmoja ;
Atukuzwe, asifiwe,
Leo, kesho, na milele. Amin.

∇. Uniponye na adui zangu, Ee Mungu wangu.

R/. Uniinue juu yao wanaoshindana nami.

Ant. Ben. Kondoo zangu waisikia sauti yangu : nami, niliye Bwana, nawajua.

(Ant. hii itumike siku za kazi.)

Sala ya Jioni.

22. Bendera za Mkuu zatangulia,
Wang'aa kwa ajabu Msalaba ;
Aliyejitwalia mwili ndipo
Alipolipa dia tuokoke.

Na huko akachomwa kwa mkuki,
Uliochuruzisha damu yake ;
Na maji nayo yakamtoka pia,
Wa kutuocha sisi mto huu.

Maneno yake Daudi yatimizwa,
Aliyomtabiria Bwana Yesu ;
Katika mataifa Mungu Mfalme,
Na Msalabani Mungu amiliki.

Ee mti mzuri sana na wa nuru,
Uliovikwa hivi kifaume !
Uliochaguliwa kwa heshima,
Uuchukue mwili wake Yesu.

Na Msalabani akatutolea
Maisha yake ya thamani kubwa ;
Awakomboe wanadamu wote,
Adui wetu akatushindie.

Ee Msalaba, tumaini letu,
Wakati wa Mateso ujaliwe
Kuzidishia neema watu wema,
Waondolewe dhambi wakoaji.

Utatu wa milele, Mungu mmoja,
Uliyetuokoa usifiwe ;
Kwa Msalaba huo wa ajabu
Utuhifadhi sasa na milele. Amin.

∇. Uniokoe, Ee Bwana, na mtu mbaya.
R/. Unihifadhi na mtu wa jeuri.

*Ant. Mag. Kazi njema nyingi nimewaonye-
sha : kwa ajili ya kazi ipi mnataka kunifisha ?*

(Ant. hii itumike siku za kazi.)

Mateso

S. B. ya Mateso.

Sala ya Jioni ya 1.

Ant. Mag. Mimi ndimi ninaejishuhudia nafsi yangu : nae Baba aliyenipeleka ananishuhudia.

Sala ya Assubuhi.

Ant. Ben. Yesu aliwaambia Wayahudi na makuhani wakuu : Aliye wa Mungu huyasikia maneno ya Mungu ; kwa hiyo ninyi hamsikii, kwa sababu ninyi si wa Mungu.

Sala ya Jioni ya 2.

Ant. Mag. Ibrahimu, baba yenu, alishangilia apate kuiona siku yangu : akaona, akafurahi.

S. B. ya Mitende.

Sala ya Jioni ya 1.

Ant. Mag. Baba mwenye haki, ulimwengu haukukujua : lakini mimi nalikujua, ya kuwa ndiwe uliyenituma.

Sala ya Assubuhi.

Ant. Ben. Watu wengi walioijia siku kuu walimpigia Bwana makelele : Ndiye mbarikiwa ajae kwa Jina la Bwana ; Hosana, uliye juu.

Sala ya Jioni ya 2.

Ant. Mag. Imeandikwa, Nitampiga mchungu, na kondoo wa kundi watatawanyika : Lakini baada ya kufufuka kwangu, nitatangulia mbele yenu kwenda Galilaya ; huko mtaniona, asema Bwana.

JUMA TAKATIFU

Juma a tatu.

Sala ya Assubuhi.

Ant. Ben. Unitukuze, Baba, pamoja nawe : kwa utukufu ule niliokuwa nao kabla ya kuwako ulimwengu.

Sala ya Jioni.

Ant. Mag. Usingekuwa na mamlaka yo yote juu yangu : kama usingepewa toka juu.

Juma a nne.

Sala ya Assubuhi.

Ant. Ben. Hatta kabla ya siku kuu ya Pasaka, Yesu akijua ya kuwa saa yake imefika : akiwa aliwapenda watu wake, aliwapenda ukomo wa upendo.

Sala ya Jioni.

Ant. Mag. Nina uweza wa kuuweka uzima wangu : tena nina uweza wa kuutwaa tena.

Juma a tano.

Sala ya Assubuhi.

Ant. Ben. Simon, umelala? : hukuweza kukesha nami saa moja ?

Sala ya Jioni.

Ant. Mag. Kijakazi kimoja alimwambia Petro, Hakika na wewe u mmoja wao : maana hatta usemi wako wakutambulisha.

¶ Baada ya Juma a tano UIMBO na V. na R7. hapana, hatta S. B. ya I Pasaka.

Juma Takatifu

Alkhamisi ya Amri.

Sala ya Assubuhi.

Ant. Ben. Na yeye anaemsaliti amewapa ishara, akinena : nitakaembusu ndiye ; mkamateni.

Sala ya Jioni.

Ant. Mag. Walipokuwa wakila, Yesu akatwaa mkate, akaubariki : akaumega, akawapa wanafunzi wake.

Ijumaa Kuu.

Sala ya Assubuhi.

Ant. Ben. Wakauweka juu ya kichwa chake mshitaka wake, ulioandikwa : Yesu Mnazareti, Mfalme wa Wayahudi.

Sala ya Jioni.

Ant. Mag. Yesu alipoipokea siki, akasema, Imekwisha : akainama kichwa, akatoa roho.

Mkesha wa Pasaka.

Sala ya Assubuhi.

Ant. Ben. Wanawake wakikaa kwenye kaburi walikuwa wakilia : wakamwomboleza Bwana.

Sala ya Jioni (*ndio ya kwanza ya Pasaka.*)

Ant. Mag. Sabato ilipokwisha, ikipambazuka siku ya kwanza ya juma : akaenda Mariamu Magdalene, na Mariamu yule wa pili, kulitazama kaburi. Halleluya.

PASAKA

Badala ya UIMBO.

23. Siku hii ndiyo aliyoifanya Bwana : Tutashangilia na kuifurahia.

Ŷ. na R7. hapana.

Sala ya Assubuhi.

Ant. Ben. Hatta assubuhi mapema, siku ya kwanza ya sabato : wakaenda kaburini, jua lilipochomoza. Halleluya.

Sala ya Jioni.

Ant. Mag. Hatta walipotazama, wakaona ya kuwa lile jiwe limekwisha kufingirishwa : nalo lilikuwa kubwa mno. Halleluya.

Antifona hizi zitumike killa siku ya Oktavo.

WAKATI WA PASAKA

Sala ya Assubuhi.

24. Tazama, kumepambazuka !
Mbinguni wanashangilia,
Na inchi imejaa furaha,
Jehanum inatetemeka.

Mfalme huyu mwenye nguvu,
Na wafu amewaokoa,
Shimoni wametoka nae,
Waone nuru ya uzima.

Kaburi lake wakalinda,
Askari wapo na muhuri,
Lakini ameshinda kufa,
Mauti haimwezi Yeye.

Maombolezo yamekwisha,
Machози tena hayafai,
Tuimbe kwa sauti kuu,
Mshinda kufa kafufuka.

Daima, Yesu, uwe Wewe
Furaha yetu ya Pasaka ;
Uzima upya umetupa,
Utuokoe na Jehanum.

Ahimidiwe Mungu Baba,
Na Mwana mwenye kufufuka,
Na Roho Mfariji nae,
Zamani, leo, na milele. Amin.

∇. Kufufuka kwako Ee Kristo. Halleluya.
R7. Mbingu na inchi zikufurahie. Halleluya.

Ant. Ben. Enendeni, kawafanyeni mataifa
yote kuwa wanafunzi : mkiwabatiza kwa Jina
la Baba na Mwana na Roho Mtakatifu. Halle-
luya.

(*Ant. hii itumike killa siku illa S. B.*)

Sala ya Jioni.

25. Karamu hii ya Mfalme mkuu,
Mavazi safi na tuvae ;
Bahari tumekwisha vuka,
Tumsifu Kristo Bwana wetu.

Ajabu ya upendo wake !
Ametunyweshwa. Damu yake,
Na Mwili wenye kuhuisha
Kuhani wetu autoa.

Kutia damu milangoni
Kumemzuia mharabu ;
Bahari imekwisha tengwa,
Adui nao wametoswa.

Pasaka yetu ndiye Kristo,
Dhabihu nae ya Pasaka,
Isiyotiwa chachu, safi,
Wapewa wenye moyo safi.

Dhabihu kweli ya mbinguni,
Mshinda nguvu za kuzimu,
Mvunja fungo la mauti,
Uzima ametupatia.

Aliyeshinda ndiye Kristo,
Mateka yake aonyesha ;
Na mbingu zimefunguliwa,
Mkuu wa giza amefungwa.

Daima, Yesu, uwe Wewe
Furaha yetu ya Pasaka ;
Uzima upya umetupa,
Utuokoe na Jehanum.

Ahimidiwe Mungu Baba,
Na Mwana mwenye kufufuka,
Na Roho Mfariji nae,
Zamani, leo, na milele. Amin.

Pasaka

¶. Kaa pamoja nasi. Halleluya.

R7. Kwa maana kumekuchwa. Halleluya.

Ant. Mag. Amani kwenu, ni Mimi, Halleluya : msiogope. Halleluya.

(Ant. hii itumike killa siku illa S. B.)

S. B. ya I Pasaka.

Sala ya Jioni ya 1.

Ant. Mag. Ikawa jioni katika siku ile ya kwanza ya sabato, na milango imefungwa walipokuwapo wanafunzi : Yesu akasimama katikati, akawaambia, Amani kwenu. Halleluya.

Sala ya Assubuhi.

Ant. Ben. kama Ant. Mag. juu.

Sala ya Jioni ya 2.

Ant. Mag. Baada ya siku nane, milango imefungwa, Bwana aliingia, akasema : Amani kwenu. Halleluya. Halleluya.

S. B. ya II Pasaka.

Sala ya Jioni ya 1.

Ant. Mag. Ndimi niliye mchungwa wa kondoo, ndimi niliye njia, na kweli, na uzima : ndimi niliye mchungwa aliye mwema, na walio wangu nawajua, na walio wangu wananjua. Halleluya.

Sala ya Assubuhi.

Ant. Ben. kama Ant. Mag. juu.

Pasaka

Sala ya Jioni ya 2.

Ant. Mag. Mimi ndimi niliye mchungwa aliye mwema, ninalisha kondoo zangu : na uzima wangu nauweka kwa ajili ya kondoo. Halleluya.

S. B. ya III Pasaka.

Sala ya Jioni ya 1.

Ant. Mag. Bado kitambo, nanyi hamnioni tena, asema Bwana : na bado tena kitambo, na mtaniona ; kwa sababu nakwenda zangu kwa Baba. Halleluya.

Sala ya Assubuhi.

Ant. Ben. kama Ant. Mag. juu.

Sala ya Jioni ya 2.

Ant. Mag. Amin, amin, narwaambieni, Ninyi mtalia na kuomboleza, bali ulimwengu utafurahi : ninyi mtahuzunishwa, lakini huzuni yenu itageuka kuwa furaha. Halleluya.

S. B. ya IV Pasaka.

Sala ya Jioni ya 1.

Ant. Mag. Nakwenda zangu kwake aliyeni-peleka : wala hakuna mmoja wenu aniulizae, Unakwenda zako wapi ? Halleluya.

Sala ya Assubuhi.

Ant. Ben. kama Ant. Mag. juu.

Sala ya Jioni ya 2.

Ant. Mag. Nakwenda zangu kwake aliyeni-peleka : illa kwa sababu nimewaambieni haya, huzuni imejaa mioyoni mwenu. Halleluya.

S. B. ya V Pasaka.

Sala ya Jioni ya 1.

Ant. Mag. Mpaka leo hamkuomba neno kwa Jina langu : ombeni na mtapata. Halleluya.

Sala ya Assubuhi.

Ant. Ben. kama Ant. Mag. juu.

Sala ya Jioni ya 2.

Ant. Mag. Ombeni na mtapata, furaha yenu iwe timilifu : kwa maana Baba mwenyewe awapenda ninyi, kwa kuwa ninyi mmenipenda Mimi, mkaamini. Halleluya.

KUPAA KWA BWANA

Sala ya Jioni ya 1.

- 26.** Mwokozi wetu wanadamu,
Furaha ya mioyo yetu,
Muumba ulimwengu wote,
Na nuru ya Watakatifu.

Kwa pendo lako la ajabu
Umechukua dhambi zetu,
Ingawa Wewe huna dhambi,
Ukafa sisi tuwe hayi.

Kuzimu ukashambulia,
Mateka yake upokonye ;
Na Baba amekuketisha
Mkono wake wa kuume.

Uponye kwa huruma zako
Jeraha za mioyo yetu ;
Tukaribie kiti chako,
Tupate na kibali kwako.

Rubani Wewe, Wewe njia,
Kufika kwako nia yetu ;
Furaha yetu uwe hapa,
Thawabu yetu ya milele.

Uliyeshinda, ukapaa,
Ee Yesu, twakusifu sana,
Pamoja nae Mungu Baba,
Na Mungu Roho Mtakatifu. Amin.

Y. Mungu amepaa kwa kelele za shangwe.
Halleluya.

R7. Bwana kwa sauti ya baragumu. Halleluya.

Ant. Mag. Jina lako nimewadhihirishia
watu wale ulionipa, na sasa nawaombea hawo :
siuombei ulimwengu, kwa kuwa naja kwako.
Halleluya.

Sala ya Assubuhi.

UIMBO 26.

Y. Bwana ameweka. Halleluya.

R7. Kiti chake cha enzi mbinguni. Halleluya.

Ant. Ben. Ninapaa kwa Baba yangu na
Baba yenu : kwa Mungu wangu na Mungu wenu.
Halleluya.

Kupaa

Sala ya Jioni ya 2.

UIMBO 26.

∇. Bwana ameweka. Halleluya.

R7. Kiti chake cha enzi mbinguni. Halleluya.

Ant. Mag. Ee Mfalme wa utukufu, Bwana wa majeshi, uliyepaa leo kwa shangwe juu kuliko mbingu : usituache yatima ; bali utuletee Ahadi ya Baba, Roho ya kweli. Halleluya.

Siku za Oktavo.

UIMBO wa Siku Kuu. ∇. na R7. Bwana, etc.

Ant. Ben. Ninapaa. . . . Ant. Mag. Ee Mfalme. . . .

S. B. ya Kupaa.

UIMBO wa Siku Kuu. ∇. na R7. Bwana, etc.

Sala ya Jioni ya 1.

Ant. Mag. Ajapo Mfariji, nitakaewapelekea toka kwa Baba, Roho ya kweli atokae kwa Baba : Yeye atanishuhudia. Halleluya.

Sala ya Assubuhi.

Ant. Ben. kama Ant. Mag. juu.

Sala ya Jioni ya 2.

Ant. Mag. Nimewaambieni haya, illi kusudi saa ile itakapokuja : myakumbuke ya kuwa Mimi naliwaambieni. Halleluya.

S. 8. Kupaa.

Yote kama Siku Kuu yenyewe.

Ijumaa na Juma a mosi.

Kama S. B. ya Kupaa.

PENTEKOTE

Sala ya Jioni ya 1.

27. Muumba Roho, utujie,
Ukae mioyoni mwetu,
Umeziumba roho zetu,
Zijaze neema ya mbinguni.

Waitwa naswi Mfariji,
Karama yake Mtukufu,
Chemchemi ya uhayi, Moto,
Mafuta ya rohoni, Pendo.

Karama saba utoae,
Kidole chake Mungu Baba,
Ahadi yake Baba, Wewe,
Wa kunenesha ndimi zetu.

Ututangaze nia zetu,
Mioyo ututie pendo,
Miili yetu i dhaifu,
Ijaze nguvu ya milele.

Adui wetu mfukuze,
Amani tupe killa siku,
Kwa kuwa Kiongozi Wewe,
Tutaepuka killa dhara.

Utupe Baba kumtambua,
Na Mwana nae, ndani yako,
Tukuamini Wewe nawe,
Wa Baba Roho, na wa Mwana.

Ahimidiwe Mungu Baba,
Na Mwana mwenye kufufuka,
Na Roho Mfariji nae,
Zamani, leo, na milele. Amin.

Ÿ. Wote wakajazwa Roho Mtakatifu. Halleluya.

R7. Wakaanza kusema. Halleluya.

Ant. Mag. Sitawaacha ninyi yatima, Halleluya; nakwenda zangu, tena naja kwenu, Halleluya: na moyo wenu utafurahi. Halleluya.

Sala ya Assubuhi.

28. Tushangilie sana leo,
Tumeiona tena siku
Alipokuja Mfariji,
Mitume akiwashukia.

Tazama, ndimi kama moto
Zawashukia killa mmoja,
Wapewe ndimi wakhubiri,
Wawashwe moto wa upendo.

Kwa lugha nyingi mbalimbali
Wasema; watu washituka,
Hudhani kama wamelewa,
Na kumbe! wamejazwa Roho.

Zatimu siku za Pasaka
Kwa mambo hayo ya ajabu,
Mithili ya kuweka huru
Watumwa siku ya Yubile.

Ee Mungu Mtakatifu, leo
Utusikie tuombapo,
Utupe neema ya mbinguni,
Karama zake Roho yako.

Utusafishe roho zetu,
Utuingie na kukaa,
Utusamehe dhambi zote,
Amani yako tujalie.

Ahimidiwe Mungu Baba,
Na Mwana mwenye kufufuka,
Na Roho Mfariji nae,
Zamani, leo, na milele. Amin.

Ÿ. Wote wakajazwa Roho Mtakatifu. Halleluya.

R7. Wakaanza kusema. Halleluya.

Ant. Ben. Pokeeni Roho Mtakatifu: wo wote mtakaowaondolea dhambi, wameondolewa. Halleluya.

Sala ya Jioni ya 2.

UIMBO 27.

Ÿ. Mitume wakasema kwa lugha mbalimbali. Halleluya.

R7. Matendo makuu ya Mungu. Halleluya.

Ant. Mag. Leo siku ya Pentekote imewadia, Halleluya; leo Roho Mtakatifu alionekana juu ya wanafunzi katika moto, akawapa karama za Roho: akawapeleka kwenda ulimwenguni mwote kukhubiri na kushuhudu; aaminiye na kubatizwa ataokoka. Halleluya.

Utatu Mt.

Siku za Oktavo.

Sala ya Assubuhi.

UIMBO 28. *Ŵ. na R7.* Wote wakajazwa, *etc.*

Ant. Ben. Pendo la Mungu limekwisha kumiminiwa katika mioyo yetu : na Roho Mtakatifu tuliyepeva sisi. Halleluya.

Sala ya Jioni.

UIMBO 27. *Ŵ. na R7.* Mitume wakasema. *etc.*

Ant. Mag. Roho atokae kwa Baba, Halleluya : Yeye atanitukuza Mimi. Halleluya. Halleluya.

UTATU MTUKUFU

Sala ya Jioni ya 1.

29. Utatu, Nuru ya milele,
Umoja, Mungu Mwenyezi,
Likichwa jua sasa kwetu,
Utuangaze nia zetu.

Twakuhimidi assubuhi,
Jioni tena twakusih,
Wanyonge sisi, tujalie
Mbinguni tukufurahie.

Ahimidiwe Mungu Baba,
Na Mwana wake wa pekee,
Na Roho Mfariji nae,
Zamani, leo, na milele. Amin.

Ŵ. Tumhimidi Baba na Mwana na Roho Mtakatifu.

R7. Tumsifu na kumwadhimisha milele.

Utatu Mt.

Ant. Mag. Twakushukuru, Ee Mungu, twakushukuru : Utatu uliye Umoja khalisi, Uungu umoja usio mfano, Umoja uliye mmoja, Mtakatifu.

Sala ya Assubuhi.

30. Utatu Mtakatifu mkuu,
Twakuhimidi, Mungu mmoja,
Unatawala ulimwengu,
Utusikie tuimbapo.

Mapambazuko assubuhi
Yatujulisha jua lipo,
Panapo giza la usiku
Tuangazie nuru yako.

Ahimidiwe Mungu Baba,
Na Mwana wake wa pekee,
Na Roho Mfariji nae,
Zamani, leo, na milele. Amin.

Ŵ. Tumhimidi Baba na Mwana na Roho Mtakatifu.

R7. Tumsifu na kumwadhimisha milele.

Ant. Ben. Ahimidiwe Utatu Mtakatifu aliye Umoja, Muumba, Mtawala vyote : sasa, na siku zote, na hatta milele na milele.

Sala ya Jioni ya 2.

UIMBO 29.

Ŵ. Umehimidiwa, Bwana, katika nafasi ya mbingu.

R7. Wastahili kusifiwa na kutukuzwa milele.

Mwili Mt.

Ant. Mag. Wewe, Ee Mungu Baba, usiyezaliwa, Wewe, Ee Mwana wa azali ; Wewe, Ee Roho Mtakatifu, Mfariji ; Utatu Mtakatifu uliye Umoja : kwa moyo wetu wote na kwa vinywa vyetu twakukiri na kukusifu na kukuhimidi ; utukufu una Wewe hatta milele.

¶ *Baada ya Siku Kuu ya Utatu Mt. hatta Majilio NYIMBO ZA JUMA zitumike, isipokurwa ni Siku Kuu.*

MWILI MTUKUFU WA KRISTO

Sala ya Jioni ya 1.

31. Ee ulimi, utukuze
Mwili wake wa fakhari,
Nayo Damu ya thamani
Yesu aliyoimwaga ;
Yeye, Mkuu wa mataifa,
Anunue ulimwengu.

Tumepewa azaliwe
Na Bikira safi sana,
Akapita duniani
Akipanda mbegu njema ;
Mwisho wa maisha yake
Ndio wa ajabu sana.

Alikaa usiku ule
Na nduguze thenashara,

Mwili Mt.

Akafanya yampasayo
Ya torati ya zamani ;
Kwa mikono yake safi
Akawapa nafsi yake.

Neno, kwa maneno yake,
Alifanya mkate kuwa
Mwili wake mtukufu,
Na divai kuwa Damu ;
Na kwa macho hatuoni,
Bali kwa imani yetu.

Siri hii iliyo kubwa
Tuisujudie vema ;
Ya zamani yamepita,
Mambo ya torati ile ;
Na yasiyoonekana
Tunaona kwa imani.

Utukufu na fakhari
Ina Mungu juu ya yote,
Baba, Mwana, nae Roho,
Nafsi tatu, Mungu mmoja ;
Atukuzwe, asifiwe,
Leo, kesho, na milele. Amin.

¶. Uliwapa chakula cha mbinguni. Halleluya.
R7. Ndicho kilicho kitamu. Halleluya.

Ant. Mag. Ee ajabu ya wema wa Roho yako, Bwana ! unawapa watoto wako chakula kizuri sana cha mbinguni, illi uwaonyeshe wema wako : wenye njaa unawashibisha mema ; wenye mali walioshiba unawaondoa mikono mitupu.

Sala ya Assubuhi.

32. Mbinguni Yesu alitoka,
Lakini asimwache Baba ;
Khuduma yake ikiisha
Kwa kufa kwake yu tayari.

Na mmoja wa Wathenashara
Alimsaliti kwa adui ;
Lakini kwanza wanafunzi
Aliwalisha Mwili wake.

Aliwalisha Mwili wake,
Na kuwanyweshwa Damu yake ;
Chakula hiki kitulinde
Miili, roho, nafsi pia.

Kwa kuzaliwa ndugu yao,
Mezani yu chakula chao ;
Mwokozi wao alipokufa,
Thawabu yao kwa kumiliki.

Dhabihu ya wokofu wetu,
Umetufungulia mbingu ;
Adui watusonga sana,
Kwa nguvu utusaidie.

Ee Mungu mmoja, Nafsi tatu,
Twakutukuza siku zote ;
Utupe raha ya milele
Katika inchi yetu juu. Amin.

∇. Afanya amani mipakani mwako. Halle-
luya.

R7. Akushibisha kwa unono wa nganu.
Halleluya.

Ant. Ben. Mimi ni mkate wa uzima ulio-
shuka kutoka mbinguni : mtu akila mkate huu,
ataishi milele. Halleluya.

Sala ya Jioni ya 2.

UIMBO 31. ∇. na R7. Uliwapa, etc.

Ant. Mag. Ee karamu takatifu! Twampokea
Kristo, twafanya ukumbusho wa mateso yake :
mioyo yetu hujazwa neema, twapewa arabuni
ya utukufu ujao. Halleluya.

Siku za Oktavo.

Sala ya Assubuhi.

UIMBO 32. ∇. na R7. Afanya, etc.

Ant. Ben. Mimi ni mkate. . . .

Sala ya Jioni.

UIMBO 31. ∇. na R7. Uliwapa, etc.

Ant. Mag. Ee karamu takatifu. . . .

S. B. ya II Pentekote.

Sala ya Jioni ya 1.

UIMBO 31.

∇. Aliwalisha kwa unono wa nganu. Halle-
luya.

R7. Akawashibisha kwa asali itokayo mwa-
mbani. Halleluya.

Ant. Mag. Mtu mmoja alifanya karamu
kubwa, akaalika watu wengi : akamtuma mtu-
mishi wake saa ya karamu kwenda kuwaambia
walioalikwa, Njoni, maana vitu vyote vime-
kwisha kuwa tayari. Halleluya.

Moyo Mt.

Sala ya Assubuhi.

UIMBO 32.

℣. Aliwapa nafaka ya mbinguni. Halleluya.

℞. Mwanadamu akala chakula cha mashujaa.
Halleluya.

Ant. Ben. kama Ant. Mag. juu.

Sala ya Jioni ya 2.

UIMBO, ℣. na ℞. kama Sala ya Jioni ya 1. juu.

Ant. Mag. Toka upesi ukaende njia kuu na vichocho vya mji : na maskini, na vilema, na viwete, na vipofu uwashurutishe waingie illi nyumba yangu ipate kujaa. Halleluya.

S. 8. Mwili Mt.

Yote kama Siku Kuu yenyewe.

MOYO MTUKUFU WA BWANA

Sala ya Assubuhi.

33. Ee Yesu, Mkombozi wetu,
Upendo wako wa moyoni
Ulikuvuta uzaliwe,
Utuokoe na Jehanum.

Kwa pendo ulifanya mbingu,
Dunia nyota, na bahari ;
Uliwahurumia baba,
Umezivunja pingu zetu.

Moyo Mt.

Na moyo wako umejaa
Upendo mwingi wa ajabu,
Chemchemi hii ya masamaha
Wanapoteka watu wote.

Huu moyo wako ulipenywa
Kwa mkuki huko Kalvarini,
Na marra ilitoka Damu
Ituoshayo dhambi zote.

Tuimbe Moyo Mtukufu
Wa Bwana wetu Yesu Kristo,
Atupendae hatta mwisho
Tumsifu leo na milele. Amin.

℣. Mwenyewe alitwaa magonjwa yetu.
℞. Na kuchukua maradhi zetu.

Ant. Ben. Alijeruhi kwa makosa yetu, alichubuliwa kwa maovu yetu : adhabu ya amani yetu ilikuwa juu yake na kwa mapigo yake sisi tumepona.

Sala ya Jioni.

UIMBO 33.

℣. Kwa furaha mtateka.
℞. Visimani mwa wokofu.

Ant. Mag. Walipomjia Yesu, wakiona ya kuwa amekwisha kufa, hawakumvunja miguu : lakini askari mmoja kwa mkuki alimchoma ubavu, ikatoka marra damu na maji.

KUTABARUKU KANISA

Sala ya Jioni ya 1.

34. Mji mzuri mbarikiwa,
Raha kwako na amani ;
Juu mbinguni imejengwa,
Mawe yako mawe hayi ;
Malaika, jeshi kubwa,
Wakuleta duniani.

Waja Bibi mtukufu
Arusini kwa Bwanawo ;
Akutaka kwa upendo,
Kwa uzuri wamstahili ;
Boma yako nazo njia
Zote za dhahabu safi.

Wazi ni milango yako,
Killa mmoja lulu moja ;
Huko wenye kumwamini
Bwana Yesu waingia ;
Hawakukataa mateso
Kwa kumpenda Bwana wao.

Hawo ndio mawe hayi,
Kazi yake Fundi mkuu,
Kuyapata, kuyakata,
Kuyaweka vema juu ;
Anataka mawe hayo
Yaipambe nyumba yake.

Sasa asifiwe Baba,
Nae Mwana asifiwe,

Asifiwe Roho pia,
Nafsi tatu, Mungu mmoja ;
Mtukufu na ukuu,
Leo, kesho, na milele. Amin.

V. Hii ndiyo nyumba ya Bwana, imejengwa imara.

R. Msingi wake juu ya mwamba ulio thabiti.

Ant. Mag. Bwana ameitakasa nyumba yake,
kwa kuwa ndiyo nyumba ya Mungu, imeitiwa
Jina lake : ndiyo iliyoandikiwa, Na Jina langu
litakuwa huko, asema Bwana.

Sala ya Assubuhi.

35. Msingi kweli ndio Kristo,
Jiwe kubwa la pembeni ;
Limeteuliwa kuwa
Unganisho la Kanisa ;
Na msaada wa Sayuni,
Tumaini lake pia.

Mji ule mtakatifu,
Upendwao nae Mungu,
Unafurahiwa mno,
Unaimba siku zote ;
Mungu mmoja, Nafsi tatu,
Wamtukuza na kumsifu.

Twakusihi, Bwana, leo
Utujie Kanisani ;
Sala zetu tutoazo
Usikie kwa rehema ;
Mibaraka yako mingi
Ilijaze kao lako.

Kutabaruku Kanisa

Wape watumishi wako
Haja za mioyo yao ;
Wazishike siku zote
Watakazopewa nawe ;
Wamiliki baadae
Na Watakatifu wako.

Sasa asifiwe Baba,
Nae Mwana asifiwe,
Asifiwe Roho pia,
Nafsi tatu, Mungu mmoja ;
Mtukufu na ukuu,
Leo, kesho, na milele. Amin.

Ŷ. na R7. kama Sala ya Jioni ya 1.

*Ant. Ben. Leo wokofu umefika nyumbani
humu : kutoka kwa Mungu.*

Sala ya Jioni ya 2.

UIMBO 34.

*Ŷ. Utakatifu ndio uifaa nyumba yako.
R7. Ee Bwana, milele na milele.*

*Ant. Mag. Panatisha namna gani mahali
hapa : bila shaka hapa ni nyumba ya Mungu, na
huu ni mlango wa mbinguni.*

Siku za Oktavo.

*Yote kama Assubuhi na Jioni ya 2. Walakini
Ŷ. na R7. na Ant. ya Jioni ya 1 zitumike katika
Sala ya Jioni ya 1 ya S. B. katika Oktavo, na
Sala ya Jioni ya 1 ya S. 8. ya Siku Kuu.*

*Aidha, Wakati wa Pasaka Ŷ. na R7. na Ant.
zitirwe Halleluya mwishoni.*

NYIMBO ZA WATAKATIFU

MARIAMU MB.

Sala ya Jioni ya 1.

36. Nyota ya bahari,
Ituongozayo
Hatta bandarini,
Tunakusalimu.

Ee Bikira safi,
Ulipewa neema
Kuwa mama yake
Yeye, Mungu Mwana.

Baada ya salamu
Yake Gabrieli
Tulipata amani
Kwa utii wako.

Mwana wako, Yesu,
Atufungulie
Pingu za Shetani,
Tukapewe nuru.

Alikuchagua
Kuwa mama yake,
Mama, tuombe,
Tusihukumwiwe.

Mariamum Mb.

Bali tuwe safi,
Kwa mfano wako,
Ee Bikira Mama,
Mpole, mnyenyekevu.

Utusaidie
Hapa duniani,
Hatta tukimwona
Yesu kwa furaha.

Asifiwe Yesu,
Mwana wa Bikira,
Nae Baba, nae
Roho Mtakatifu. Amin.

☩. Salamu, Mariamu, umejaa neema.

R7. Bwana yu pamoja nawe.

Ant. Mag. Vizazi vyote wataniita kheri : kwa kuwa aliye hodari amenitendea makuu. Halleluya.

Sala ya Assubuhi.

37. Bikira Mariamu
Ametukuzwa pote,
Aliyepewa neema
Kumzaa Mwokozi wetu.

Kwa kosa lake Hawa
Tulipotea sana ;
Na huyu amekuwa
Mlango wa wokofu.

Katika tumbo lake
Yuaja Kiongozi,

Mariamum Mb.

Na sisi wanadamu
Twaona njia tena.

Wakristo, furahini,
Ajabu ya Uzazi ;
Wapewe watu wote
Wokofu na uzima.

Ee Mwana wa Bikira,
Twakuabudu sana,
Pamoja nae Baba,
Na Roho Mtakatifu. Amin.

☩. Salamu, Mariamu, umejaa neema.

R7. Bwana yu pamoja nawe.

Ant. Ben. U kheri, Mariamu, uliyesadiki : kwa maana yatatimizwa uliyoambiwa na Bwana. Halleluya.

Sala ya Jioni ya 2.

UIMBO, ☩. na R7. kama Sala ya Jioni ya 1. juu.

Ant. Mag. Vizazi vyote wataniita kheri : kwa kuwa Mungu ameutazama unyonge wa mjakazi wake. Halleluya.

Siku za Oktavo.

Yote kama Assubuhi na Jioni ya 2. Walakini ☩. na R7. na Ant. ya Jioni ya 1 zitumike katika Sala ya Jioni ya 1 ya S. B. katika Oktavo, na Sala ya Jioni ya 1 ya S. 8. ya Siku Kuu.

Aidha, katika Antifona Halleluya iachwe tokea Septuagesima hatta Pasaka. Na Wakati wa Pasaka ☩. na R7. zitiwe Halleluya mwishoni.

MTUME AU MTUNGA INJILI

38. Dunia ifurahi sana,
Waitikie Malaika,
Pamoja nao wanadamu
Waimbe sifa za Mitume.

Wa ulimwengu waamuzi,
Na nuru kweli ya dunia,
Saidieni tukiomba
Aturehemu Bwana Kristo.

Funguo mmepewa ninyi
Za mbingu, mtufungulie ;
Twamwomba Mungu neema yake,
Tufunguliwe dhambi zetu.

Maneno yenu yaliponya
Wagonjwa wengi wa zamani ;
Wagonjwa sisi wa mioyo,
Turudishiwe afya zetu.

Na Kristo atakaporudi
Kuuhukumu ulimwengu,
Tushirikishwe sisi nanyi
Furaha zenu za milele.

Kwa Mungu Baba utukufu,
Pamoja nae Mungu Mwana,
Na Mungu Roho Mtakatifu,
Zamani zote za milele. Amin.

Mtume

V. Sauti yao imeenea duniani mwote.
R7. Na maneno yao hatta miisho ya
ulimwengu.

Ant. Watawapelekeni mabarazani, na katika
masunagogi mtapigwa : na mtachukuliwa mbele
a maliwali na wafalme kwa ajili yangu, kuwa
ushuhuda kwao na kwa mataifa.

MTUME AU MTUNGA INJILI

(Wakati wa Pasaka)

39. Khabari za huzuni kuu,
Mitume wanasikitika ;
Watumwa wamemwua Bwana,
Hayupo Yesu, amezikwa.

Khabari za furaha kuu,
Wapewa kwanza wanawake ;
Waambieni ndugu zake,
Hayupo Yesu, kafufuka.

Waenda mbio kwa Mitume
Wasilifiche neno hili ;
Wakakutana nae Yesu
Njiani, wakamsujudia.

Mitume wakashika njia
Waende marra Galilaya,
Wamwone huko mlimani,
Wakaipata haja yao.

Mtume

Daima, Yesu, uwe Wewe
Furaha yetu ya Pasaka ;
Uzima upya umetupa,
Utuokoe na Jehanum.

Ahimidiwe Mungu Baba,
Na Mwana mwenye kufufuka,
Na Roho Mfariji nae,
Zamani, leo, na milele. Amin.

✓. Mfurahieni Bwana, enyi Watakatifu wenye haki. Halleluya.

R7. Mungu amewachagua ninyi kuwa urithi wake. Halleluya.

Ant. Nuru ya daima itawaangaza Watakatifu wako, Ee Bwana : nao watapata uzima wa milele. Halleluya.



SHAHIDI MMOJA

40. Wa Mashahidi Bwana mkuu,
U taji na thawabu juu,
Shahidi wako tukimsifu,
Tupewe na utakatifu.

Matata kwake si kikwazo,
Anasa hakunaswa nazo,
Alizona kuwa taka,
Kashiba sasa mibaraka.

Mateso huyu yalimfaa,
Kazi si kazi kwa shujaa,
Alikufia kwa furaha,
Ee Yesu, ukampa raha.

Tukimtukuza asikari
Wa vita zako, Jemadari,
Rehema zako tupokee,
Makosa utuondolee.

Ee Mungu mmoja, Mtakatifu,
U Nafsi tatu, twakusifu ;
Ufalme, nguvu, na heshima
Ni zako, leo na daima. Amin.

✓. Umemvika taji ya utukufu na heshima.
R7. Umemtawaza juu ya kazi ya mikono yako.

Ant. Mtu atakae kuandama nyuma yangu :
ajikane nafsi yake, ajitwike msalaba wake,
anifuate.

SHAHIDI MMOJA

(*Wakati wa Pasaka*)

41. Wa Mashahidi Bwana mkuu,
U taji na thawabu juu,
Shahidi wako tukimsifu,
Tupewe na utakatifu.

Matata kwake si kikwazo,
Anasa hakunaswa nazo,
Alizona kuwa taka,
Kashiba sasa mibaraka.

Mateso huyu yalimfaa,
Kazi si kazi kwa shujaa,
Alikufia kwa furaha,
Ee Yesu, ukampa raha.

Tukimtukuza asikari
Wa vita zako, Jemadari,
Rehema zako tupokee,
Makosa utuondolee.

Ahimidiwe Mungu Baba,
Na Mwana mwenye kufufuka,
Na Roho Mfariji nae,
Zamani, leo, na milele. Amin.

∇. Ina thamani machoni pa Bwana. Halle-
luya.

R7. Mauti ya Watakatifu wake. Halleluya.

Ant. Mfurahieni Bwana, enyi Watakatifu
wenye haki. Halleluya : Mungu amewachagua
ninyi kuwa urithi wake. Halleluya.

MASHAHIDI WENGI

Sala ya Jioni (*ya 1 na ya 2*).

42. Haya, tuimbe khabari tukufu,
Sifa na heshima ya Mashahidi ;
Kiisha kushinda wapata furaha,
Hawo ni mashujaa.

Ndio waliochukiwa na watu,
Wakadharau anasa na raha ;
Wakitafuta kukufuatisha,
Yesu, Mfalme wao.

Hawakukhofu maneno makali,
Wala kupigwa vibaya na watu ;
Kucha za nyama zikiwararua,
Hawakushindwa kamwe.

Kama kondoo walichinjwa kwa panga,
Walikubali pasipo kununa ;
Walisubiri kwa moyo mkuu,
Wenye dhamiri safi.

Nani aweza kunena thawabu
Ya Mashahidi waliyowekewa ?
Hawo waliokubali mateso
Enzi wapewa juu.

Nasi twaomba, Ee Mungu Mwenyiezi,
Tuondolewe maovu na dhambi ;
Tupe amani tupate daima
Kukutukuza Wewe. Amin.

Mashahidi

℣. Shangilieni, enyi wenye haki.

R7. Pigeni vigelegele vya furaha.

Ant. Mag. Roho za Watakatifu wanafurahi mbinguni, ndio waliofuata nyayo za Kristo : na kwa sababu wamemwaga damu yao kwa ajili ya kumpenda, wanashangilia pamoja na Kristo hatta milele.

Sala ya Assubuhi.

43. Mfalme mkuu wa Mashahidi,
Waliokufa waamini,
Wakadharau ulimwengu,
Uliwaleta kwako juu.

Utege masikio, Bwana,
Usikilize sala zetu,
Utusamehe dhambi zetu,
Utupe na kushinda pia.

Kwa neema yako walishinda
Waungamaji Mashahidi ;
Twaomba kwa unyenyekevu
Dhaifu zetu utuponye.

Kwa Mungu Baba utukufu,
Pamoja nae Mungu Mwana,
Na Mungu Roho Mtakatifu,
Zamani zote za milele. Amin.

℣. Watakatifu waushangilie utukufu.

R7. Waimbe kwa sauti kuu vitandani mwao.

Ant. Ben. Nywele za vichwa vyenu zimehesabiwa zote : Msiogope bassi ; bora ninyi kuliko videge vingi.

MASHAHIDI WENGI

(*Wakati wa Pasaka*)

44. Mfalme mkuu wa Mashahidi,
Waliokufa waamini,
Wakadharau ulimwengu,
Uliwaleta kwako juu.

Utege masikio, Bwana,
Usikilize sala zetu ;
Utusamehe dhambi zetu,
Utupe na kushinda pia.

Kwa neema yako walishinda
Waungamaji Mashahidi ;
Twaomba kwa unyenyekevu
Dhaifu zetu utuponye.

Ahimidiwe Mungu Baba,
Na Mwana mwenye kufufuka,
Na Roho Mfariji nae,
Zamani, leo, na milele. Amin.

℣. Ina thamani machoni pa Bwana. Halleluya.

R7. Mauti ya Watakatifu wake. Halleluya.

Ant. Mfurahieni Bwana, enyi Watakatifu wenye haki. Halleluya : Mungu amewachagua ninyi kuwa urithi wake. Halleluya.

MWUNGAMAJI ALIYE ASKOFU. I

45. Na tumtukuze huyu Mwangamaji
Leo katika ulimwengu wote ;
Alistahili siku hii kwenda
Raha ilipo.

Mnyenyekevu, mcha Mungu, mtawa,
Mwenye upole na maisha safi,
Mwenye huruma, mfadhili wote,
Ndiye wa kheri.

Kheri na sisi tufanane nae,
Tukimwimbia nyimbo za heshima,
Kheri tupate kushiriki nae
Mambo ya mbingu.

Mungu Mwenyiezi, Baba, Mwana, Roho,
Unatawala ulimwengu wote ;
Sifa, heshima, nguvu, utukufu,
Kwako milele. Amin.

∇. Bwana alimpenda akampamba.

R7. Akamvika vazi la utukufu.

*Ant. Vema, mtumishi mwema na amini ;
ulikuwa amini kwa machache : nitakuweka juu
ya mengi, asema Bwana.*

*Wakati wa Pasaka ∇. na R7. na Ant. zitiwe
Halleluya mwishoni.*

MWUNGAMAJI ALIYE ASKOFU. II

46. Kristo, Mchungu wa wachunga wote,
Huyu Askofu twamkumbuka leo,
Tukimheshimu, na kukuletea
Nadhiri zetu.

Mnyenyekevu, mwenye kutawala,
Kwa cheo chake hakutakabari,
Na kwa upole alitwaa mamlaka
Uliyompa.

Wa watu wako baba na mchungu,
Na moyo wake umejaa huruma,
Si mwenye choyo, mpaji, akawapa
Mfano wa wema.

Kwa sala zake atusaidie
Watumwa wako, illi tufikie
Kwako mbinguni, na pamoja nae
Tukuabudu. Amin.

∇. Bwana alimwongoza mwenye haki kwa
njia sawa.

R7. Akamwonyesha ufalme wa Mungu.

*Ant. Bwana alimpenda akampamba, akamvi-
ka vazi la utukufu : akamtia taji penye milango
ya Peponi.*

*Wakati wa Pasaka ∇. na R7. na Ant. zitiwe
Halleluya mwishoni.*

MWALIMU WA DINI

47. Ninyi mianga, Waalimu wetu,
Ninyi ni chumvi ya dunia hii,
Mwatuhifadhi kwa elimu yenu
Tusipotee.

Kwa kazi yenu Kweli ya Injili
Bila makosa imekaa salama,
Mkijaliwa kutufahamisha
Neno la Mungu.

Ninyi vijito vyenye maji safi,
Shamba la Mungu mnanyweshwa vema,
Na killa Mkristo anapata kwenu
Malisho mema.

Yesu Mwokozi, Kweli ya milele,
Ingawa bado hatujasikia
Sauti yako, kwa elimu yao
Tuarifiwe. Amin.

Ÿ. Yu kheri mtu yule umwadibuye, Ee Bwana.
R7. Umfundishae kwa sharia yako.

*Ant. Walio na hekima watang'aa kama
mwangaza wa anga : nao waongozao wengi
kutenda haki kama nyota milele na milele.*

*Wakati wa Pasaka Ÿ. na R7. na Ant. zitiwe
Halleluya mwishoni.*

MWUNGAMAJI ASIYE ASKOFU

48. Yesu Mwokozi, Kweli ya milele,
Wewe U taji ya Watakatifu ;
Umemtukuza huyu Mwangamaji
Kwa wema wako.

Alidharau mambo ya dunia,
Aliungama Wewe Bwana wake,
Alimshinda kwa imani yake
Adui wetu.

Yesu kwa wingi wa upendo wako
Ulimhifadhi, akakaa thabiti ;
Leo twaomba, akituombea,
Tusamehewe.

Mungu Mwenyiezi, Baba, Mwana, Roho,
Unatawala ulimwengu wote ;
Sifa, heshima, nguvu, utukufu,
Kwako milele. Amin.

Ÿ. Bwana alimpenda akampamba.
R7. Akamvika vazi la utukufu.

*Ant. Nitamfananisha na mtu mwenye akili :
aliyejenga nyumba yake juu ya mwamba.*

*Wakati wa Pasaka Ÿ. na R7. na Ant. zitiwe
Halleluya mwishoni.*

MTAWA

49. Bwana Mwenyezi, wateule wako
Wakuletea sala na nadhiri ;
Huzikubali, hivi kwa ajabu
Unawalea.

Mji hawana hapa duniani,
Wanatamani kuuona mbali,
Na kwa utawa, mwisho wa safari,
Kuufikia.

Kwa maumivu Mashahidi wako
Wamezipata taji za mbinguni ;
Kwa kujitenga na dunia hawo
Watazipata.

Yesu Mwokozi, twakusifu sana,
Kwa kuwalea watu wako hivi ;
Nasi tutenge na dunia hii,
Kwako tufike. Amin.

℣. Wazao wake watakuwa hodari duniani.

R. Kizazi cha mwenye adili kitabarikiwa.

Ant. Toka wewe katika inchi yako, na jamaa zako, na nyumba ya baba yako, hatta inchi nitakayokuonyesha : nami nitakufanya kuwa taifa kubwa, nitakubariki.

Wakati wa Pasaka ℣. na R. na Ant. zitiwe Halleluya mwishoni.

BIKIRA

50. Wa Mabikira taji na thawabu,
Ulizaliwa na Bikira safi ;
Na mama yako ndiye peke yake
Mama Bikira.

Kwenye bustani ya upendo wako
Wanajilisha wateule wako,
Wakuimbia nyimbo nzuri sana,
Ndio wa kheri.

Wakufuata killa uendako,
Yesu, Furaha ya Watakatifu ;
Utusikie, na kwa neema yako
Tuwafuate.

Na tumhimidi Baba Mwenyezi,
Na Bwana Yesu, Mwana wa pekee,
Na Mfariji, Roho Mtakatifu,
Mungu milele. Amin.

℣. Neema imemininiwa midomoni mwako.

R. Kwa hiyo Mungu amekubariki hatta milele.

Ant. Njoo, bibi arusi wa Kristo : uipokee taji uliyowekewa tayari na Bwana milele.

Wakati wa Pasaka ℣. na R. na Ant. zitiwe Halleluya mwishoni.

Jan. 25. Kuongoka kwa Paolo, Mtume.

MWANAMKE

51. Leo tuimbe Wanawake wema,
Hawakuona khofu mioyoni,
Kwa wema wao na utawa mwingi
Wametukuzwa.

Kwa pendo lako huyu aliacha
Mali na raha yote ya dunia,
Akitafuta mali ya mbinguni,
Na raha yake.

Aliutiisha mwili kwa kufunga,
Aliilisha roho kwa kusali,
Na nuru yake ya matendo mema
Iliangaza.

Na tumhimidi Baba Mwenyiezi,
Na Bwana Yesu, Mwana wa pekee,
Na Mfariji, Roho Mtakatifu,
Mungu milele. Amin.

¶. Utukufu wako na fakhari yako.

R7. Katika fakhari yako usitawi, uendeleo.

Ant. Ufalme wa mbinguni umefanana na
mtu mfanyi biashara, atafutae lulu nzuri : nae
alipoona lulu moja ya thamani kubwa akaenda
akauza alivyo navyo vyote, akainunua.

*Wakati wa Pasaka ¶. na R7. na Ant. zitiwe
Halleluya mwishoni.*

52. Mtume mkuu, twakukumbuka
Kwa shangwe kuongoka kwako ;
Na Bwana wako twamtukuza,
Aliyekugeuza moyo.

Dameski ulikaribia
Uwafukuze watu wake ;
Mchungu mkuu anavyolinda
Kondoo zake usijue.

Akutazama kwa huruma,
Asema nawe, Jinsi gani
Wanifukuza ? ni vigumu
Kupiga teke mchokoo.

Kwa macho ulimwona Yesu
Katika utukufu wake
Ukaanguka, huna nia
Ya kushindana nae tena.

Akaamuru, ukatii,
Na kwa bidii ukakhubiri
Injili yake duniani
Kwa mataifa yote pia.

Geuza, Bwana, nia zetu,
Tuache ukaidi wetu,
Tukukhudumu kwa bidii,
Kwa mfano wa Mtume wako.

Kwa Mungu Baba utukufu,
Pamoja nae Mungu Mwana,
Na Mungu Roho Mtakatifu,
Zamani zote za milele. Amin.

Y. Ndiwe chombo kiteule, Ee Paolo Mtume
Mtakatifu.

R7. Mkhubiri kweli katika ulimwengu wote.

Ant. Enenda zako, Anania, ukamtafute Saul,
maana anasali : kwa maana huyu ni chombo
kiteule kwangu, alichukue Jina langu mbele
ya mataifa, na wafalme, na wana wa Israeli.

Mar. 19. Yusuf, Mtunza Bwana wetu.

53. Yusuf mtawa, wakushangilie
Na Malaika na Wakristo pia,
Uliyekuwa Mtunza Bwana wetu
Bin Mariamu.

Ulishangazwa hatta Malaika
Akuambie kuwa yule Mtoto,
Mwana wa Mungu, Jina lake Yesu,
Ndiye Mwokozi.

Akazaliwa, nawe ukamtunza,
Aliyotaka mfalme kuyatenda
Hakudiriki, Yesu amekwenda
Misri salama.

Sisi Wakristo, tutakapokufa,
Ndipo mbinguni tutamwona Yesu ;
Umempakata hapa duniani,
Ndiwe wa kheri.

Yesu, Mfalme na Mwokozi wetu,
Twakuabudu, nae Mungu Baba,
Na Mfariji, Roho Mtakatifu,
Mungu milele. Amin.

Y. Kinywa chake mwenye haki hunena
hekima.

R7. Ulimi wake husema hukumu.

Ant. Yusuf alipoamka katika usingizi : aka-
tenda kama Malaika wa Bwana alivyomwagiza,
akamchukua mkewe.

Mar. 24. Gabrieli, Malaika Mkuu.

Tazama UIMBO 63.

Apr. 24. Mnyang'anyi mwenye toba.

(aitwae Dismas)

54. Mchungu mwema wa kondoo,
Unaewatafuta sana
Kondoo waliokupotea,
Mpaka uwaone tena.

Tunamkumbuka siku hii
Kondoo aliyekukimbia,
Ukamtafuta kwa bidii,
Ukampata msalabani.

Upendo wa ajabu huu !
Kuvumilia maumivu
Uipokonye roho yake
Katika nguvu za Shetani.

Yohana Mbatizaji

Katika msalaba wake
Alikuona msalabani ;
Kwa pendo ulimvuta kwako,
Akakukiri Bwana wake.

Na sisi, Bwana, tu kondoo
Wa kundi lako, tuokoe
Kwa msalaba, tukaige
Imani yake ya ajabu.

Ahimidiwe Mungu Baba,
Na Mwana mwenye kufufuka,
Na Roho Mfariji nae,
Zamani, leo, na milele. Amin.

Y. Bwana alimpenda akampamba. Halleluya.
R7. Akamvika vazi la utukufu. Halleluya.

Ant. Mkhalifu mmoja akamwambia mwenzake, Sisi tunalipwa ijara ya haki ya matendo yetu, bali huyu hakutenda neno lisilofaa: Bwana, unikumbuke ujapo katika ufalme wako. Halleluya.

Jun. 24. Kuzaliwa kwa Yohana Mbatizaji.

55. Hatustahili kwa midomo yetu
Kuyatangaza maajabu yako ;
Inahitaji kwanza kutakaswa,
Ee Yohana.

Toka mbinguni aja Gabrieli
Kwa baba yako mle hekaluni,
Akamjulisha kuzaliwa kwako,
Na jina lako.

Yohana Mbatizaji

Hakuamini, akiona shaka,
Marra akawa bubu, asiseme
Hatta ikawa amekupa jina,
Kumbe! asema.

Nawe, tumboni mwake mama yako,
Ulimtambua Bwana ukaruka ;
Na mama zenu walifahamishwa
Fumbo la Mungu.

Na tumhimidi Baba Mwenyiezi,
Na Bwana Yesu, Mwana wa pekee,
Na Mfariji, Roho Mtakatifu,
Mungu milele. Amin.

Sala ya Jioni ya 1.

Y. Palitokea mtu ametumwa kutoka kwa Mungu.

R7. Jina lake Yohana.

Ant. Mag. Zakaria alipoingia katika hekalu la Bwana, alitokewa na Malaika Gabrieli: amesimama upande wa kuume wa madhbahu ya kufukizia.

Sala ya Assubuhi.

Y. Mtoto huyu atakuwa mkuu mbele za Mungu.

R7. Kwa maana mkono wa Bwana u pamoja nae.

Ant. Ben. Zakaria akafunguliwa kinywa, akatabiri, akinena : Atukuzwe Bwana, Mungu wa Israeli.

Petro na Paolo

Sala ya Jioni ya 2.

¶. Mtoto huyu atakuwa mkuu mbele za Mungu.

R7. Kwa maana mkono wa Bwana u pamoja nae.

Ant. Mag. Mtoto aliyezaliwa kwetu ni mkuu kuliko nabii ; kwa khabari zake Mwokozi alinena : Hajaonokea mtu katika wazao wa wanawake aliye mkuu kuliko Yohana Mbatizaji.

Siku za Oktavo.

Yote kama Assubuhi na Jioni ya 2. Walakini ¶. na R7. na Ant. ya Jioni ya 1 zitumike katika Sala ya Jioni ya 1 ya S. B. katika Oktavo.

Jun. 29. Mitume wabarikiwa, Petro na Paolo.

56. Ni Siku Kuu ya utukufu mwingi, Walipopata taji zao Mitume ; Mbinguni wanakaa na kutuita, Huko waliko tufuate nasi.

Funguo za ufalme wa mbinguni Anazo huyu, huyu ilmu yake ; Na sasa wamepata taji, huyu Kwa msalaba, huyu kwa upanga.

Ee Rumi mbarikiwa, ndani yako Imemwagika damu ya Mitume ; Kwa damu yao ya thamani nyingi Heshima na fakhari umepata.

Petro na Paolo

Mwenyiezi Mungu, Baba, Mwana, Roho, Utawalae ulimwengu wote, Heshima kwako, nguvu, utukufu, Twakuhimidi leo na milele. Amin.

Sala ya Jioni ya 1.

¶. Sauti yao imeenea duniani mwote.

R7. Na maneno yao hatta miisho ya ulimwengu.

Ant. Mag. Wewe ndiwe mchungu kondoo, mkuu wa Mitume : wewe ulipewa funguo za ufalme wa mbinguni.

Sala ya Assubuhi.

¶. Walitangaza matendo ya Mungu.

R7. Na kazi zake wakazitafakari.

Ant. Ben. Lo lote utakalolifunga duniani, litafungwa mbinguni : na lo lote utakalolifungua duniani, litakuwa limefunguliwa mbinguni.

Sala ya Jioni ya 2.

¶. Walitangaza matendo ya Mungu.

R7. Na kazi zake wakazitafakari.

Ant. Mag. Leo Simon Petro aliupanda msalaba, Halleluya ; leo mchukua funguo za ufalme alihama kwa furaha amwendee Kristo : leo Paolo Mtume, nuru ya ulimwengu, aliinama kichwa kwa ajili ya Jina lake Kristo, akatiwa taji ya ushahidi. Halleluya.

Siku za Oktavo.

Yote kama Assubuhi na Jioni ya 2. Walakini ¶. na R7. na Ant. ya Jioni ya 1 zitumike katika Sala ya Jioni ya 1 ya S. 8. ya Siku Kuu.

Damu ya thamani

Jul. 1. Damu iliyo ya thamani ya Bwana.

57. Twakusalimu, Bwana Yesu,
Uliyetoa Damu yako,
Kwa mto huu tumeokoka,
Ishara ya upendo wako.

Ulipopigwa mijeledi,
Ulipovikwa taji ile,
Ilipozua misumari
Mikono yako na miguu.

Askari na alipokuja
Msalabani, akapenya
Kwa mkuki wake Moyo wako,
Hii Damu yako ilitoka.

Ingawa tuna dhambi nyingi,
Umetufia, Bwana Yesu,
Na Damu yako ya thamani
Yatusafisha dhambi zote.

Ee Bwana Yesu, umeketi
Kitini pake Mungu Baba,
Uliyetukomboa kwanza,
Twakuhimidi siku zote. Amin.

∇. Umetukomboa, Ee Bwana, kwa damu
yako.

R7. Ukatufanya kuwa ufalme kwa Mungu
wetu.

Ant. Damu ya Mwana Kondoo itakuwa ishara
kwenu, asema Bwana : nami nitakapoiona ile
damu, nitapita juu yenu, lisiwapate pigo lo lote.

Mariamum Magdalene

Jul. 22. Mariamu (wa Magdala), mwenye
toba.

58. Baba Mwenyiezi, Wewe kwenye nuru
Ulimtazama huyu Mariamu,
Amechomeka kwa upendo wake
Yesu Mwokozi.

Kwenye karamu Yesu ameketi,
Kumbe! aleta nardo akampaka,
Akaifuta na miguu yake
Kwa nywele zake.

Hakuogopa penye Msalaba,
Akasimama asimwache Yesu ;
Walipomzika alikhudhuria
Kaburi lake.

Yesu, chemchemi ya upendo wote,
Khatiya zetu utuondolee,
Tujazwe pendo mioyoni mwetu,
Tukae nawe. Amin.

∇. Neema imemiminiwa midomoni mwako.
R7. Kwa hiyo Mungu amekubariki hatta
milele.

Ant. Mariamu alimpaka Yesu miguu, akai-
futa miguu yake kwa nywele zake : nyumba
ikajaa harufu ya yale marhamu.

Aug. 1. Kufungwa kwa Petro, Mtume.

59. Mtume Petro gerezani
Kwa minyororo alifungwa,
Na Malaika akatumwa
Na Bwana wake kumfungua.

Kung'aa Bwana

Mchungu yeye wa kondoo,
Sauti yake wasikia,
Aonya njia ya uzima,
Afukuzia mbali mbweha.

Kwa Mungu Baba utukufu,
Pamoja nae Mungu Mwana,
Na Mungu Roho Mtakatifu,
Zamani zote za milele. Amin.

V. Wewe ndiwe Petro.

R. Na juu ya mwamba huu nitalijenga
Kanisa langu.

Ant. Wewe ndiwe mchungu kondoo, mkuu
wa Mitume : wewe ulipewa funguo za ufalme
wa mbinguni.

Aug. 6. Kung'aa kwa Bwana wetu.

60. Amtafutae Bwana nani ?
Na amtafute juu aliko,
Alama ataona huko
Ya utukufu wa daima.

Ni utukufu wake Mungu
Tuliopewa kuuona,
Hauna mwanzo wala mwisho,
Hakijaumbwa kitu, upo.

Wa Wayahudi Mfalme huyu,
Wa mataifa yote pia,
Mtoto wa ahadi ndiye,
Mzao wake Ibrahimu.

Jina Takatifu

Washuhudia manabii
Wawili, Musa na Eliya,
Na Mungu Baba ashuhudu,
Akiamuru tumsikie.

Ee Yesu, utukufu wako
Tumeuona, twakusifu,
Pamoja nae Mungu Baba,
Na Mungu Roho Mtakatifu. Amin.

V. Ulionekana mtukufu machoni pa Bwana.

R. Kwa sababu Bwana amekuvika uzuri.

Ant. Sauti ilitoka katika lile wingu, ikinena :
Huyu ni Mwanangu, mpendwa wangu, niliye-
pendezwa nae ; msikieni Yeye. Halleluya.

Aug. 7. Jina Takatifu, YESU.

61. Ee Yesu, tukikukumbuka
Mioyo imejaa furaha ;
Lakini ukiwapo nasi
Baraka hii hupita yote.

Kuimba neno hatuwezi
Lililo tamu kama Yesu,
Kulisikia ni kuzuri,
Kutamu kulitafakari.

U tumaini peke yako
La wakosaji wenye toba,
Na wote wakutafutao
Ulivyo mwema wamejua.

Msalaba Mt.

Lakini wenye kukupata
Upendo wako wameonja,
Na hawo wamejua kweli
Ajabu ya upendo ule.

Ee Yesu, uwe shangwe letu,
Thawabu yetu utakuwa,
Twakutukuza siku zote,
Na kuliimba Jina lako. Amin.

Ÿ. Jina la Bwana lihimidiwe. Halleluya.

R7. Tangu leo na hatta milele. Halleluya.

Ant. Utamwita Jina lake Yesu : maana, ndiye atakaewaokoa watu wake na dhambi zao. Halleluya.

Sep. 14. Msalaba Mtakatifu.

Sala ya Jioni (*ya 1 na ya 2.*).

UIMBO 22.

Ÿ. Ishara hii ya Msalaba itakuwako mbinguni.

R7. Atakapokuja Bwana kuuhukumu ulimwengu.

Ant. Mag. Ee Msalaba mbarikiwa : ndiwe peke yako uliyestahili kumchukua Mfalme wa mbinguni, Bwana wetu. Halleluya.

Sala ya Assubuhi.

UIMBO 21.

Ÿ. Twakuabudu, Ee Kristo, twakuhimidi.

R7. Maana kwa Msalaba wako umeukomboa ulimwengu.

Ant. Ben. kama Ant. Mag. juu.

Mikael

Sep. 29. Mikael, Malaika Mkuu, na Malaika zote.

Sala ya Jioni (*ya 1 na ya 2.*).

62. Wa Baba Mwanga na Fakhari,
Uzima wetu wa rohoni,
Mkaa palipo Malaika
Wamezunguka kiti chako.

Kwa amri yako elfu elfu
Tayari kukushindania,
Bendera yao Msalaba,
Achukuae ni Mikael.

Mikael alimtupa Joka
Katika giza la Jehanum,
Mishale yake ni ya moto,
Umeme wako wa mbinguni.

Shetani na majeshi yake,
Kwa mfano wa Mikael Mkuu,
Tumshinde, tustahili nasi
Kuvikwa taji ya fakhari.

Kwa Mungu Baba utukufu,
Pamoja nae Mungu Mwana,
Na Mungu Roho Mtakatifu,
Zamani zote za milele. Amin.

Ÿ. Malaika alisimama mbele ya madhbahu.
R7. Mwenye chetezo cha dhahabu mkononi mwake.

Mikael

Ant. Mag. Yohana alipokuwa akitazama siri takatifu, Mikael, Malaika Mkuu, alipiga panda : utusamehe, Ee Bwana Mungu wetu, Wewe ukifunguae kitabu na kuzivunja muhuri zake. Halleluya.

Sala ya Assubuhi.

63. Yesu Mwokozi, Mkuu wa Malaika,
Muumba wetu, Mtawala sisi,
Utujalie kuipanda ngazi
Tukufikie.

Na aje kwetu Mikaeli mkubwa,
Yu Jemadari wa majeshi yako,
Aifukuze vita mbali nasi,
Tuwe na raha.

Atufikie Gabrieli mjumbe,
Mleta khabari za wokofu wetu,
Awakimbize jeshi la Shetani,
Tusiwakhofu.

Umpeleke Rafaeli mwema,
Msaidia, mwenye shauri nae,
Atuongoze hapa duniani
Tusipotee.

Utujalie hayo tuombayo,
Mungu Mwenyiezi, Baba, Mwana, Roho,
Wakuhimidi Malaika, watu,
Viumbe vyote. Amin.

Malaika Walinzi

Ÿ. Malaika alisimama mbele ya madhbahu.
R7. Mwenye chetezo cha dhahabu mkononi mwake.

Ant. Ben. Kukawa kimya mbinguni, Joka alipokifanya vita : na Mikael akafanya vita nae, akamshinda. Halleluya.

[Mar. 24. Gabrieli, Malaika Mkuu.

UIMBO 63. *Ÿ. na R7.* Malaika, etc.

Ant. Malaika Gabrieli alimjia Mariamu, aka-sema : Salamu, uliyepewa neema, Bwana yu pamoja nawe ; umebarikiwa wewe katika wanawake.

Okt. 24. Rafael, Malaika Mkuu.

UIMBO 63. *Ÿ. na R7.* Malaika, etc.

Ant. Mimi ni Rafael, Malaika, nisimamae mbele za Mungu : nanyi mhimidini Bwana mkayakhubiri mambo yake yote ya ajabu.]

Okt. 2. Malaika Walinzi.

64. Twaimba leo Malaika
Walinzi, wenye kazi njema
Ya kutulinda duniani,
Tusishawishwe na Shetani.

Shetani na wenzake wote,
Walipokosa kwa kiburi,
Walifukuzwa, wakatupwa
Katika moto wa Jehanum.

Watakatifu Wote

Na siku hizi wanataka
Kuwapoteza waamini,
Kwa hila nyingi na werevu
Wakitunasa kwa mitego.

Ee Mlinzi wangu, nakuita
Wakati wa kujaribiwa,
Dhaifu mimi, namwogopa
Shetani, nisishindwe nae.

Utatu Mtakatifu Mkuu,
Twakuhimidi siku zote,
Utujalie, twakuomba,
Tulindwe leo na daima. Amin.

℣. Mbele za Malaika nitakuimba zaburi.

℞. Nitasujudu nikikabili hekalu lako takatifu.

Ant. Hawo wote ni roho zitumikazo : wakitu-mwa kuwakhudumu wale watakaourithi wokofu.

Okt. 24. Rafael, Malaika Mkuu.

Tazama UIMBO 63.

Nov. 1. Watakatifu wote.

65. Ee Kristo, Mkombozi mwema,
Tulinde hapa duniani,
Upendezwae tuombewe
Na Mama yako Mtakatifu.

Daraja kenda, Malaika,
Watukingie killa siku
Mabaya tupatayo hapa,
Ya leo na yanayokuja.

Watakatifu Wote

Nabii wa Neno la milele,
Mitume nao wasiache
Kutuombea kwa Mwamuzi,
Tusamehewe dhambi zetu.

Na jeshi kuu la Mashahidi,
Waungamaji watukufu,
Kwa sala nyingi watuvute
Tufike huko juu waliko.

Jamii ya Mabikira safi,
Na Wanawake mashuhuri,
Watakatifu wote pia
Watuombe tuwafikie.

Adui asi afukuzwe,
Asiwadhuru waamini,
Tumpe Kristo kwa umoja
Sifa zilizo haki yake.

Kwa Mungu Baba utukufu,
Pamoja nae Mungu Mwana,
Na Mungu Roho Mtakatifu,
Zamani zote za milele. Amin.

Sala ya Jioni ya 1.

℣. Shangilieni, enyi wenye haki.

℞. Pigeni vigelegele vya furaha.

Ant. Mag. Wamevikwa mavazi meupe,
wakilia kwa sauti kuu, wakisema : wokofu una
Mungu wetu, aketiye katika kiti cha enzi, na
Mwana Kondoo.

Watakatifu Wote

Sala ya Assubuhi.

¶. Watakatifu waushangilie utukufu.

R7. Waimbe kwa sauti kuu vitandani mwao.

Ant. Ben. Wakusifu Wewe jamii tukufu ya Mitume, shirika lenye sifa la Manabii, jeshi la Mashahidi waliovaa mavazi meupe : Watakatifu na wateule wote kwa sauti moja wakukiri, Ee Utatu Mtukufu, Mungu mmoja.

Sala ya Jioni ya 2.

¶. Watakatifu waushangilie utukufu.

R7. Waimbe kwa sauti kuu vitandani mwao.

Ant. Mag. Ee ajabu ya utukufu wa ufalme ule! Ndipo wanapofurahi Watakatifu wote pamoja na Kristo : wamevikwa nguo nyeupe, wanamfuata Mwana Kondoo killa aendako.

Siku za Oktavo.

Yote kama Assubuhi na Jioni ya 2. Walakini ¶. na R7. na Ant. ya Jioni ya I zitumike katika Sala ya Jioni ya I ya S. B. katika Oktavo, na Sala ya Jioni ya I ya S. 8. ya Siku Kuu.



ANTIFONA ZA SIKU ZA BWANA

Antifona hizi zaweza kutumika katika Makanisa yenye kawaida ya kuimba.

S. B. ya II Ufunuo.

Ant. Mag. Hatta divai ilipowatindikia, Yesu aliwaambia wajalize mabalasi maji : yakageuka kuwa divai.

S. B. ya III Ufunuo.

Ant. Mag. Bwana, ukitaka waweza kunitakasa : nae Yesu akasema, Nataka, takasika.

S. B. ya IV Ufunuo.

Ant. Mag. Bwana, tuokoe, tunaangamia : uamuru, Mungu, ufanye utulivu.

S. B. ya V Ufunuo.

Ant. Mag. Yakusanyeni kwanza magugu, myafunge matita matita, mkayachome : bali nganu ikusanyeni ghalani mwangu, asema Bwana.

S. B. ya VI Ufunuo.

Ant. Mag. Ufalme wa mbinguni umefanana na chachu aliyotwaa mwanamke : akaisetiri katika pishi tatu za unga, hatta ukachacha wote pia.

S. B. ya Septuajesima.

Ant. Mag. Mwenye nyumba aliwaambia wakulima, Mbona mmesimama hapa mchana kutwa bila kazi? Wakamwambia, Kwa sababu

Siku za Bwana

hakuna mtu aliyetuajiri : Enendeni na ninyi katika shamba la mizabibu, na iliyo haki nitakupeni.

S. B. ya Seksajesima.

Ant. Mag. Ninyi mmejaliwa kuzijua siri za ufalme wa Mungu : bali wengineo kwa mifano, aliwaambia Yesu wanafunzi wake.

S. B. ya Kwinkwajesima.

Ant. Mag. Yesu alisimama, akaamuru kipofu aletwe kwake, akamwuliza, Wataka nikufanyie nini? Bwana, nipate kuona : Yesu akamwambia, Upewe kuona, imani yako imekuponya. Marra akapata kuona, akamfuata, akimtukuza Mungu.

S. B. ya III Pentekote.

Ant. Mag. Mwanamke gani aliye na rupia kumi, akipotewa na rupia moja : asiyewasha taa, na kuifagia nyumba, akitafuta kwa bidii, hatta atakapoiona?

S. B. ya IV Pentekote.

Ant. Mag. Bwana, tulisumbuka usiku kucha, tusipate kitu : illakini kwa neno lako nitazishusha nyavu.

S. B. ya V. Pentekote.

Ant. Mag. Ukileta sadaka yako madhbahuni, na huku ukikumbuka ya kuwa ndugu yako ana neno juu yako : iache sadaka yako mbele ya madhbahu, nenda zako, kwanza patana na ndugu yako, kiisha rudi utoe sadaka yako.

Siku za Bwana

S. B. ya VI Pentekote.

Ant. Mag. Nawahurumia makutano kwa sababu yapata siku tatu wamekaa nami, wala hawana kitu cha kula : hatta nikiwaaga waende zao nyumbani kwao wanafunga, watazimia njiani.

S. B. ya VII Pentekote.

Ant. Mag. Mti mwema hauwezi kuzaa matunda hafifu, wala mti uliopea kuzaa matunda mazuri : Killa mti usiozaa tunda zuri hukatwa ukatupwa motoni.

S. B. ya VIII Pentekote.

Ant. Mag. Nifanyeje, kwa maana bwana wangu ananiondolea uwakili? Kulima siwezi, kuomba natahayari : Nimekwisha kujua nitakalotenda, illi, nitolewapo katika uwakili, wani-karibishe nyumbani mwao.

S. B. ya IX Pentekote.

Ant. Mag. Imeandikwa, Nyumba yangu itakuwa nyumba ya sala : bali ninyi mmeifanya kuwa pango la wanyang'anyi. Akawa aki-fundisha killa siku hekaluni.

S. B. ya X Pentekote.

Ant. Mag. Hvyu alishuka nyumbani kwake amepata kibali kuliko yule : kwa maana killa ajikwezae atadhilika, nae ajidhiliye atakwezwa.

S. B. ya XI Pentekote.

Ant. Mag. Ametenda yote vizuri : viziwi awafanya wasikie, na bubu waseme.

S. B. ya XII Pentekote.

Ant. Mag. Kulikuwa na mtu akishuka kutoka Yerusalemi kwenda Yeriko ; akaangukia katika mikono ya wanyang'anyi : wakamvua nguo zake, wakamtia jeraha, wakaenda zao, wakamwacha nussu ya kufa.

S. B. ya XIII Pentekote.

Ant. Mag. Mmoja wao akiona ya kuwa amepona : alirudi akimtukuza Mungu kwa sauti kuu.

S. B. ya XIV Pentekote.

Ant. Mag. Utafuteni kwanza ufalme wa Mungu, na haki yake : na haya yote mtazidishiwa.

S. B. ya XV Pentekote.

Ant. Mag. Nabii mkuu ametokea kwetu : na Mungu amewajilia watu wake.

S. B. ya XVI Pentekote.

Ant. Mag. Ukiitwa arusini, enenda ukaketi mahali pa chini ; illi aliyekuita akuambie, Rafiki yangu, jongea huku mbele : ndipo utakapokuwa na heshima machoni pao wote waketio pamoja nawe.

S. B. ya XVII Pentekote.

Ant. Mag. Mwaonaje katika khabari za Kristo? Yu mwana wa nani? Wakamwambia, Wa Daudi : Yesu akawaambia, Imekuwaje bassi Daudi katika Roho kumwita Bwana, akinena, Bwana alimwambia Bwana wangu, Keti mkono wangu wa kuume?

S. B. ya XVIII Pentekote.

Ant. Mag. Mwenye kupooza alichukua kitanda chake alichokilalia, akimtukuza Mungu : makutano wakimwona, wakamtukuza Mungu.

S. B. ya XIX Pentekote.

Ant. Mag. Alipoingia mfalme kuwatazama wageni, akaona mle mtu mmoja asiyevaa vasi la arusi : Akamwambia, Rafiki, uliingiaje humu nawe huna vazi la arusi ?

S. B. ya XX Pentekote.

Ant. Mag. Baba alifahamu ya kuwa ni saa ileile aliyoambiwa na Yesu, Mwana wako yu hayi : Akaamini yeye na nyumba yake yote.

S. B. ya XXI Pentekote.

Ant. Mag. Ewe mtumishi mwovu, nalikusa-mehe deni ile yote, uliponisihi : nawe, je, haikukupasa kumrehemu mjoli wako, kama mimi nilivyokurehemu wewe ?

S. B. ya XXII Pentekote.

Ant. Mag. Mlipeni Kaisari yaliyo ya Kaisari : na Mungu yaliyo ya Mungu.

S. B. ya XXIII Pentekote.

Ant. Mag. Yesu aligeuka, akamwona, akamwambia : Jipe moyo mkuu, binti yangu, imani yako imekuponya.

S. B. kabla ya Majilio.

Ant. Mag. Amin, narwaambieni, Hakitapita kizazi hizi, hatta yatakapokuwa haya yote : Mbingu na inchi zitapita ; bali maneno yangu hayatapita kamwe, asema Bwana.

INDEX

HYMNS.

A solis ortus cardine	13
Ad regias Agni dapes	25
Angularis fundamentum	35
Auctor beate saeculi	33
Audi benigne Conditor	20
Aurora caelum purpurat	24
Ave maris stella	36
Beata nobis gaudia	28
Caelestis urbs Jerusalem	34
Caeli Deus sanctissime	6
Christe pastorum	46
Christe sanctorum	63
Creator alme siderum	11
Crudelis Herodes	17
Custodes hominum	64
Decora lux aeternitatis	56
Deus Creator omnium	9
Deus tuorum militum	14, 40, 41
Ecce jam noctis	1
En clara vox redarguit	10
Exultet orbis gaudiis	15, 38
Fortem virili pectore	51
Hominis superne Conditor	8
Immense caeli Conditor	4
Iste Confessor	45

Jam sol recedit	29
Jesu corona celsior	48
Jesu corona Virginum	50
Jesu dulcis memoria	61
Jesu Redemptor omnium	12
Lucis Creator optime	2
Lustra sex qui jam peregit	21
Magnae Deus potentiae	7
Mchungwa mwema wa kondoo	54
Miris modis repente liber	59
Mtume mkuu twakukumbuka	52
Nunc Sancte nobis Spiritus	3
O gloriosa Virginum	37
O sol salutis	19
O sola magnarum urbium	18
Pange lingua	31
Pater superni luminis	58
Placare Christe servulis	65
Quicumque Christum quaeritis	60
Rector potens verax Deus	page 18
Rex gloriose Martyrum	43, 44
Salutis humanae Sator	26
Salvete Christi vulnera	57
Salvete flores Martyrum	16
Sanctorum meritis	42
Te Joseph celebrent	53
Te lucis ante terminum	page 47
Te splendor et virtus	62
Telluris alme Conditor	5
Tristes erant Apostoli	39
Tu Trinitatis Unitas	30
Tua beandos gloria	49

Ut queant laxis	55
Veni Creator Spiritus	27
Verbum supernum prodiens	32
Vexilla regis prodeunt	22
Vos succensa Deo	47

*Imprinted in Great Britain at the
Mayflower Press, Plymouth, for the
Society of SS. Peter & Paul, Ltd.*